**12 APRILI, 2022**

**BUNGE LA TANZANIA**

**MAJADILIANO YA BUNGE**

**MKUTANO WA SABA**

**Kikao cha Tano – Tarehe 12 Aprili, 2022**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Mwenyekiti (Mhe. David M. Kihenzile) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tukae. Katibu!

**NDG. PAMELA PALLANGYO – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZA KUWASILISHA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA NA VIJANA (MHE. UMMY H. NDERIANANGA):**

Taarifa ya Matoleo ya Gazeti la Serikali pamoja na Nyongeza zake yaliyochapishwa tangu Mkutano wa Bunge uliopita kama ifuatavyo: -

Toleo Na. 05 la Tarehe 04 Februari, 2022;
Toleo Na. 06 la Tarehe 11 Februari, 2022;
Toleo Na. 07 la Tarehe 18 Februari, 2022;
Toleo Na. 08 la Tarehe 25 Februari, 2022;
Toleo Na. 09 la Tarehe 04 Machi, 2022;
Toleo Na. 10 la Tarehe 11 Machi, 2022;
Toleo Na. 11 la Tarehe 18 Machi, 2022;
Toleo Na. 12 la Tarehe 25 Machi, 2022;
Toleo Na. 13 la Tarehe 01 Aprili, 2022.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Ummy Hamis Nderiananga. Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:**

Ripoti ya Mwaka ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Ukaguzi wa Serikali Kuu kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 *(The Annual General Report of the Controller and Auditor General on the Audit of Central Government for the Financial Year 2020/2021)*.

Ripoti ya Mwaka ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 *(The Annual General Report of the Controller and Auditor General on the Audit of Development Projects for the Financial Year 2020/2021)*.

Ripoti ya Mwaka ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Ukaguzi wa Mashirika ya Umma kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 *(The Annual General Report of the Controller and Auditor General on the Audit of Public Authorities and Other Bodies for the Financial Year 2020/21)*

Ripoti ya Jumla ya Mwaka ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Ukaguzi wa Ufanisi kwa Kipindi kinachoishia tarehe 31 Machi, 2022 *(The Annual Report of the Controller and Auditor General on the Performance Audit for the Period ending 31st March, 2022)*

Ripoti ya Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Utoaji wa Fedha na Usimamizi wa Mifuko na Programu za Serikali za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi *(Performance Audit Report on Financing and Management of Government Funds and Programs)*.

Ripoti ya Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Usimamizi wa Miradi ya Maendeleo ya Ujenzi inayotekelezwa kwa Fedha za Mikopo *(Performance Audit Report on the Management of Construction Development Projects Financed Through Loans)*.

Ripoti ya Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa Mapendekezo ya Kaguzi za Ufanisi zilizofanyika na kuwasilishwa Bungeni Mwezi Aprili, 2017 *(Follow – Up Report on the Implementation of the Controller and Auditor General's Recommendations for the Performance Audit Reports issued and tabled before the Parliament in April, 2017.;*

Ripoti Kuu ya Mwaka ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya Ukaguzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 *(The Annual General Report of the Controller and Auditor General on the Audit of Local Government Authorities for the Financial Year 2020/2021)*.

Ripoti ya Ukaguzi wa Ufanisi katika ya Usimamizi na Uhifadhi wa Mifumo ya Ekolojia ya Ardhi Oevu (*Performance Audit Report on the Management of Conservation and Protection of Wetland Ecosystems in Tanzania)*

Ripoti ya Mwaka ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Ukaguzi wa Mifumo ya TEHAMA kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 *(The Annual General Report of the Controller and Auditor General on the Audit of Information Systems for the Financial Year 2020/2021)*.

Ripoti ya Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Usimamizi na Utoaji wa Huduma za Miundombinu ya Mahabusu na Magereza *(Performance Audit Report on Administration and Provision of Remands and Prisons Infras*tructure).

Ripoti ya Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Usimamizi wa Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu *(Performance Audit Report on the Allocation and Disbursement of Higher Education Students' Loans)*.

Ripoti ya Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Usimamizi wa Usajili wa Biashara na Utoaji wa Leseni *(Performance Audit Report on the Business Registration and Licensing)*.

Ripoti ya Ukaguzi wa Ufanisi katika Utekelezaji wa Udhibiti wa Shughuli za Vipimo *(Performance Audit Report on Implementation of Control Activities on Measurements)*.

Ripoti ya Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Usimamizi wa Mifumo ya Haki Jinai *(Performance Audit Report on the Criminal Justice System in Tanzania)*.

Ripoti ya Ukaguzi wa Ufanisi katika Usimamizi wa Ukarabati wa Barabara *(Performance Audit on the Management of Maintenance of Roads)*.

Ripoti ya Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Usimamizi wa Mapato katika Sekta ya Madini *(Performance Audit Report on the Management of Mechanisms for Revenue Collection in the Mining Sector)*.

Ripoti ya Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Uendeshaji na Utangazaji wa Sekta ya Utalii Nchini *(Performance Audit Report on the Development and Promotion of Tourism Sector in Tanzania)*.

Ripoti ya Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Usimamizi wa Makumbusho na Maeneo ya Urithi wa Utamaduni Nchini *(Performance Audit Report on the Management of National Museums and Cultural Heritage Sites in Tanzania)*.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango Mheshimiwa Hamad Hassan Chande. Katibu!

**NDG. EMMANUEL MPANDA- KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tutaanza na maswali Ofisi ya Rais TAMISEMI, sasa namwita Mheshimiwa Jacqueline Kainja Andrea ambapo swali lake litaulizwa na Mheshimiwa Nicolaus Ngasa Mbunge wa Igunga.

Na. 40

**Hitaji la Shule Nyingine ya Msingi Kata ya Ng'ambo – Tabora Mjini**

**MHE. NICHOLAUS G. NGASSA K. n. y. MHE. JACQUELINE K. ANDREA** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Shule nyingine ya Msingi katika Kata ya Ng'ambo Tabora Mjini kwani Kata hiyo ni kubwa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri – TAMISEMI, Mheshimiwa David Silinde

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jacqueline Andrea Kainja Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli shule nyingi za msingi hapa nchini zina wanafunzi wengi wanaozidi kiwango katika shule. Hali hiyo pia ni matokeo ya utekelezaji wa Sera ya Elimu Msingi bila malipo iliyoanza utekelezaji wake mwaka 2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Kata Ng'ambo ina shule moja ya msingi yenye madarasa 17 ambayo yanahudumia wanafunzi 2,408. Aidha, ili kukabiliana na ongezeko la wanafunzi katika Kata hiyo Halmashauri ya Manispaa ya Tabora kwa mwaka wa fedha 2022/2023 imetenga Shilingi Milioni 50 za mapato ya ndani kwa ajili ya ujenzi madarasa mawili ya shule mpya ya msingi inayotarajiwa kujengwa katika eneo la Kilimani katika Kata hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali katika mwaka wa fedha 2022/2023 itatenga fedha ya ujenzi wa madarasa katika shule mpya ya msingi eneo la Kilimani kupitia programu ya *EP4R*.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nicholaus Ngassa Mbunge wa Igunga swali la nyongeza.

**MHE. NICHOLAUS G. NGASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto iliyopo kwenye shule ya msingi Ng'ambo Tabora ni sawa na changamoto iliyopo kwenye shule ya msingi Igurubi ambayo ni Makao Makuu ya Tarafa ya Igurubi Jimbo la Igunga. Tunayo shule ya msingi ambayo kwa sasa ina wanafunzi wengi mpaka imezidiwa, kwa hiyo tunaomba pia Serikali katika utatuzi wa changamoto hizi iweze kuangalia pia shule ya msingi Igurubi ili iweze kulipatia ufumbuzi wa tatizo hili na changamoto hii ili wanafunzi wetu wasome kwa uhuru?*(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Nicholaus Ngassa Mbunge wa Igunga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nae ameeleza tu kwamba katika Jimbo lake la Igunga Tarafa ya Igurubi kuna Shule ya Msingi Igurubi ambayo na yenyewe ina wanafunzi wengi. Nimhakikishie tu kwamba moja ya mpango wa Serikali sasa hivi ni kutapisha shule zote zenye wanafunzi zaidi ya 2000 na ndio maana tuko katika mkakati wa kutafuta fedha na tumezitambua shule zote ambazo zina changamoto hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo mpango huu utakapokamilika maana yake tutawafikia na wao. ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kakunda swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami ningependa niongeze hapo swali la nyongeza, kwa kuwa Serikali imekiri hapa kwamba shule nyingi zimezidiwa na wanafunzi kwa nini Serikali sasa isitangaze kwamba hapa Tanzania tuna upungufu wa shule badala ya kuendelea kutangaza kwamba tuna upungufu wa madarasa peke yake?*(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri TAMISEMI majibu

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa George Kakunda Mbunge wa Sikonge, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la Mheshimiwa Mbunge tu ni kwamba anataka kufahamu tutangaze kwamba tuna uhaba wa shule na siyo

madarasa. Nimhakikishie tu kwamba Serikali inatambua changamoto zote, katika baadhi ya maeneo tuna changamoto ya madarasa na kuna baadhi ya maeneo tuna changamoto ya shule, ndiyo maana katika maeneo ambayo yana changamoto ya shule Serikali tunapeleka fedha kwa ajili ya ujenzi wa shule mpya, kwa hiyo hatuwezi kutangaza kama janga kwa sababu Serikali ipo kazini na inafanya kazi kutatua hizi changamoto ambazo Mheshimiwa Mbunge ameainisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.*(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante tunaendelea. Sasa namwita Mheshimiwa Oliver Daniel Semuguruka Mbunge wa Viti Maalum aulize swali lake.

Na. 41

**Njia Mbili katika Barabara ya Bandarini hadi Rwamishenye na CRDB mpaka Njiapanda ya Kashai**

**MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itajenga njia mbili katika barabara ya Bandarini hadi Rwamishenye na *CRDB* mpaka Njiapanda ya Kashai ili kuondoa msongamano?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais -TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Oliver Daniel Semuguruka, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Bandarini – Rwamishenye yenye urefu wa kilomita 4.6 inafanyiwa usanifu wa kina ulioanza tarehe 22 Machi, 2022 kwa ajili ya kuwa Barabara ya njia mbili. Kazi ya usanifu inafanywa na Mhandisi Mshauri *Luptan Consult Ltd* kwa gharama ya Shilingi Milioni 70.05 na kazi inategemewa kukamilika mwezi Mei, 2022. Kazi za ujenzi zitaanza mara baada ya upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usanifu wa barabara ya *CRDB* – Njiapanda ya Kashai yenye urefu wa kilomita 0.5 itaanza mara tu kazi ya usanifu wa kina wa barabara ya Bandarini – Rwamishenye utakapokamilika na fedha za usanifu zitakapopatikana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Oliver Daniel Semuguruka Mbunge wa Viti Maalum Kagera, swali la nyongeza

**MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali lakini ninayo maswali madogo mawili ya nyongeza.

Ili kuweka taarifa sahihi kwa wananchi wangu wa Bukoba Mjini. Je, Serikali kupitia *TARURA* ina maana kuwa barabara hizi zimehamishiwa *TARURA* badala ya *TANROADS* nilitaka kujua hilo maana hizi barabara ni za *TANROADS* siyo za *TARURA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili kumekuwepo na malalamiko mengi ya fidia kwenye miradi ya aina hii. Je, Serikali inatoa ahadi gani kwa wananchi wangu wa Bukoba Mjini endapo wakipitiwa katika hii barabara watapata fidia kwa uharaka?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa David Silinde Naibu Waziri TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali madogo mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Oliver Daniel Semuguruka, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba anasema barabara hii huenda imehamishwa kutoka *TANROADS* kwenda *TARURA,* nimwambie tu kwamba hapana ni kwa sababu Serikali hii ni moja na inafanya kazi kwa pamoja nasi Ofisi ya Rais, TAMISEMI kupitia *TARURA* na *TANROADS* tunafanya kazi kwa umoja. Kwa hiyo, kikubwa katika swali lake la msingi alilouliza hapa juu ya kuhakikisha usanifu unakamilika na ujenzi wa barabara unaanza vitafanyika kama ambavyo ameainisha hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili kuhusu fidia anataka tu mara baada ya usanifu ni wananchi wale walipwe fidia kwa wakati, Serikali italipa fidia kulingana na tathmini ambayo itafanywa katika maeneo hayo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri naomba ukaketi ahsante kwa majibu mazuri. Tunaendelea na Ofisi ya Makamu wa Rais Muungamo na Mazingira sasa namuita Mheshimiwa Omar Ali Omar Mbunge wa Wete, aulizwe swali lake.

Na. 42

**Ukataji wa Mikoko na Uvunaji wa Matumbawe**

**MHE. OMAR ALI OMAR** aliuliza:-

Je, Serikali imejipanga vipi kukabiliana na uharibifu unaotokana na ukataji mikoko na uvunaji wa matumbawe ili kuvinusuru visiwa visitoweke?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Omar Ali Omar, Mbunge wa Wete, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kukabiliana na changamoto iliyoainishwa na Mheshimiwa Mbunge Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar zimekuwa zikichukua juhudi mbalimbali za kisera, kisheria pamoja na kuandaa miongozo mbalimbali ya utunzaji wa mazingira ya baharini ili kuhakikisha uharibifu wa mazingira ya bahari unadhibitiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miongoni mwa juhudi hizo ni kama zifuatazo:

Kwanza, kujenga uelewa kwa wanajamii juu ya utunzaji wa mazingira na rasilimali za bahari ikiwemo uhifadhi wa mikoko na matumbawe.

Pili, upandaji wa mikoko na matumbawe katika maeneo yaliyoathirika kwa kutumia njia mbalimbali endelevu na za kitaalamu. Kwa mfano upandaji wa hekta Saba za mikoko Unguja na hekta 10 Pemba kwa mwaka 2020 – 2021 pamoja na kuweka matumbawe bandia 90 Unguja na Pemba.

Jambo lingine ni ushirikishwaji wa jamii katika kusimamia maeneo ya mikoko na matumbawe ikiwemo kuanzisha hifadhi ndogondogo za kijamii katika maeneo ya Kukuu, Fundo, Makoongwe kwa Kisiwa cha Pemba na maeneo ya Mtende, Tumbatu na Kizimkazi kwa upande wa Kisiwa cha Unguja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Omar Ali Omar Mbunge wa Wete, swali la nyongeza.

**MHE. OMAR ALI OMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa hii ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la kwanza ni kwamba pamoja na juhudi kubwa za Serikali za kuangalia hifadhi ya mazingira lakini swali la kwanza ni kwamba Serikali ina mpango gani wa kuviwezesha vikundi vinavyojishughulisha na upandaji wa mikoko pamoja na matumbawe?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, katika visiwa vidogovidogo vilivyopo Pemba Kisiwa cha Mtambwi Mkuu ni moja kati ya visiwa ambavyo vinaathirika kwa hali ya juu kabisa.

Je, Serikali ina mpango gani kukihami kisiwa kile ili kisipotee katika sura ya dunia? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Khamis Hamza Khamis Naibu Waziri Muungano na Mazingira majibu

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Omar Ali Omar, Mbunge wa Wete, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Omar kwa kazi nzuri anayoifanya kutuwakilisha katika suala zima la utunzaji na uhifadhi wa mazingira hasa katika suala la uhifadhi wa vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo juhudi mbalimbali ambazo tumezichukua katika kuhakikisha kwamba tunawasaidia hawa watu wa vikundi, cha kwanza ni kuelimisha. Tumegundua kwamba changamoto kubwa iliyokuwepo ni kwamba watu wengi taaluma kwao imekuwa ni changamoto. Kwa hiyo, tumekuwa tukichukua juhudi ya kuwaelimisha kuhusu suala la uhifadhi wa mazingira pia tunawahamasisha juu ya upandaji wa miti na kuishughulikia, kwa sababu kuipanda ni suala moja na kuishughulikia ni suala jingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa nitoe wito kwa jamii hasa Waheshimiwa Wabunge tushirikiane, kila mmoja apande mti lakini kila mtu ashughulikie mti wake, kuipanda tu miti haitoshi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kikubwa zaidi kwa kushirikiana na Wizara ya Uvuvi tunahakikisha kwamba tunapambana dhidi ya uvuvi haramu ambao unaharibu hayo masuala ya mazingira.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Juma Usonge Hamad swali la nyongeza.

**MHE. JUMA USONGE HAMAD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miongoni mwa Vijiji ambavyo vipo hatarini kutoweka kwa miamba hii ya matumbawe ni Kijiji cha Pwani Mchangani ambacho kipo katika Jimbo langu la Chaani.

Je, ni lini Serikali itachukua hatua za haraka ili sasa kunusuru Matumbawe yale yasiharibike lakini pia yasitoweke kutokana na shughuli za kibinadamu ambazo zinaendelea?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri Khamis Khamis jibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Juma Usonge Mbunge wa Jimbo la Chaani Kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nae nimshukuru na nimpongeze kwamba ni mmoja wa miongoni mwa Mabalozi wetu wazuri wa mazingira hasa katika Mkoa wa Kaskazini Unguja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazo juhudi mbalimbali ambazo tumepanga kwa ajili ya kuhakikisha kwamba Kijiji cha Pwani Mchangani kinaendelea kuwa salama hasa katika suala zima la uhifadhi wa mazingira. Moja ni kupitia taaluma lakini yapo matumbawe ambayo tumeshayaandaa kwa ajili ya kuhakikisha kwamba tunakwenda kuyaweka angalau sasa vile viumbe ambavyo vimo kwenye bahari viweze kuishi katika mazingira ambayo wanaweza waka-*survive* ili waweze kuhifadhi mazingira zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais na Mazingira tunaomba ukaketi sasa.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ninamuita Mheshimiwa Askofu Josephat Mathias Gwajima aweze kuuliza swali lake. *(Makofi)*

Na. 43

**Umuhimu wa Kuunganisha Mifumo ya Vitambulisho**

**MHE. ASKOFU JOSEPHAT M. GWAJIMA** aliuliza: -

Je, Serikali haioni umuhimu wa kuunganisha mifumo ya Kitambulisho cha Mpiga Kura na Kitambulisho cha Taifa ili kuepusha usumbufu kwa wananchi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, kwa niaba yake Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA K.n.y WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Askofu Josephat Mathias Gwajima, Mbunge wa Kawe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua umuhimu wa kuunganisha mifumo ya Kitambulisho cha Mpiga Kura na Kitambulisho cha Taifa ili kutumia Kitambulisho cha Taifa katika uchaguzi wa kawaida na ule wa kieletroniki *(e-voting)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matumizi haya yatapunguza gharama kwa Serikali katika kuandikisha na kutengeneza daftari pamoja na kurahisisha usimamizi wa wapiga kura.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mawasiliano kati ya Taasisi hizi mbili yenye dhumuni la kuwezesha kanzidata ya *NIDA* kutumika katika katika zoezi la uboreshaji wa daftari la Wapiga Kura yameanza mwezi Machi, 2022. Mazungumzo ya awali kati ya wataalam wa taasisi zote mbili yenye nia ya kuunganisha mifumo hiyo miwili yamepangwa kufanyika kabla ya mwezi Mei, 2022.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matarajio ya Serikali ni kuona mifumo hiyo inaunganishwa ili kuwarahisishia wananchi kushiriki katika shughuli za uchaguzi na kuipunguzia Serikali gharama katika uandikishaji na uchapishaji wa vitambulisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.*(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Askofu Josephat Mathias Gwajima swali la nyongeza.

**MHE. ASKOFU JOSEPHAT M. GWAJIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Pamoja na majibu mazuri ya Mhehimiwa Waziri nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa kitambulisho cha *NIDA* kinamthibitisha mtu kwamba ni Mtanzania, inakuwaje sasa wakati mtu anakwenda kutafuta hati ya kusafiria *(Passport),* anaombwa vitu vilevile alivyokuwa anaombwa wakati anaomba hati ya kusafiria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili Je, Serikali haioni sasa umuhimu wa kufanya hiyo namba ya Kitambulisho cha Taifa kuwa hiyo hiyo namba ya *TIN* na kuwa hiyo hiyo namba ya mita ya umeme kwa watu ambao wana nyumba zao? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Hamza Khamis Khamis.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA K.n.y WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali la Mheshimiwa Dkt. Askofu Josephat Gwajima maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapofika wakati tukawa tuna mdadisi mtu mara mbilimbili maana yake tumemdadisi kwenye *NIDA* pia tunamdadisi tupate maelezo yake kwenye hati ya kusafiria, suala kubwa hapa tunataka tujiridhishe. Kwa hiyo inabidi lazima tufike wakati tumhoji ili tuweze kujiridhisha kwa sababu hali za mifumo zinabadilika lakini na hali za binadamu pia zinabadilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inawezekana kitambulisho ambacho alikuwa nacho, kwa sababu vitambulisho pia vina-*expire date,* vinakuwa na *date of issue,* kwa hiyo tunataka tujiridhishe kwamba ni yeye na labda alipotokea na mazingira mengine, kwa hiyo, kubwa hapa huwa tunataka kujiridhisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lake la pili ameuliza Je, Serikali haioni haja ya kusema sasa tuunganishe mifumo. Hilo ni jambo jema na tunalichukua ni wazo zuri kwenda kulifanyia kazi kwa sababu siyo Tanzania tu, zipo nchi ambazo tayari zimeshafanya huo mfumo na zinatumia *NIDA* na kitambulisho kingine. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na Wizara hiyo ya Mambo ya Ndani ya Nchi, sasa ninamuita Mheshimiwa Haji Amour Haji Mbunge wa Pangawe aulize swali lake.

Na. 44

**Mrundikano wa Hati za Ukaazi Uhamiaji Zanzibar**

**MHE. HAJI AMOUR HAJI** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itashughulikia suala la mtambo wa kielektroniki ulioharibika kwa zaidi ya mwaka sasa na kusababisha mlundikano mkubwa wa hati za ukaazi katika Idara ya Uhamiaji Zanzibar.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hamza Khamis Khamis kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA K.n.y WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi naomba kujibu swali la Mheshimiwa Haji Amour Haji Mbunge wa Pangawe, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwezi Januari, 2020 hadi Juni, 2020 mtambo wa kuchapisha kadi za vibali vya elektroniki vya hati za ukaazi *(E-Permit)* wa Idara ya Uhamiaji Zanzibar ulisitishwa na kupelekea kadi za hati za ukaazi 139 kuchelewa kuchapishwa kwa sababu ya hitilafu ya mtambo wa kuchapia kadi za vibali vya hati za ukaazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, huduma za utolewaji wa hati za ukaazi ziliendelea kutolewa kwa wageni kwa kugongewa muhuri katika pasipoti ili kuthibitisha kuwepo kwao kihalali hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuanzia Julai, 2020 huduma za utoaji wa hati za kielektroniki ziliendelea kutolewa ambapo hadi kufikia mwezi Machi, 2022 jumla ya vibali 799 vya hati za ukaazi vya kielektroniki vimetolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Haji Amour Haji swali la nyongeza.

**MHE. HAJI AMOUR HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa ruhusa yako nina maswali mawili ya nyongeza:-

Swali la kwanza, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania yupo katika jitihada za kuwaita wawekezaji nchini kwetu Tanzania kwa ajili ya kuja kuwekeza nchini mwetu, wakati huo huo pia kuna kuwa na idadi kubwa ya wageni ambao wanakuja Tanzania kwa ajili ya kuja kujifunza.

Je, kwanini vibali vinachelewa?

Swali la pili, ninamuomba Mheshimiwa Waziri kama ataridhia kwake tukaongozana mimi na yeye kufanya ziara ya maksudi kwenda kuangalia mtambo ule ambao ulikuwepo Zanzibar na kuangalia vile vibali walau 100 vilivyochapishwa kwa mwaka huu 2022. Naomba sana hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Hamza Khamis Khamis kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA K.n.y WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Haji Mbunge wa Pangawe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu ya kuchelewa, kwanza nikiri hii changamoto ipo, lakini changamoto hii inasababishwa zaidi na wananchi wenyewe au wale ambao wanaotaka kuomba vile vibali vyewewe. Sababu moja ni za kimtandao unajua tumeingia katika *e-permit* kwa hiyo *time* nyingine inawezekana mtandao ukawa unasumbua ukacheleweshа kidogo, lakini sababu nyingine ni kwamba wananchi wenyewe au wale ambao wanaomba zile *permit* huwa wanafika wakati wanakuwa wanashindwa kukamilisha vigezo na masharti hivi vinapelekea sasa kuchelewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kikubwa ni kwamba kuna baadhi ya watu huwa wanawapitisha hawa wageni katika njia ambazo siyo rasmi wala siyo sahihi hii inapelekea vilevile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine kwa upande wa kwenda kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi tupo tayari kwa ajili ya kwenda huko kukagua huo mtambo huko Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Leah Komanya swali la nyongeza, Mheshimiwa Cecilia Paresso nimekuchanganya na Leah Komanya. *(Kicheko)*

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zoezi la kuwapatia Watanzania vitambulisho vya Taifa limechukua muda mrefu sana na imekuwa na sintofahamu. Kuna Watanzania ambao takribani miaka mitatu mpaka minne wana namba tu hawana kadi.

Je, ni nini kauli ya Serikali kuhusiana na jambo hili? Kama mmeshindwa muwaambie Watanzania kwamba mmeshindwa na haiwezekani zoezi hili. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri Hamza Khamis Khamis.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli hili jambo lilikuwa limekwama kidogo, lakini tulikuwa tuna changamoto na sababu ya kwamba hivi vitambulisho vichelewe kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kikubwa nimwambie Mheshimiwa kwamba bado Serikali haijashindwa kuwapatia wananchi vitambulisho, hivi ninavyokuambia vitambulisho vimeshazalishwa na tayari huko Wilayani

vimeshasambazwa. Kikubwa ni kwamba kama Wilaya ambavyo vitambulisho havijafika basi tuelezane tujue namna ya kufanya lakini vitambulisho tayari vimeshapelekwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *even if* vinazalishwa kwa *speed* siyo ile ya kawaida lakini kwa ufupi ni kwamba vitambulisho vinazalishwa na vitawafikia wananchi ili waweze kupata hiyo huduma ya vitambulisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Hamza Khamis Khamis kwa majibu sasa unaweza kwenda kuketi.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea Wizara ya Kilimo, ninamwita Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa Mbunge wa Namtumbo aulize swali lake.

Na. 45

**Kudhibiti bei ya Mbolea Nchini**

**MHE. VITA R. KAWAWA** aliuliza: -

Je, Serikali inachukua hatua gani kudhibiti kuongezeka kwa bei ya mbolea nchini hasa Mkoani Ruvuma: -

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Kilimo Mheshimiwa Hussein Mohamed Bashe majibu.

**WAZIRI WA KILIMO** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa Mbunge wa Namtumbo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, bei za mbolea duniani imekuwa ikiongezeka kutokana na kuongezeka kwa gharama za uzalishaji na mahitaji hususan kwenye nchi zenye watumiaji wakubwa wa mbolea kama vile China na India. Ongezeko hilo kwa msimu wa 2021/2022 limechangiwa na athari za UVIKO- 19 na vita kati ya Nchi ya Urusi na Ukraine ambao ni wazalishaji wa malighafi zinazotumika katika utengenezaji wa mbolea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeweka utaratibu wa kudhibiti upandishaji holela wa bei za mbolea kwa kuhusisha Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea nchini, inafanya tathmini ya gharama halisi ya mbolea na kutoa bei elekezi. Mwezi Machi, 2022 Serikali kupitia *TFRA* imetoa bei elekezi za mbolea za *DAP, UREA, CAN* na *SA* katika Mikoa mbalimbali nchini ikiwemo Mkoa wa Ruvuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuondokana na utegemezi wa uagizaji wa mbolea nje ya nchi, Serikali inaendelela kuvutia uwekazaji wa viwanda vya mbolea hapa nchini. Baadhi ya wawekezaji waliojitokeza ni pamoja na kampuni *Itracom* inayojenga kiwanda cha mbolea Jijini Dodoma chenye uwezo wa kuzalisha tani 600,000 na Kiwanda cha Minjingu kuendelea na kuongeza uzalishaji kutoka uwezo wa tani 100,000 za sasa hadi kufikia tani 500,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia Bunge lako Tukufu Serikali inasisitiza viongozi wa Mikoa na Wilaya kuhakikisha kuwa bei elekezi zinazotolewa zinazingatiwa katika vituo vyote vya mauzo ya mbolea. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa swali la nyongeza.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa nina maswali mawili ya nyongeza.

Kutokana na ongezeko kubwa la mbolea katika msimu huo uliopita, Je, sasa hivi Serikali sikivu ya CCM inaweza sasa kwa msimu unaokuja kuweka mpango wa kutoa ruzuku ya mbolea kwa wakulima wa mazao ya chakula mahindi na mpunga kwa utaratibu mtakaoona unafaa. *(Makofi)*

Swali la pili, kwa kuwa wakulima wa mahindi msimu huu wamelima kwa gharama kubwa kutokana na bei ya juu ya mbolea. Je, Serikali inaweza kwa msimu huu wa mavuno ikatangaza bei yake mapema *NFRA* ili wakulima waweze kupata unafuu au bei dira katika soko la mazao ya mahidi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Hussein Bashe Waziri wa Kilimo.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Vita Kawawa ya nyongeza kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu bei elekezi ya *NFRA immediately* baada ya Bunge lako Tukufu kupitisha bajeti na tutakapo *table* bajeti ya Wizara ya Kilimo na bajeti hiyo kupitishwa na Bunge lako Tukufu *NFRA* itatoa bei ambayo tutanunulia mazao ya nafaka kutoka kwa wananchi. Kwa hiyo Waheshimiwa Wabunge wasubiri hiyo itafanywa baada ya Bunge la Bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu hoja ya ruzuku ninataka nitumie nafasi hii kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge, maelekezo ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimwa Samia Suluhu Hassan ni kwamba mwaka ujao wa fedha baada ya Julai Mosi, tumepewa jukumu Wizara ya Kilimo na Wizara ya Fedha kukaa chini pamoja kutengeneza muundo wa namna ambavyo tutatoa ruzuku kwenye mbolea na siyo tu kwenye mazao maalum tutatoa ruzuku ya mbolea kwa mazao yote ya kilimo ili kutokurudia makosa yaliyokuwepo huko awali. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante kwa majibu mazuri sana Mheshimiwa Waziri wa Kilimo sasa namuita Mheshimiwa Condester Sichalwe Mbunge wa Momba aulize swali lake la nyongeza.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia nafasi.

Kwa kuwa Wizara ya Kilimo iliongezea fungu Benki ya Maendeleo ya Kilimo kwa lengo la kuwasaidia wakulima wadogo wadogo, inaonaje kama itatenga *percent* ya fedha hizo kwa ajili ya kutumia ruzuku ili bei ya mbolea kwenye msimu unaokuja iwe sawa na vile wananchi wamezoea ili kuwaondoa kwenye changamoto na majonzi ambayo wameyapitia katika msimu uliopita kwa mfumko mkubwa wa mbolea ambao wameupata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.*(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Kilimo Hussein Bashe majibu.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Condester kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutatumia *instrument* gani kwa ajili ya kutoa ruzuku. Niwaomba Waheshimiwa Wabunge wasubiri kwamba tumalizane kazi tunayoifanya kati ya Wizara ya Fedha na Wizara ya Kilimo kama tutatuma *through TADB,* tutatumia mfumo mwingine wowote ule tutalitaarifu Bunge lako Tukufu, uhakika tu ni kwamba kuanzia Julai tutatoa ruzuku kwa ajili ya kushusha bei ya mbolea. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Aida Khenani swali la nyongeza.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa nafasi na mimi niulize swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Waziri pamoja na bei elekezi ambazo zimekuwa zinatangazwa kila wakati, lakini bado imekuwa haitekelezeki kutoka kwenye Mkoa mmoja kwenda Mkoa mwingine hasa Mikoa ile ambayo ni *big five* kwa uzalishaji wa chakula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa changamoto hiyo ya uzalishaji ambayo ilikumba na nchi nyingine zote lakini kuna nchi ambazo bado zilifanya vizuri. Je, upo tayari kwenda kujifunza kwenye nchi ambazo nazo zilipata hiyo changamoto ya *COVID* lakini bado bei ya mbolea iliendelea kuwa nzuri au yenye unafuu wa kwa wakulima ikiwemo Ethiopia, Zambia, Uganda na maeneo mengine. Mpo tayari kwenda kujifunza kwa kuwa ni jambo jema. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri wa Kilimo majibu.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka tu kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba wataalam wa Wizara ya Kilimo wamekwenda Rwanda kwenda kuangalia *subsidy scheme* ya Rwanda inafanya kazi namna gani, wengine wamekwenda Zambia kwenda kuangalia *subsidy scheme* ya Zambia inafanya namna gani, wengine wamekwenda Malawi wameenda kuangalia *subsidy* scheme ya nchi hizo inafanya namna gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka tu niwaambie Waheshimiwa Wabunge ni kwamba jambo la *subsidy* kwenye nchi linahitaji mambo mawili, moja *political will* na ninamshukuru Mheshimiwa Rais ameonesha utashi wa kisiasa kuwepo kwa *subsidy* lakini la pili ni *management* ya mfumo wa *subsidy.* Nchi yetu ilikuwa na mfumo wa *subsidy* ambayo ulikuwa *abused* lakini ukiutazama mfumo ule ya *subsidy* uliokuwepo ambao ulikuwa *abused it was* ni mfumo ambao *abuse* ilitokana na *systematic system* ambayo ilitengenezwa na kuanzia na aliyekuwa anausimamia mpaka aliyekwenda kuutekeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nataka niwahakikishie tu kwamba Waheshimiwa Wabunge ni kwamba tutafanya mfumo wa utoaji wa ruzuku ambao hautoweza kuturudisha kule ambako tumetokea na utashi wa kisiasa wa Mheshimiwa Rais umeonekana hadharani na tarehe Nne mbele ya Watanzania aliahidi na alitoa agizo. Kwa hiyo, mtuachia tulifanyie kazi tuta-*communicate* na watanzania na kuwaambia namna gani tunalifanyia kazi hili jambo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Waziri wa Kilimo. Mheshimiwa Emmanuel Cherehani Mbunge wa Ushetu swali la nyongeza.

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuondoka kwa kampuni ya *TLTC* hapa nchini kumechangia kudorora kwa soko la Tumbaku.

Je, ni lini Serikali itakamilisha mazungumzo na kampuni hii ili iweze kurudi Tanzania kununua Tumbaku za wakulima na kuongeza tija na ushindani? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu kwa ufupi Mheshimiwa Waziri wa Kilimo Mheshimiwa Hussein Bashe.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka tu niwaambie wakulima wa Tumbaku na niwaambie Watanzania, kiwanda kilichokuwa cha *TLTC* na kampuni ya *TLTC* imenunuliwa na sasa hivi amepatikana mwekezaji mwingine na mwekezaji huyu yupo kwenye hatua za mwisho na mwaka huu kiwanda kile kitafunguliwa. Serikali tunawasaidia wawekezaji wapya kuweza kupata *minimum quantity* ya tumbaku ili kiwanda kile kifunguliwe, kwa hiyo

nataka niwaambie tu wakulima wa tumbaku kilichokuwa kiwanda cha *TLTC* amerudi sokoni kupitia kampuni nyingine ambayo imeweza kununua kiwanda kile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo niwahakikishie tu kwamba kiwanda kile kinafunguliwa na ninaamini msimu ujao wa 2022/2023 uzalishaji na makisio yataongezeka tofauti na tulivyokuwa sasa hivi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Daniel Awack Mbunge wa Karatu.

**MHE. DANIEL A. TLEMAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwakuwa Benki hii ya Kilimo imeanzishwa kwa namna ya kuwasaidia wakulima wa Tanzania na hii benki inapatikana katika *center* ya Makao Makuu.

Je, Wizara ina mkakati gani wa hii benki hata kama itashindikana kwa kila Mkoa angalau iende kwenye kila ukanda wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Waziri wa Killimo Mheshimiwa Hussein Bashe.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme jambo moja kwanza ieleweke Tanzania *Agricultural Development Bank*, siyo Commercial *Bank is a Development Bank.* Kisera tusitajarajie nami nataka niwe mkweli mbele ya Bunge lako Tukufu. Tusitarajie *TADB* kuwa na matawi kama alivyo *CRDB* na *NMB*, huo ndiyo ukweli. Jukumu la kisera la *TADB* ni Benki ya Maendeleo ambayo moja ya *function* yake ni ku- *de risk* sekta ya kilimo kwa kutoa dhamana kwenye *commercial banks*, ili *commercial banks* ziweze kuwakopesha wananchi, hili ni jambo la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili tumeitaka *TADB* iwe na ofisi katika Mikoa na Kanda, sasa hivi Kanda ya Kati wapo, Kanda ya Magharibi wapo, Kanda ya Ziwa wapo, Kanda ya Kaskazini wameshafungua ofisi. Kwa hiyo, wana ofisi zao. Wanachokifanya sasa hivi *TADB* ni kuwa na makubaliano na *commercial banks* ambazo zitafanya kazi na wao na wao wanatoa dhamana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie Bunge lako kuwaambia sekta ya kilimo sasa hivi imekuwa ikipata mikopo mingi sana kutokana na guarantee zinazotolewa na *Tanzania Agricultural Development Bank.* Tunaendelea majadiliano na *TADB* kuboresha na kufanya *awareness* kwamba namna gani huduma zao zinaweza kuwepo katika taasisi za benki, katika Mikoa na Wilaya ili angalau wawe na madawati waweze kufanya kazi vizuri na *Commercial Banks.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tusidhani kwamba *TADB* ni kama ilivyo *CRDB, NMB* ama ilivyo Akiba *Commercial Bank* hii ni *Development Bank* ina majukumu yake ambayo yamewekwa wazi. Nasi tunawaomba Waheshimiwa Wabunge tuache kuitaka *TADB* kwenda Wilaya, bali tui-*demand TADB* itoe dhamana kwenye *Commercial Banks* ili wakulima wadogo wadogo wasiokuwa na dhamana waweze kukopesheka kirahisi na *Commercial Banks. (Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Noah Ole Saputu.

**MHE. NOAH L. S. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kumuuliza Waziri swali la nyongeza kwamba kumekuwepo na malalamiko kwa wananchi kuhusu ubora wa mbolea zinazoingizwa nchini na makampuni mbalimbali hasa mahindi na mazao ya kunde.

Je, ni nini hasa kauli ya Serikali kuhusu mbegu hizo ambazo zinaingizwa na hazina ubora nchini na wananchi wanaendelea kupata hasara? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Kilimo majibu.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Noah kwa ufupi tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kuna Mtanzania ambaye amenunua mbegu na ana *receipt* ya duka lililomuuzia mbegu ile na mbegu ile ikawa ni *fake*, atoe taarifa Wizara ya Kilimo, kwa sababu tutamchukulia hatua muuzaji kwa maana ya *dealer* na *distributor*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upo utaratibu wa kisheria ambao unasimamiwa na taasisi yetu ya *TOSCI* na *TOSCI* anatoa namba maalum katika kila mbegu inayouzwa mtaani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kuna Mtanzania amenunua mbegu na ikawa feki tunamkaribisha afike Wizara ya Kilimo, tutachukulia hatua wote. Tunayo kesi Mkoa wa Ruvuma ambayo mtu aliuza mbegu, alizitia rangi na sasa hivi amepelekwa mahakamani, anachukuliwa hatua kwa sababu huu ni uhujumu uchumi na hatuwezi kuruhusu hili. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Hussein Bashe kwa majibu mazuri sana kwenye Wizara yako ahsante. Tunaendelea na Wizara ya Afya namuita Mheshimiwa Stella Ikupa Alex, Mbunge wa Viti Maalum aulize swali lake.

Na. 46

**Hitaji la Vyumba vya Kujifungulia Wanawake Wenye Ulemavu**

**MHE. AGNES M. MARWA K.n.y. MHE. STELLA A. IKUPA** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kuwa kuna vyumba maalum kwa ajili ya kujifungulia wanawake wenye ulemavu?

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Agnes Marwa aliyeuliza kwa niaba ya Mheshimiwa Stella Ikupa Alex, sasa namuita Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Mheshimiwa Mollel aweze kujibu maswali.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Afya, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Stella Alex Ikupa, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeshalitambua tatizo hilo na kwa muda mrefu sasa marekebisho yamekuwa yakifanyika kwenye miundombinu isiyo rafiki kwa wanawake wenye ulemavu na tayari kwenye ramani mpya za ujenzi wa vituo vya afya, hospitali, ununuzi wa vifaa tiba, mahitaji kwa watu wenye mahitaji maalum yamezingatiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Agnes Marwa swali la nyongeza.

**MHE. AGNES M. MARWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Kwanza nimshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri katika Wizara hii. Niombe na kuishauri Serikali ifanye hivyo kwa Mikoa yote ya Tanzania nzima ukizingatia wanawake wenzetu na wao wanatakiwa wazae katika uzazi salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la nyongeza liko hivi, Mkoa wa Mara, ni kati ya Mikoa yenye changamoto yenye uhitaji huu wa vyumba vya kujifungulia wanawake wenzetu wenye uhitaji maalum.

Je, Serikali ina mpango gani wa kwenda kujenga vyumba hivyo katika Wilaya zote za Mkoa wa Mara ukizingatia ni Mkoa *special* alikotoka muasisi wa Taifa hili Baba yetu Mwalimu Julius Nyerere?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Dkt. Godwin Mollel, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza maelekezo ya Rais wetu Mama Samia Suluhu Hassan hasa alipokuwa anatusisitiza kuhusu eneo la kupunguza vifo vya akina Mama na Watoto mojawapo ni eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala siyo kujenga maeneo maalum kwa ajili ya wao kujifungulia, lakini ni suala la ndani ya ramani yenyewe na huduma yenyewe ambayo akina mama wengine wote wanapata huduma ndani humo kuhakikisha kwamba kuna usaidizi mazingira *infrastructure* inawasaidia wao kuweza kupata huduma hiyo. Lakini kunakuwepo na vifaa ambavyo vinaweza vikawasaidia wenzetu wenye mahitaji maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii kwa niaba ya Waziri wa Afya kwa kushirikiana na wenzetu wa TAMISEMI kwamba sasa Waganga Wakuu wa Mikoa yote wanapokwenda kufanya usimamizi shirikishi eneo hilo liwe sehemu yao ya hadidu rejea ya kufuatilia kuhakikisha kila Wilaya, kuhakikisha kila Kituo cha Afya kila Zahanati wamezingatia hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Komanya swali la nyongeza.

**MHE. LEAH J. KOMANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zahanati zilizojengwa miaka ya 2000 vyumba vyake havikidhi hadhi ya kujifungulia kinamama kwa kuwa ni vidogo na vingine ni mfano wa *corridor* limewekwa pazia tu.

Je, Serikali haioni haja zahanati hizo za zamani kukajengwa wodi ya akina Mama ili kuendana na sera ya afya ya kinamama baada ya kujifungua wapumzike Saa 24? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri kwa ufupi kabisa kwa sababu maswali ya nyongeza yapo mengi sana hapa.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ndiyo maana nimesema Serikali imeanza na imegundua tatizo hilo kwamba lipo na ndiyo maana kumekuwa na marekebisho yanayoendelea kwenye vituo mbalimbali. Nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge katika harakati za kupunguza vifo vya akina Mama na Watoto hayo anayoyasema yamezingatiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaona kuna fungu maalum kwa kushirikiana na wenzetu wa TAMISEMI, limekuwa likipelekwa kwa ajili ya kujenga hayo maeneo ya akina Mama kwa ajili ya kujifungulia.

**MWENYEKITI**: Ahsante. Mheshimiwa Ritta Kabati swali la nyongeza.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza.

Kwa kuwa, changamoto kubwa kabisa inayokabili watu wenye ulemavu wanapokwenda hospitali hasa ni mawasiliano kati ya Daktari na mgonjwa, kwa sababu ulemavu unatofautiana.

Je, nini mkakati wa kuhakikisha kwamba Madaktari wanaelewa lugha za watu wenye ulemavu, kwa sababu wengine wanaongea kwa ishara? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mkakati Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niseme Mheshimiwa kwa kweli ameelezea suala siyo tu kusema ulemavu lakini ni wenzetu wenye mahitaji maalum kwa sababu kila mmoja ana mahitaji yake tofauti ukilinganisha na mwenzake. Na anasema mojawapo ya sehemu ni kwenye mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli kwa mfano kwenye hospitali ya Kanda ya Mkoa wa Mbeya tayari tumeanza *process* ya kuweka wale watu wanaoweza kutafsiri lugha kwa ajili ya watu wenye mahitaji maalum, tunaendelea sasa ku-roll *out* kuingia kila mahali. Lakini kwa kweli kuna shida kubwa hasa kupata watu wale wenye uwezo wa kufafanua lugha, kufafanua na mambo mengine hasa inapofika maeneo ya kitiba. Lakini Serikali inawekeza eneo hilo nguvu kuhakikisha hao watu wanapata huduma hiyo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Catherine Magige swali la nyongeza.

**MHE. CATHERINE V. MAGIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa sera ya Taifa ya Afya inatamka kuwa kila Kijiji kinastahili kuwa zahanati, kila Kata inastahili kuwa na kituo cha afya, na kila Wilaya inastahili kuwa na hospitali ya Wilaya.

Je, nini mkakati wa Serikali kuhakikisha vijiji 22 vilivyopo katika Wilaya ya Longido Mkoa wa Arusha, ambavyo havina zanahanti wala kituo cha afya vinafikiwa na huduma hii?

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge amesema na inakumbukwa kwenye Bunge hili yalishatoka maelekezo kwa maana kwa Halmashauri zetu kwamba

watenge bajeti wao wenyewe kwa maana ya kujenga zahanati kulingana na mapato yao, lakini bado Serikali inafikiria namna ya kufanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelekezo yalishatoka kwamba utaenda utajenga kituo cha afya kwenye Kata lakini ukweli ukiangalia idadi ya watu eneo husika na mahitaji ya kituo cha afya kile kituo cha afya inakuwa kama kinatumika chini ya kiwango. Ndiyo maana tumekwenda kwenye kusema kila Tarafa ipate kituo cha afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachukua mawazo ya Mheshimiwa Mbunge hasa ulipozungumzia Longido kwa sababu ukizungumzia Longido ni karibia mara 2.5 ya Mkoa wa Kilimanjaro. Kwa hiyo, kwa kuangalia Longido *specifically* tunaweza tukakaa kwa pamoja na tuone ni namna gani tunaweza kufanya kwa *approach* hiyo ili tuweze ku-*treat* kila eneo kulingana na changamoto za eneo husika bila ku-*generalize*. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Eng. Manyanya, halafu Mheshimiwa Zaituni Swai, maswali ya nyongeza.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa kumekuwa na changamoto kubwa ya kuwatambua watoto ambao wamezaliwa na ulemavu katika hatua za awali kutokana na uelewa usiokuwa wakutosha kwa wale ambao wanazalisha yaani Manesi.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuendeleza elimu hiyo kwa kasi hasa vijijini ili mtoto atambuliwe katika hatua za awali kabisa na kuweza kusaidiwa kwa mfano kwenye mtindio wa ubongo? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri Daktari Godwin Mollel.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli anachokisema Mbunge, lakini nimuondoe wasiwasi, uelewa kwa manesi ni mkubwa, lakini kumekuwa kukitokea maeneo machache ambayo kweli watoto wanachelewa kutambuliwa hasa kwa mfano wa wenye *autism* na matatizo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri tutaendelea kuhakikisha elimu inakwenda na utaona sasa hivi kuna taasisi ambazo zinahamasaisha hayo maeneo ambayo kwa kweli yamekuwa na changamoto. Ukiona Rais wetu mama Samia Suluhu Hassan ametenganisha Wizara ya Afya na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, ni kwa sababu vile kuna masuala mengine ni ya kijamii na sasa kupitia Wizara ya Maendeleo ya Jamii tutahakikisha kwenye eneo la jamii sasa hata wale ambao wanaoweza jamii ikashirikiana na sisi kuwatambua kwa sababu bado tuna tatizo vilevile, kuna watu wanaozalia majumbani na wakati mwingine wasifike kwenye vituo vyetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kushirikiana wote kwa pamoja ninahakika tutaweza kutatua hayo matatizo na Mbunge uwe mmojawapo wa balozi wetu kuhakikisha eneo hilo linafanyiwa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zaytuni Swai, swali la mwisho la nyongeza.

**MHE. ZAYTUN S. SWAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa fursa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hospitali zetu nyingi katika Mkoa wa Arusha hususan zile zilizoko kwenye Wilaya za pembezoni zina uhaba mkubwa wa vifaa vya kujifungulia kinamama.

Je, Serikali ina mikakati gani ya kuhakikisha vifaa hivi vinapatikana na vinatolewa bure kwa akina mama? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Daktari Godwin Mollel.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kama anavyosema Mheshimiwa Mbunge kwamba kuna maeneo yenye changamoto. Lakini Rais wetu Mama Samia Suluhu Hassan kama ambavyo nimekwishaeleza hapa Bungeni hapo kabla ameshatoa Shilingi Bilioni 333.8 na kila mwezi imekuwa ikitoka Bilioni 15.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kumekuwa na shida kwenye eneo la manunuzi kuhakikisha kwamba zile fedha zinanunuliwa vitu na kuhakikisha zinafika eneo husika. Tutaenda kulitatua hilo na kuhakikisha tunatekeleza kama alivyosema. Kwa sababu sasa hivi tatizo siyo fedha, tatizo ni kasi ya kuhakikisha vifaa vinafika eneo husika. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Daktari Godwin Aloyce Mollel kwa majibu mazuri. Sasa tunakwenda Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, ninamuita Mheshimiwa Bupe Nelson Mwakang'ata, Mbunge wa Viti Maalum, aulize swali lake.

Na. 47

**Ujenzi wa Uwanja wa Ndege  Sumbawanga**

**MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango wa kukamilisha ujenzi wa uwanja wa Ndege wa Sumbawanga Mjini.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Kasekenya!

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi naomba kujibu swali la Mheshimiwa Bupe Nelson Mwakang'ata, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiwanja cha Ndege cha Sumbawanga ni miongoni mwa miradi ya Ujenzi na Upanuzi wa Viwanja vya Ndege Vinne (4) ambavyo ni Kigoma, Tabora, Sumbawanga na Shinyanga inayotarajiwa kutekelezwa kwa Ufadhili wa Benki ya Uwekezaji ya Ulaya (*European Investment Bank - EIB*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka sasa, matakwa ya kimkataba kati ya Serikali na *EIB* yamekamilishwa na mfadhili tayari ameshatoa fedha kwa ajili ya kuanza utekelezaji wa miradi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa mradi huu ulichelewa kuanza kwa wakati, kwa sasa taratibu za kimkataba kati ya Serikali na Mkandarasi zinaendelea. Aidha, Mkandarasi amewasilisha maombi ya kufanyika kwa marekebisho ya Mkataba wa awali. Hivyo, marekebisho haya yameshafanyika na kuwasilishwa kwa Mfadhili *(EIB)* kwa ajili ya kupata idhini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa, Serikali imejipanga kuanza utekelezaji wa mradi huu kabla ya mwaka wa fedha 2021/2022 haujaisha endapo idhini itatolewa na mfadhili kwa wakati.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Bupe Mwakang'ata swali la nyongeza.

**MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama hapa kwa mara ya saba kulalamikia uwanja wa Sumbawanga Mjini, leo nataka *commitment* ya Serikali, ni lini kazi ya ujenzi wa uwanja wa Sumbawanga Mjini utaanza?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, Serikali sasa ina mpango gani wa kuweka basi hata *route* ya kutoka Songwe moja kwa moja mpaka Dodoma wakati huo inaendelea kujipanga kwa ujenzi wa Sumbawanga Mjini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri Eng. Kasekenya? Majibu!

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Bupe Nelson Mwakang'ata Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Rukwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi, ilitakiwa kiwanja hiki kianze kujengwa mwaka wa fedha wa 2017/2018, lakini kutokana na changamoto ambayo ilikuwepo *EIB* hawakutoa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Mbunge amenisikiliza tayari *EIB* wameshatoa Dola Milioni 12 kwa ajili ya kuanza viwanja hivi vinne. Lakini kwa kuwa usanifu ulifanyika zamani, Mkandarasi ameomba mkataba huo urudiwe kwa sababu ya gharama, na kwa sababu gharama zitabadilika lazima tuwasiliane na mtoa fedha ili aweze kutoa *no objection*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika jibu langu nimesema kama atatoa kwa sababu Mkandarasi yupo basi itaanza kujengwa kabla ya mwisho wa mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu route ya Songwe hadi Dodoma, tumelichukua lakini pia nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Shirika letu la Ndege la *ATCL* inayafanyia kazi masuala yote haya ya usafiri kuona namna ya kuunganisha kati ya Dodoma - Mwanza, Dodoma- Kilimanjaro, Dodoma – Mbeya, lakini hii itategemea na wao watakavyofanya *study* kuona kama wakifanya hivyo kwao biashara itakuwa ni nzuri. Kwa hiyo, wapo wanaendelea kulifanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi. nimekuona Mheshimiwa Bonnah Kamoli, uliza swali lako.

**MHE. BONNAH L. KAMOLI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Kwa kuwa hii ni Wizara ya Ujenzi, Je, Mheshimiwa Naibu Waziri ni lini *TANROAD* wataenda kutengeneza barabara ambayo wameiparua pale Kata ya Segerea kwa muda wa Miezi Mitatu sasa na wananchi wanapata vumbi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi.

**NAIBU WAZIRI UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Bonnah Kalua Mbunge wa Segerea kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli hii barabara imekuwa inatengenezwa kwa vipande na kipande anachokisema kweli tulikuwa tumeanza kufanya maandalizi lakini kulikuwa na shida ya kupata msamaha wa kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimhakikishe Mheshimiwa Mbunge kwamba msamaha huu umeshatolewa na mara moja Mkandarasi atakuwa yuko *site* kuondoa lile vumbi ambalo linaleta shida kwa wananchi wa Jimbo la Segerea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba tu kupitia nafasi hii pia nimjulishe ama kumuagiza Meneja wa *TANROAD* kwamba kwa kuwa msamaha umeshatolewa basi Mkandarasi aende *site* ili aweze kukamilisha kazi ambayo anatakiwa aifanye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Ndaisaba swali la nyongeza.

**MHE. NDAISABA G. RUHORO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa, uwanja wa ndege wa Ruganzo umejengwa muda mrefu umechoka na sasa unahitaji ukarabati. Na kwa kuwa, sasa Ngara imefunguka, wageni ni wengi, *Nickel* inatakiwa kuchimbwa na biashara mpakani imeshamiri.

Je, ni lini Serikali itakuja kukarabati uwanja wa ndege wa Ruganzo?

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Ndaisaba kwa swali la nyongeza sasa nakuita Mheshimiwa Naibu Waziri uweze kujibu swali husika kwa ufupi ili nitoe nafasi kwa watu wengine.

**NAIBU WAZIRI UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ndaisaba, Mbunge wa Ngara kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba suala lake limepokelewa na tunajua wageni wengi wanaenda Ngara ambapo ni mbali kutoka viwanja vyote vya ndege ambavyo viko karibu. Kwa hiyo, suala lake tumelichukua na Serikali itatafuta fedha ili kuweza kukikarabati kiwanja hiki ili wageni na watu mbalimbali waweze kufika kwa urahisi kwa ndege katika Wilaya ya Ngara.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Rashid Shangazi, Mbunge wa Mlalo, swali la nyongeza.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Mheshimiwa Naibu Waziri anajibu swali la msingi, alitaja viwanja Vinne lakini kwa bahati mbaya kiwanja cha Tanga sijakiona ilihali Tanga tuna ujenzi wa bomba la mafuta na ujenzi huu utahitaji uwanja wa ndege wa Tanga uwe umepanuliwa kwa ajili ya kutoa huduma.

Je, ni upi mkakati wa Serikali kupanua uwanja wa ndege wa Tanga ili kuruhusu shughuli za bomba la mafuta?

**NAIBU WAZIRI UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Rashid Shangazi, Mbunge wa Mlalo kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanja nilivyovitaja vine vipo kwenye *package* moja, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge Shangazi kwamba Serikali kama bajeti ya mwaka huu tunaokwenda kuipitisha itapita, kuna viwanja vingine ambavyo pia tuna mpango wa kuvipanua na hasa kiwanja alichokisema cha Tanga ambacho katika kipindi hiki ni kiwanja muhimu sana kwa shughuli ambazo zinaendelea katika Mkoa wa Tanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tuna uwanja wa Tanza, kuna uwanja wa Lake Manyara, Simiyu, Lindi, ni kati ya viwanja ambavyo tunategemea kama bajeti itapita, vitakuwa ni baadhi ya viwanja ambavyo tutavipanua na kuvifanyia maboresho makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ester Midimu, halafu atamalizia Mheshimiwa Deo Mwanyika.

**MHE. ESTHER L. MIDIMU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa, ujenzi wa uwanja wa ndege wa Mkoa wa Simiyu upo kwenye Ilani na eneo tayari limeshajengwa.

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa ndege katika Mkoa wa Simiyu?

**NAIBU WAZIRI UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Esther Midimu Mbunge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyomjibu Mheshimiwa Shangazi, nimetaja kiwanja cha Simiyu kwamba ni kati ya viwanja ambavyo vipo katika bajeti ambayo tunaenda kwenye mpango wa kuanza kivijenga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Deo Mwanyika.

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwanja wa Njombe Mjini ni uwanja ambao wananchi wanauhitaji mkubwa sana wa usafiri wa anga, na kwenye ahadi ya Chama cha Mapinduzi umesemwa, Waziri Mkuu ameahidi.

Je, ni lini sasa uwanja huo utaanza ujenzi?

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Mheshimiwa Injinia Kasekenya.

**NAIBU WAZIRI UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Deo Mwanyika, Mbunge wa Njombe Mjini kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli uwanja wa Njombe unatakiwa ujengwe na tayari upembuzi yakinifu ulishafanyika. Serikali inatafuta fedha ili iweze kufanya usanifu wa kina wa uwanja huu ili uweze kujengwa hasa tukizingatia kwamba nguvu kubwa ya kiuchumi ya Mkoa wa Njombe, kwamba tunahitaji kuwa na uwanja kwa ajili ya ku-*attract* si tu wafanyabiashara, lakini pia tunajua ndiyo kuna uwekezaji mkubwa wa madini ya makaa ya mawe na chuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tuna uhakika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inatafuta fedha kufanya usanifu na hatimae kuujenga huo uwanja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri, Ujenzi na Uchukuzi, Injinia Godfrey Kasekenya Msongwe kwa majibu. Tunakwenda Wizara ya Maji, sasa namuita Mheshimiwa Alexander Pastory Mnyeti Mbunge wa Misungwi aulize swali lake.

Na. 48

**Hitaji la Maji Mji wa Misasi**

**MHE. ALEXANDER P. MNYETI** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itapeleka maji katika Mji wa Misasi?

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, Mheshimiwa Injinia Maryprisca Mahundi.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waaziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Alexander Pastory Mnyeti Mbunge wa Misungwi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kata ya Misasi ina vijiji Vinne (4) vya Inonelwa, Misasi, Mwasagela na Manawa na vinapata huduma ya maji kupitia visima virefu viwili pamoja na skimu za maji za mtandao wa bomba. Hali ya upatikanaji wa huduma ya maji katika Kata hiyo ni asilimia 40. Katika kuboresha huduma ya maji katika Kata ya Misasi, Serikali inaendelea na ujenzi wa mradi unaotoa maji kwenye bomba kuu la Mabale-Mbarika kwenda kwenye vijiji vya Kata hiyo ambapo utekelezaji wake umefikia asilimia 90 na unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2022.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kukamilika kwa mradi huo kutaboresha hali ya upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama katika Kata ya Misasi kufikia asilimia 80. Katika mwaka wa fedha 2022/2023, Serikali itaendelea na upanuzi wa mradi huo ili kuhakikisha wananchi wote wa Kata ya hiyo wanapata huduma ya maji safi na salama na yenye kutosheleza.

**MWENYEKITI:** Swali la nyongeza Mheshimiwa Alexander Pastory Mnyeti.

**MHE. ALEXANDER P. MNYETI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo langu siyo kubishana na Mheshimiwa Waziri kuhusu asilimia zinazopatikana pale Misasi. Kwa mtizamo wangu kwa sababu naishi huko, kutoka asilimia 40, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Waziri kwamba upatikanaji wa maji Misasi ni chini ya asilimia Nne hakuna maji, watu wanatafuta maji, hakuna maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, Mkandarasi aliyetekeleza mradi huu naweza nikasema ni kandarasi ya kitapeli, na Wizara imerithi miradi mingi ya kitapeli ya sampuli hii kwenye Taifa letu. Wakandarasi wanachukua fedha, lakini hawatekelezi miradi iliyokusudiwa kulinga na mkataba. Mradi huu tangu mwaka 2013 leo ni miaka tisa, kupeleka maji kilomita 15 kutoka chanzo cha maji, imekuwa ni stori za hapa, stori za pale, stori za kule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri, ni lini upo tayari twende Misasi ukawaeleze hizi stori wananchi wa Misasi wewe mwenyewe kwa sababu Wabunge tumeshachoka, tumeshayaeleza mambo haya kila siku, mradi huu umesimama, Mkandarasi haeleweki, fedha ameshachukua, hakuna kinachoendelea *site*.

**MWENYEKITI:** Haya ahsante.

**MHE. ALEXANDER P. MNYETI**: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri, ni lini mtaanza kuyafuta makandarasi ya namna hii kwenye Taifa letu, kwa sababu tumejaribu kufuatilia, Mkandarasi huyu kote alikotekeleza miradi hii yote ni feki, hakuna anachokifanya anachukua fedha. Mbaya zaidi….

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Alexander Mnyeti, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ameuliza lini kufuatana na mimi mara baada ya Bunge hili tutakwenda kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na Wakandarasi feki, tayari Wizara imeshughulika nao ipasavyo, huyo unayemuongelea tutaendelea kumfuatilia pia tufanye kama tulivyofanya kwa wengine. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ally Kassinge swali la nyongeza.

**MHE. ALLY M. KASSINGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nifahamu mradi wa maji wa kutoka Mto Mavuji kuelekea katika miji ya Kilwa Kivinje na Kilwa Masoko lini utaanza kutekelezwa?

**MWENYEKITI:** Rejea swali lako Mheshimiwa Ally Kassinge, Mbunge wa Kilwa.

**MHE. ALLY M. KASSINGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa maji kutoka mto Mavuje, kuelekea katika miji ya Kilwa Masoko na Kilwa Kivinje, ni lini utaanza kutekelezwa?

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ally Mbunge wa Jimbo la Kilwa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huu ni mradi muhimu sana kwa Jimbo la Kilwa na tunafahamu namna ambavyo Mheshimiwa Mbunge amekuwa akifuatilia kwa karibu sana. Mheshimiwa Mbunge mradi huu tunakwenda kuutekeleza mwaka ujao wa fedha.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Shally Raymond.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama hapa kwa ajili ya mradi mmoja tu, mradi wa Mwanga, Same, Korogwe. Ukitaja Moshi, katika Mkoa wa Kilimanjaro, Mji mkubwa unaofuata ni Same, lakini takribani ni miaka kadhaa toka tumepata uhuru same haijawahi kupata maji safi na salama na wanaogea maji ya kununua mpaka leo.

Je, ni lini sasa ule mradi ambao tuliambiwa ungekamilika mwaka jana Septemba utakamilika?

**MWENYEKITI:** Majibu kwa ufupi sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Shally, Mbunge Viti Maalum kutoka Kilimanjaro kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huu wa Same -Mwanga ni mradi ambao ni mkubwa na umetumia fedha nyingi na sisi kama Wizara tumefuatilia kwa karibu na tayari kazi zinaendelea. Hivyo nipende kusema mradi huu utakamilika ndani ya wakati kwa namna ambavyo usanifu unaonesha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Profesa Muhongo swali la nyongeza, Mheshmiwa Dkt. Musukuma.

**MHE. DKT. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, umenipandisha cheo nafaa kuwa profesa, nakushukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa Miji 28 ni mradi ambao ulikuwa unaifaidisha sana Geita Mjini na Geita Vijijini, lakini kila tukiuliza hapa tunaambiwa tunakamilisha makaratasi.

Je, Mheshimiwa Waziri, ni lini mradi wa Miji 28 ambao unalifaidisha Jimbo la Geita kwa Kata utaanza? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Daktari Musukuma kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi ya Miji 28 tayari tumefikia hatua nzuri sasa ya manunuzi na mradi huu unaelekea kwenye utekelezaji kabla ya mwezi Juni, 2022.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Esther Matiko.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa ikitoa takwimu za upatikanaji wa maji kwenye maeneo yote takribani nchini ambazo hazina uhalisia. Sasa ni lini Serikali itafanya rejea ili iweze kuja na uhalisia wa upatikanaji wa maji kwenye maeneo yetu nchini kuliko ilivyo sasa hivi? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri Eng. Maryprisca Mahundi.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba kujibu swali la Mheshimiwa Esther Matiko, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la takwimu, ni suala la pana, pale tunaposoma takwimu 40 *percent*, maana yake kuna *calculation* zinazofanyika, zinazojumuisha mtandao wa mabomba, pamoja na namna ambavyo ukubwa wake umefikia katika eneo la usambazaji. Hivyo masuala ya takwimu, katika mifumo ya usambazaji wa maji yanahesabu zake, lakini kikubwa ninachoweza kusema tusiangalie tu hii takwimu, angalieni kazi inayofanywa na Wizara ya Maji, mabadiliko ni makubwa, mageuzi ni makubwa na tutaendelea kuwafikia wananchi wote kutoa huduma safi ya maji safi na salama. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Maswali mawili ya mwisho ya nyongeza yatauliza na Mhesimiwa Zainab Katimba na Mheshimiwa Mulugo.

**MHE. ZAINAB A. KATIMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Nataka kufahamu Je, Serikali ni kwa kiwango gani inatakeleza mkakati wa hifadhi na matumizi endelevu ya maji, kama vile kujenga au kutengeneza miradi ya uvunaji maji ya mvua kama vile ilivyoainishwa kwenye ukurasa 36, 37(a)(3) cha Ilani ya Chama cha Mapinduzi?

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri Maji.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Zainab Katiba kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa miundombinu ya mabwawa ndani ya Wizara ya Maji, kwa sasa tuna mabwawa Sita ambayo yako kwenye utekelezaji, lakini tuna sanifu mbalimbali ambazo zinaendelea na nyingine zimekamilika na katika utekelezaji huo, tayari tunatarajia kuwa na bwawa kubwa la Kidunda, ambalo wenzetu wa DAWASA chini ya uongozi wa Cyprian tayari wamepata kibali cha kuweza kwenda kumpa kazi Mkandarasi pamoja na Mhandisi Mshauri na hawa wote wameshaenda

kuoneshwa *site* na tunarajia lile Bwawa la Kidunda liweze kuwa ukombozi mkubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kwa hapa Dodoma Bwawala Farkwa na lenyewe pia tunaendelea kulifanyia kazi ili liwe ni jibu sahihi la miradi kuwa endelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maeneo yote ya nchi tunatarajia kuchimba mabwawa mengi. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais Mama Samia Suluhu Hassan ameweza kuruhusu zaidi ya shilingi bilioni 34 tunazitumia kwa ajili ya kuleta mitambo seti Nne kwa ajili ya kuchimba mabwawa, vilevile seti 25 za kuchimba visima na seti za kufanya utafiti wa maji chini ya ardhi ziko nne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya mitambo hii yote kuwasili nchini Waheshimiwa Wabunge, tutafikia Majimbo yote kwa urahisi na suala la kuvuna maji ya mvua litapewa kipaumbele na kuona kwamba linaenda kuleta uendelevu wa miradi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Philip Mulugo swali la nyongeza.

**MHE. PHILIPO A. MULUGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana niweze kuuliza swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Maji imekuwa ikijipambanua vizuri sana kwamba inafanya vizuri na sisi tumeona lakini wana mapungufu mengine ni makubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi navyosema Mikoa ya Rukwa, Mbeya, Songwe, miradi mingi inachelewa kwa sababu *RUWASA* hawana *tender board*. Bodi ya manunuzi haipo kabisa katika Mikoa hiyo na hii inasababisha miradi mingi inachelewa. Hivi navyosema Jimboni Songwe miradi mingi toka mwaka jana imesuasua kwa sababu tenda bodi ya pale Mkoani haipo na wanatumia tenda bodi ya kwa *RAS* pale.

Je, ni lini Serikali sasa itawezesha Mikoa kuwa na bodi ya manunuzi ili miradi iweze kuharakishwa?

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Philipo Mulugo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, inapendeza wote tukiwa na ufahamu wa pamoja kwamba hizi bodi huwa zina ukomo wa muda wake, bodi nyingi

zime-*expire* muda wake, tayari Mheshimiwa Waziri ameaanza kufanyia kazi na maeneo yote yatapata *boards* ambazo zitaharakisha utendaji wa kazi zetu.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, sasa unaweza kuketi.

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa *session* yetu ya maswali na majibu, maswali ya nyongeza ni mengi sana na kuna watu wengi sana wamenyoosha mikono waweze kuzungumza lakini nafasi isingeweza kutosha, hata hivyo tunawapongeza walioweza kuchangia wamechangia kwa ufupi pia Mawaziri wamejitahidi kujibu kwa kasi. Kwa mwelekeo huu tutapata fursa kubwa wote kuweza kuchangia. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wageni waliopo hapa Bungeni leo ni wageni waliopo Jukwaa la Spika; wageni kutoka Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Ndugu Charles Kichere - Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali *(CAG)*. Ndugu Benjamin Mashauri - Naibu Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Ahsante. Ndugu Salhina Mkuba - Naibu Mkurugenzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Ndugu Wendy Massoy - Naibu Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Ndugu Benja Majura - Naibu Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Ndugu George Haule - Naibu Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Ahsante. *(Makofi)*

Aidha, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ameambatana na Maafisa wengine Saba kutoka Ofisi yake wasimame kwa umoja wao. Karibuni sana kwenye Bunge letu. *(Makofi)*

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge; wageni 26 wa Mheshimiwa Anna Lupembe Mbunge, ambao ni wana maombi kutoka Jijini Dodoma wakiongozwa na Mtumishi Isaya Njendaluzi. Ahsante sana Watumishi wa Mungu. *(Makofi)*

Wageni 18 wa Mheshimiwa Daktari Ritta Kabati Mbunge, ambao ni wanakwaya wa Kwaya ya Vijana wa Kanisa la Mlima wa Bwana kutoka Jijini Dodoma, wakiongozwa na Askofu Silvanus Komba. Ahsanteni sana karibuni. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Ali Juma Mohamed Mbunge, ambaye ni Dada yake Ndugu Fatma Hassan Ali kutoka Mkoa wa Mjini Magharibi Zanzibar. Ahsante karibu.*(Makofi)*

Wageni 26 wa Mheshimiwa Noah Lemburis Saputu Mollel Mbunge, ambao ni wanachuo cha *East Africa* kutoka Jijini Arusha. Karibuni sana wanafunzi kutoka Arusha. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Edward Olelekaita Kisau Mbunge, ambaye ni Afisa Mtendaji Mkuu wa Muungano wa Jumuiya za Hifadhi ya Wanyamapori Tanzania, Ndugu Mohamed Kamuna kutoka Jijini Dar es Salaam. Ahsante. *(Makofi)*

Wageni Wawili wa Mheshimiwa Jackson Kiswaga - Mbunge, ambao ni wapiga kura wake kutoka Jimboni kwakwe Kalenga Mkoani Iringa. Karibuni sana wageni kutoka Mkoani Iringa, ambao ni pamoja na Ndugu Yoel Mofuga na Hadija Luvanga. Ahsante. *(Makofi)*

Wageni 11 wa Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo, Mbunge, ambao ni viongozi wa Serikali ya wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam wakiongozwa na Rais wa Serikali ya Chuo hicho Ndugu Godwell Lukumay. Rais yupo wapi wa Serikali ya wanafunzi? Ahsante sana, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni Wanne wa Mheshimiwa Philipo Mulugo ambao ni wapiga kura wake kutoka Mkoani Songwe ikiwa ni pamoja na Delias Nshiga, Petro Chungu, John Zawila pamoja na Frank Mwanaloga. *(Makofi)*

Tangazo la Katibu wa Bunge; Waheshimiwa Wabunge, Katibu wa Bunge anawatangazia Waheshimiwa Wabunge na Watumishi wa Ofisi ya Bunge kuwa Mtaalam wa Afya kutoka Hospitali ya Macho ya Dkt. Agarwal Tanzania wapo kwenye viwanja vya Bunge eneo la nyuma ya Ukumbi wa Msekwa kwa ajili ya kutoa huduma maalum ya upimaji wa macho pamoja na miwani. Huduma hii inatolewa kuanzia leo tarehe 11 mpaka tarehe 14 Aprili, 2022. Hivyo, Waheshimiwa Wabunge mnakaribishwa kupata huduma hiyo.

Waheshimiwa Wabunge, watalaam wanaotoa huduma hii wapo hapa ukumbini nao ni kama wafuatao; tunaye Daktari Emilius Chibuga - Daktari Bingwa wa Macho, Meneja wa Maendeleo ya Biashara - Ndugu Seleman Chilo, Ndugu Thomas Mbezi hawapo wote. Ahsante. *(Makofi)*

Tangazo la kikao cha Wabunge Wanawake wa CCM kitakachofanyika tarehe 12 Aprili katika Ukumbi wa Msekwa B. Wabunge Wanawake wa CCM mnatangaziwa kuwepo kwenye Kikao cha muda mfupi mara baada ya kuahirishwa kwa Bunge leo tarehe 12 Mwezi wa Nne, Saa Saba Mchana Ukumbi wa Msekwa B. Tangazo limetolewa kwa niaba ya Ofisi ya Katibu wa Wabunge wa CCM.

Tangazo lingine maalum, Mheshimiwa Waziri Mkuu Kassim Majaliwa anawaalika katika *Iftar* leo. Naomba kurejea Mheshimiwa Waziri Mkuu Kassim Majaliwa anawaalika katika *Iftar* leo Jioni mara baada ya kuahirishwa Shughuli za Bunge katika viwanja vya *parking* za Wabunge jirani na Zahanati ya Bunge. Waheshimiwa Wabunge wote, wafanyakazi wote wa Serikali na

Watumishi wote wa Bunge Mheshimiwa Waziri Mkuu anawakaribisha. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea, Katibu.

**NDG. ASIA MINJA – KATIBU MEZANI**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MWENYEKITI**: Tunaendelea na majadiliano na mchangiaji wetu wa kwanza kabisa leo atakuwa ni Mheshimiwa Deodatus Mwanyika, akifuatiwa na Mheshimiwa Livingstone Lusinde na ajiandae Mheshimiwa Judith Salvio Kapinga.

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia katika hoja iliyo mbele yetu ya ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza sana Rais wetu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa mambo makubwa ambayo wote tumeyashuhudia katika hiki kipindi cha mwaka mmoja na miezi kadhaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Njombe tumeshuhudia madarasa mapya mazuri, karibu madarasa 38 lakini tumeona maeneo ya afya, vituo vya afya vikiendelea kujengwa kwa kasi kubwa, lakini kubwa kuliko yote katika azma ya kazi iendelee tumeshuhudia hospitali yetu kubwa ya rufaa ikipata fedha zote ili iweze kukamilika na huduma iweze kuendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee kabisa nimshukuru sana Mheshimiwa Rais pamoja na Serikali ya Awamu ya Sita kwa kutekeleza na kuchukua hatua kubwa sana ambayo ilikuwa ni kilio kikubwa cha wananchi wa Njombe kutupatia barabara ya Itoni mpaka mpakani mwa Njombe na Ludewa. Tunaambiwa sasa barabara hiyo inakwenda kuanza kujengwa kwa sababu mchakato mzima wa manunuzi umekamilika na mkataba umesainiwa. Kwa hiyo, nishukuru sana kwa jambo hilo kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuongelea kuhusu uwekezaji. Nashukuru sana Serikali kuendelea kufungua milango na kuboresha mazingira ya uwekezaji, tumeshuhudia kwamba miradi zaidi ya 300 yenye gharama ya karibu Dola Bilioni 8.4 tunazungumzia Shilingi Trilioni 18, hili ni jambo kubwa sana kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kushauri kwamba bado tunaomba sana Serikali iendelee kupitia sheria na sera za uwekezaji ili ziweze kuendana na hali halisi. Tunadhani kwamba baadhi ya maeneo na mitazamo ya kisera inawezekana imepitwa na wakati hasa unapoangalia miradi mikubwa ya kimkakati kama Liganga na Mchuchuma. Tuondoke kule kwenye kuangalia zaidi kodi peke yake tuende kwenye kuangalia faida kubwa, tuangalie *multiplier effect. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sitaliongelea Liganga na Mchuchuma kwa sababu nina uhakika tutapata nafasi hapo mbele na kwa vile Waziri mhusika ameshatuambia kwenye Kamati kwamba ataongea nasi kutupa *update* ya suala hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kuendelea kuchangia kwenye eneo la kilimo, tumekuwa na changamoto kubwa sana ya mbolea na imeongelewa hapa, nipenda kushukuru sana Serikali kwa suala hili kwamba sasa kilio kikubwa cha Watanzania kimepata kusikika na Serikali imeamua sasa kwamba tutakuwa na mfuko wa pembejeo. Katika bajeti hii wananchi watapunguziwa maumivu, katika hali ya bei kupanda haya ni maamuzi makubwa sana na tumshukuru na kumpongeza sana Rais wetu kama alivyosema Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, utashi wa kisiasa katika jambo hili ulihitajika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Njombe ni moja ya maeneo yanayokuwa kwa haraka na takwimu zinaonyesha wazi ni Mkoa ambao una mchango mkubwa sana kiuchumi na hasa katika maeneo ya vijijini. Kwenye kilimo asilimia 90 ya wananchi wa Njombe ni wakulima na mchango mkubwa wa pato la Taifa unatoka katika kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili tuweze kufanikiwa zaidi katika Mkoa wa Njombe tunahitaji miundombinu wezeshi kwa kiasi kikubwa. Serikali yetu imekuwa na miradi mikubwa miwili ambayo inafadhaliwa na wafadhali ya kusaidia maeneo ya kilimo kutengeneza miundombinu wezeshi. Kwa bahati mbaya sana Njombe haikuwemo katika maeneo hayo au katika miradi hiyo, kwa sababu ambazo zimeelezewa kwamba ni Njombe Mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Njombe Mjini ni Jimbo lakini asilimia 70 ya Njombe Mjini ni vijiji ambapo ndipo uzalishaji mkubwa unapotoka. Napenda kuiomba sana Serikali pamoja na kwamba hatupo kwenye miradi hii mikubwa ya fursa za kiuchumi ya kufungua miundombinu wezeshi, tupate fedha za kutosha na ninawashukuru kwamba katika bajeti iliyopita tulichangiwa fedha za kutosha kiasi cha Shilingi 1.5 Bilioni kwa ajili ya maeneo ya vijijini. Ninaomba na mwaka huu tuweze kuangaliwa ili miradi ya kufungua maeneo ya vijijini na uzalishaji yanayokuza ajira kwa kiasi kikubwa, yaweze kupata fedha na barabara zetu ziweze kukabaratiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, upande wa elimu, tunashukuru Serikali kama nilivyosema tumeona makubwa lakini napenda kusema kwamba bado tuna changamoto kubwa ya watumishi, tuna tatizo la watumishi kiasi cha Walimu kwa upande wa Shule za Msingi karibu 350 hiyo ni *gape* ambayo tunayo. Tunashukuru Serikali na maamuzi ya Serikali kuwaajiri Walimu 32,000 tuna matumaini makubwa sana nasi katika kipindi hiki tutaangaliwa kwa jicho la karibu kwa vile tuna uhitaji mkubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo hilo lipo pia kwenye afya, tuna upungufu mkubwa wa watumishi katika afya. Lakini kwenye afya napenda kusema watu wa Njombe Mjini ni watu wa kujituma ni watu wa kufanya maendeleo, katika kilimo na katika kujitolea. Katika Mji wa Njombe tayari tulishajenga Vituo vya Afya kabla hata Serikali haijatoa mkakati wa kuwa na kituo cha mkakati cha afya katika kila Kata. Tuna vituo ambavyo vinakuja vimeshakamilika na vinangoja vifaa tiba na watumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuiomba Serikali kuangalia kwa karibu ili maeneo haya vituo hivi ambavyo vimeshakamilika kwa asilimia 90 na vinangoja tu vipate vifaa tiba viweze kuangaliwa ili huduma ziweze kumfikia mwananchi kwa karibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, upande wa umeme tunashukuru tunaendelea na mradi *REA*, lakini napenda kusema ni vizuri Serikali ikajitahidi tuweze kupata fedha za kutosha mradi huu ni mzuri na tunaelewa kwamba ndani ya miaka hii mitano vijiji vyote vitapata umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuwe *realistic* kwa *speed* ambayo *REA* wanakwenda nayo tunaanza kupata wasiwasi kwamba tutafanikiwa kukamilisha kupata hii miradi yote ya umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kuongelea jambo moja kubwa ambalo wananchi wa Njombe tuna wasiwasi nalo, aliongea Mheshimiwa Chumi hapa kuhusiana na nguzo za umeme, uchumi wa Njombe ardhi nzima ya Mji wa Njombe au Mkoa wa Njombe asilimia 30 ni miti ambayo ndani ya miti hiyo tunatoa nguzo na ndiyo tumesaidia nchi hii kuweza kuendelea na miradi mikubwa ya *REA*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa habari tuliyoisikia kwamba wenzetu wa *TANESCO* wanataka kuanza kuagiza nguzo kutoka nje ya nchi, jambo hili pamoja na kwamba la kibiashara lakini halina afya, litakwenda kuongeza umaskini kwa wananchi wengi ambao tayari wameanza kujikomboa na wanajitolea na kufanya kazi kwa bidii kujenga maisha yao, itapunguza mapato ya Halmashauri zetu kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia Halmashauri ya Njombe kwa mwaka tunapata kutoka katika msitu karibu Shilingi Bilioni Mbili ambazo zinakwenda kusaidia maendeleo ya wananchi. Vile vile tuna viwanda Sita

ambavyo vinashughulikia nguzo na katika muda mfupi huu viwanda vimeongezeka katika nchi ya Tanzania, kwa sababu sera zimefunguka na wawekezaji wanazidi kuja na kuna wawekezaji wa ndani hapa hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kampuni ya *TANWOOD* peke yake katika miaka miwili iliyopita imelipa zaidi ya Shilingi Bilioni Nne kama *corporate tax,* lakini inaajiri wafanyakazi wengi karibu 200 na inalipa mishahara ambayo ni mizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kujiajiri kuna Watanzania wananchi wa Njombe wengi wanajiajiri katika sekta ya misitu. Napenda sana kuiomba Serikali ifanye maamuzi ikizingatia kwamba katika Ilani yetu ya Uchaguzi tunataka kuwawezesha watanzania waweze kujitegemea wao wenyewe na sekta ya misitu inatoa hiyo fursa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naona muda wangu umeisha, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Judith Salvio Kapinga na Mheshimiwa Lusinde ajiandae, wakati huo Mheshimiwa Salim, Mheshimiwa Ester Bulaya na Mheshimiwa Halima Mdee wanajindaa.

**MHE. JUDITH S. KAPINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto ya ajira ni changamoto inayokumba nchi nyingi za Afrika na dunia kwa ujumla, tofauti pekee iliyopo kwa nchi ambazo tunakumbwa na changamoto ya ajira kwa vijana ni namna ama *approaches* tunazotumia kwenye kukabiliana na changamoto ya ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda niipongeze Serikali kwa *program* mbalimbali zinazofanyika kwa vijana kwa ajili ya kutatua changamoto ya ajira ikiwemo *program* ya kukuza ujuzi kwa vijana ambayo mpaka sasa imewanufaisha vijana zaidi ya 5,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi hizi ningependa nishauri masuala kadhaa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, *program* ya kukuza ujuzi ilitakiwa iongezwe na kuwa *program* ya kukuza ujuzi pamoja na mitaji. Nasema hivi kwa sababu ninaogopa kwamba tunapoelekea *program* hii ya ujuzi inaenda kuleta daraja lingine la wahitimu tofauti na wahitimu tulionao wa vyuo vikuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *program* hii kama nilivyosema imezalisha wahitimu zaidi ya elfu tano ambao hawana mitaji wapo mitaani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tofauti ya mhitimu wa *program* ya ujuzi na mhitimu wa Chuo Kikuu ni kwamba wa Chuo Kikuu anakuwa na ujuzi wa darasani huyu anakuwa na ujuzi wa stadi za kazi lakini wana-*share* kitu kimoja wote hawana ajira na hawana mitaji. Halmashauri zetu Tanzania nzima karibia 185 zinatoa takribani Shilingi Bilioni 28 kila mwaka kwa ajili ya mikopo ya vijana, *program* hii ya ujuzi imetengewa Bilioni Tisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani haina tija *program* kutengewa Bilioni Tisa halafu iende kwenye mafunzo, mikutano, tathmini na masuala mengine ambayo hayaweki masuala ya mitaji kwa vijana halafu tumeweka Bilioni Moja ya mitaji kwenye Mfuko wa Maendeleo ya Vijana, naona hapa hesabu hazijakaa sawa yaani Bilioni Tisa iishie kwenye mafunzo halafu Bilioni moja iende kwenye mitaji nadhani ilitakiwa iwe *vice versa*. Bilioni Moja ya mafunzo, Bilioni Tisa iwe ni mitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafunzo ni muhimu lakini haiwezekani tukaweka Bilioni Tisa kwenye mafunzo halafu bilioni moja kwenye mitaji sisi kama vijana haturidhiki tuambiwe kwamba kuna vijana 5,000 wamepewa mafunzo na wako mtaani haiwezekani tunaomba Wizara itusaidie ili fedha hizi zinazotolewa ziweze kuwa na tija kwa vijana *end result* lazima iwe ajira ama mitaji kwa vijana lakini siyo kuongeza idadi ya wahitimu ambao wanaenda kukaa mitaani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatusaidia sana kuwekeza kwenye masuala ya *ICT* na kwa kweli nipongeze Serikali *digital infrastructure* imewekezwa kwa kiasi kikubwa, mfano ni *National* na *Regional ICT broadband backbone* ambayo imeweza kuwa *connected* kwenye *three International undersea cables.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inafanya uwekezaji kwenye *ICT* kwa maana ya kukuza matumizi ya teknolojia na tunategemea kwamba Wizara nyingine itaenda sambamba na utekelezaji wa mambo kama hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara inayohusiana na masuala ya vijana ninadhani inabidi wawasaidie vijana kuwekeza katika *program* za ubunifu ili waweze kutumia hizi *infrastructures* ambazo zinatengenezwa na Serikali lakini leo hii *startup programs* tunawajima mikopo ya vijana. Sasa ninapenda niwaulize hivi tumeambiwa *model* ya kutoa mikopo ni ile tu ya kusaidia vijana ambao wanataka kufanya *physical investment* kama viwanda? tunapoelekea kweli tunahitaji kukumbushana kwamba sayansi na teknolojia ndiyo habari ya mjini? Kwa hiyo, Serikali inawekeza hii miundombinu ili tufanye nini sasa kama vijana hawawezi kupewa mikopo ili wawekeze kwenye *startup programs?*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaamini Serikali inaweka miundombinu ili vijana waweze kufanya *program* za ubunifu ambazo zitasaidia kutoa huduma lakini zitasaidia kuajiri wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *startup program* ikiwa *properly invested* inaajiri zaidi ya vijana hata 100. Sasa kwanini hatuoni hili? Wataalam watusaidie! Haiwezekani tukawa tuna *model* moja ya kutoa mikopo ya vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana wote ni sawa, wale wenye bunifu na ambao wanataka kufanya *physical investments* wote ni wa aina moja na wote ni vijana wa Tanzania. Wizara ipanue mawazo ku- *accommodate* vijana ambao *they want* kufanya *startup programs.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii tunawaambia benki wawakopeshe, watawakopesha vipi kama sisi wenyewe tu tunashindwa kuwakopesha. Kwa hiyo tunaomba Serikali itusaidie vijana hawa wapo wengi mno, *startup programs* zipo tunahitaji uwekezaji hapa ili *infrastructure* zinapotengenezwa na Serikali ziweze kusaidia vijana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ndiyo tunaongoza *East Africa* kwa idadi kubwa ya watu *(population),* hapa tunavyoongea tupo kwenye kuweka sera kwa ajili ya uhamaji wa nguvukazi ndani ya *East Africa*. Tusipokuwa makini changamoto ya ajira itaendelea kukua hapa nchini kwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda nitoe mfano, *startup program* 24 katika Afrika Mashariki ziliomba *capital* ya pamoja na wakaweza kupatiwa zaidi ya USD Milioni Moja. Nataka niwaambie Tanzania *startup program* zilikuwa ngapi? Ilikuwa ni Moja, 17 Kenya, Sita Uganga. Sasa tunapoendelea huku kwenye masuala ya uhamaji wa nguvu kazi lazima tuhakikishe tunaweka mambo yetu vizuri ili tuweze ku-*compete* katika Afrika Mashariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo langu la mwisho kuhusiana na mikopo ya Halmashauri. Mikopo hii haina mjadala, inasaidia vijana wengi sana, lakini sasa hivi tumeenda kwenye aina ya kuweka mikopo kwa maana ya viwanda. Utaratibu uliokuwepo huko mwanzoni, ule muda wa vijana kuweza kufanya marejesho ya mikopo ilikuwa ni miezi mitatu, lakini ilikuwa ni kwa sababu tulikuwa tunatoa *startup capitals* za Milioni mbili mpaka Milioni tano, lakini *model* ya sasa hivi ni viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezekani wakaanza kufanya marejesho ndani ya miezi mitatu kwa sababu wote tunafahamu mpaka uweze kupata vibali *SIDO*, uweze kupata vibali *TBS* sijui *BRELA*, ufungiwe umeme kule kwetu kijijini Mbinga ni zaidi ya miezi mitatu. Kwa hiyo, tunaomba Wizara ipitie kanuni upya ili vijana hawa wanaopewa mikopo kwa maana ya kuanzisha viwanda, mikopo, majeresho yaweze kuongezeka muda, *at least* wapewe muda wa matazamio miezi Sita. Ndani ya miezi mitatu kwa kiwanda huwezi kufanya marejesho kuangalia na hali yetu ya Kitanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho na hili suala sitaogopa kulirudia na naliongea mara nyingi sana. Wizara ya Vijana lazima msaidie Wizara nyingine iweze kuona mambo yenye tija kwa vijana, hususani pesa za kimtandao kwa malipo nje ya nchi. Nalirudia tena tunataka *PayPal* iweze kufanya kazi hapa Tanzania. Kama Wizara ya Fedha hawalioni, Waziri utusaidie kuwaonesha kwamba vijana wanaojiajiri hapa Tanzania wanahitaji kulipwa na wenyewe kupitia njia hizo, siyo tu sisi tulipe alafu tusilipwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunapoendelea kupambana na changamoto za ajira sisi kama vijana tunaumia roho kwamba sisi tunakuwa tu ni soko la watu wengine kuchukua bidhaa zetu lakini sisi hatuwezi kuuza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Wizara mtusaidie muwaambie Wizara nyingine kwamba vijana wa Kitanzania kwa sababu ninyi ndiyo mna uchungu na ajira za vijana, muwaambie Wizara nyingine haya masuala yanayohusiana na vijana ni lazima yachukuliwe kwa tahadhari kubwa sana na kwa u-*serious* mkubwa sana kwa sababu changamoto ya ajira ni kubwa sana nchini kwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo tunategemea katika Bunge hili la Bajeti suala la *PayPal* tunaomba litafutiwe ufumbuzi. Tumeshalizungumza hatuwezi kuzungumza kitu hapa zaidi ya miaka tisa hadi kumi na Serikali mpo. Tunaomba mtusaidie *PayPal* ifunguliwe, vijana wafanye malipo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Sasa namuita Mheshimiwa Livingstone Lusinde aweze kuchangia. *(Makofi)*

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa mwaka 2022/2023. Vilevile nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Mkuu na Amiri Jeshi Mkuu Mheshimiwa Rais, Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa ambayo wamekuwa wakiifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nianzie ukurasa wa 18 Ibara ya 26 ya hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu anazungumzia habari ya kufanya mapitio ya sera ya uwekezaji. Tanzania tuna Wizara ya Uwekezaji na Ukuzaji wa Mitaji kwa Umma. Ukiitazama bajeti ya Wizara hiyo na kama Wizara hiyo itaamua sasa kuihamishia bajeti hiyo kwenye kukuza mitaji ya wananchi wenzetu tutasogea mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nini nataka kusema hapa. Badala ya kila siku kusema Wizara inashughulika na sera, hapana! Wizara sasa iende ikuze mitaji ya watu na ituletee orodha ya wananchi ambao mitaji yao imekuzwa. Hivyo ndivyo tutakavyotengeneza mabilionea wa nchi yetu.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusiwe na Wizara za kisera tu, sasa una Wizara ya Uwekezaji na Ukuzaji wa Mitaji ya Umma halafu huna mtu hata mmoja wa kutolea mfano kwamba mtaji wake umekuzwa, hiyo inasaidia nini? Haisaidia chochote!

Mheshimiwa Mweyekiti, kwa hiyo ninataka niishauri Serikali kama kweli tuna Wizara ya Uwekezaji na Ukuzaji wa Mitaji ya Umma basi mwakani watuletee hapa orodha ya wafanyabiashara waliokuwa na mitaji midogo, mitaji yao imekuzwa nakufikia hatua ya juu. Vinginevyo tutakuwa na Wizara inatamkwa vizuri lakini kazi inayofanyika haionekani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazungumzia habari ya mfumuko wa bei. Juzi hapa tulipata maoni mengi sana kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge. Tulimsikia Mheshimiwa Shabiby akisema, tukamsikia Profesa Kitila Mkumbo akisema, tukamsikia Mheshimiwa Tabasam akisema. Nini nataka kusema hapa, ili tuwe na uelewa wa pamoja tunaomba Wizara pamoja na taasisi zake ikiwemo *EWURA* waje hapa Bungeni watupe semina ya pamoja tenda zinatolewaje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiwa na uelewa wa pamoja Wabunge ni rahisi sana kuishauri Serikali vizuri kuliko kila Mbunge akiwa na uelewa wake. Huyu anasema tenda zinatolewa kimagumashi, huyu anasema watu wanne ndiyo wanaopanga, haya mambo yanaumiza sana watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niwaambie nchi yetu tusisahau kwamba ni nchi maskini na Wabunge hata nikiwemo ninayezungumza natokana na familia maskini. Kuna watu leo wanashindwa kula, wanakula mlo mmoja, hali ni mbaya sana mtaani hatuwezi kufanya kama hatuoni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali wakati wa njaa kubwa ikitokea hapa, tunaona Serikali inafungua maghala ya Serikali inashusha bei ili kupunguza makali. Vipi Serikali haifungui maghala ya mafuta ya Serikali? Kama haina kwa nini? Kwa nini tusianze mchakato wa kutengeneza maghala tuwe na mafuta ya Serikali ikitokea bei kubwa kama hii Serikali inafungua maghala yake inashusha bei ina-*regulate,* mambo yanakaa sawa. *(Makofi)*

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti taarifa!

**MWENYEKITI:** Taarifa kutoka wapi?

**T A A R I F A**

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimweleze mchangiaji kwamba Serikali inayo maghala, inayo maghala

TIPER, Oryx ana 49 na Serikali ina 51, Serikali ina maghala mengine tena kama BP, kule BP ambapo sasa hivi ni PUMA tuna zaidi ya Milioni 80 ya kuhifadhi mafuta. Endelea mchangiaji.

**MWENYEKITI:** Unaipokea taarifa Mheshimiwa. Haya endelea.

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naipokea taarifa yako Mheshimiwa Tabasam. Ninaiomba Serikali ifungue maghala kama yapo. Ndugu zangu mnakumbuka Waheshimiwa Wabunge wote wakati wa shida ya chakula Serikali hufungua maghala yake na kushusha bei ya mahindi. Ikishusha bei ya mahindi tunaona wafanyabiashara nao wanashusha. Kama Serikali ina maghala na ina mafuta iyafungue sasa ili bei ya mafuta ishuke. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezekani tuwe tunazungumza tu yatapanda tena. Lakini vilevile Mheshimiwa Mwenyekiti hebu ninaomba nisaidie muda wangu huo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Unazungumza na kiti, endelea.

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niiombe Serikali…

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa!

**MWENYEKITI:** Taarifa kutoka wapi? Mheshimiwa Shangazi aah! umesimama hapo. Mheshimiwa Shangazi taarifa. *(Makofi)*

**T A A R I F A**

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza pamoja na mchango mzuri wa mzungumzaji lakini ninataka tu nitoe taarifa kwamba Serikali ina zile *facility* lakini *stock* iliyoko kwenye maghala yale siyo ya Serikali. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lusinde unapokea taarifa?

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama taarifa ya Mheshimiwa Shangazi ni ya kweli basi tuna mtihani mkubwa sana. *(Makofi/Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Endelea Mheshimiwa Lusinde.

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna mtihani mkubwa kwa sababu jambo kubwa kama hili ndugu zangu hivi hata kweli ndio imetokea shida purukushani hayo mafuta tunayatoa wapi? Hili ni jambo

kubwa sana ni suala la usalama wa nchi. Kweli kabisa Taifa hili likose maghala ya Serikali ya kutunza mafuta? Hii ni hatari. Hatari kubwa sana hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo ninakuomba Serikali kama kweli hakuna, hili tatizo ni kubwa wala siyo jambo la kufumbia macho, tuende tupange bajeti tuanze kutengeneza maghala ya kutunza mafuta ili tuwe na hifadhi ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine mimi nakushuru sana.

**MHE. CHARLES J. MWIJAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa!

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwijage taarifa.

**T A A R I F A**

**MHE. CHARLES J. MWIJAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nimpe taarifa mzungumzaji kwamba pamoja na Serikali haina mafuta kwenye maghala yale ya kwake lakini kutokana na *location advantage* na mfumo wa kudhibiti mafuta Tanzania nchi yetu iko salama na ina mafuta ya kutosha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Unapokea taarifa Mheshimiwa Lusinde?

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, yaani sasa tena Mwijage unataka kunipiga siasa hata mimi Mbunge mwenzako bwana? Hili jambo ni zito. Jamani eeh! hili jambo ni kubwa. Hili jambo tusiliongelee kwa lugha hiyo. Tusipige siasa kwenye mambo ya hatari. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wajumbe muacheni Mbunge achangie. Endelea Mheshimiwa Lusinde.

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi kufika mahala inakosa akiba ya mafuta ya Serikali halafu tunasema nchi iko salama! tunasema hali ni nzuri! Hii jamani tutakuwa tunajifungia humu ndani tunajidanga. Hapana, hapana, hapana! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima tuwe na utaratibu mzuri na nataka nikwambie, nisikilize. Sisi hali hii siyo ya kwanza, alizungumza hapa Profesa. Sisi vita imeshapigana kwenye eneo ambako ndiko tunanunua mafuta. Ishapigana na Uajemi vita lakini hali yetu haikufikia kama hii ambayo vita inapigana Urusi ambako ni mbali. Sasa hebu niambie kama hali hii vita wanapigana Urusi na Ukraine. Je ingepigana hapa *OPEC* ambako ndiko tunanunua mafuta tungeishi hapa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii kuna watu wanashindwa kufikisha wagonjwa hospitalini wanakufa. Ndugu zangu kukodi pikipiki gharama imeongezeka mara kumi. Vijijini huko lita moja ya *petrol* inauzwa Shilingi Elfu Nne, nani atakubali kumsafirisha mgonjwa wako kumkimbiza? A*mbulance* za Watanzania ni pikipiki za vijijini!

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya mambo lazima tuyazungumze katika ukubwa wake tusiweke mambo ya siasa kwenye jambo hili, hapana tumsaidie mama kwenye jambo hii. *(Makofi)* Kwa hiyo, mimi ninasema hapa hii itasaidia kushusha mfumuko wa bei.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna miaka 60 ya kuongoza hili Taifa, tunashindwaje kuwa na hifadhi ya mafuta ya kwetu, tunashindwaje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya naona alikuwa amesimama Waziri wa Fedha.

**MWENYEKITI:** Nimemuona Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango. Karibu uchangie.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nitambue mchango wa mchangiaji na jambo analochangia ni jambo la msingi na ni jambo kubwa, kitu ambacho ninataka kukisema ni kwamba sambamba na mchango wake na dira hiyo anayoisema, Serikali inalifuatilia kwa umakini mkubwa sana jambo hili na siyo tu kwa maana ya hivi vita vinavyoendelea pamoja na majanga mengine yanayojitokeza lakini Wizara imeendelea na dira hiyo hiyo ya kufufua Tanzania iwe na akiba ya kutosha na siyo tu yakutosha kwa maana na majanga lakini iwe *focal point* kwa sababu ni *entry* ya nchi nyingi za ukanda huu hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo tunaenda kuwa na akiba ya kutosha siyo tu kwa ajili ya majira haya ya sasa ya vita, lakini tutakuwa na utaratibu tu wa kuwa na mafuta ya kutosha na *actualy* tuta-*supply* na kwenye nchi majirani kwa sababu lango la mafuta haya katika ukanda huu linapitia kwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuhusu hiki kinachoendelea ambacho ni cha sasa hivi, tumesema hata jana tumetoa kauli ambayo tumewaambia wananchi kwamba tunaenda kuangalia baadhi ya maeneo ambayo hayagusi *Development Budget* yanayogusa *Other Charges* matumizi ambayo yanaenda kwa njia ya makato kwenye *TBS, EWURA* na maeneo mengine *TPA*, *customs* tunaenda kuyaangalia yale ili tuweze kuchomoa ili kuweka unafuu kwa wananchi na wakati ule ule Hazina iweze kuzisaidia zile taasisi zilizokuwa zinachukua kwenye mafuta. Maana yake tutoe unafuu kwa wananchi lakini Hazina na taasisi zingine ambazo zilikuwa zinachukua kwenye eneo lile tuweze kuangalia namna ya uendeshaji ndani ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo hili ni jambo ambalo linafanyiwa kazi na liko kwenye vipaumbele vya Mheshimiwa Rais na viko kwenye dira ya Wizara na Serikali inaipa umuhimu mkuwa kwa sababu mafuta ni injini ya uchumi wa nchi yoyote ile.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lusinde.

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, bado narudia kwanza tukubaliane kwamba ni lazima tuwe na hifadhi ya mafuta ya kwetu kama nchi, kama Taifa. Mafuta ya Serikali kuacha hivi visheli vya Serikali magari yanapita Mawaziri kuweka mafuta. Tuwe na hifadhi ya mafuta ya nchi, sisi kama Taifa ili hata ikitokea huko duniani kuna shida, sisi tunakuwa nayo. Jamani tunashindwaje kutunza? Watu wa kawaida tu wanatunza chakula wakati wa njaa anaenda anafumua watoto wanaishi, hayo ndiyo ninayoyataka maono yetu yawe hapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ni lazima inapotokea *crisis* kubwa kama hii tuiangalie jamii. Tuangalie maisha ya watu mtaani tunayafanyaje? Haiwezekani tuwe tunaendelea kupanga. Tunapanga maendeleo, tunapanga matumizi makubwa kana kwamba hakuna tatizo. Hiyo haiwezekani! Tukijifungia humu tuelewe kwamba Watanzania wana wakati mgumu sana kutokana na hii hali iliyopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nihame hapo niende kwenye kilimo. Hebu niwaombe Serikali Maprofesa wale wa *SUA* pale watutengenezee mtaala wa kilimo ufundishwe kuanzia shule ya msingi mpaka sekondari. Kwa kufanya hivyo tutakuwa na wataalam wa kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu anayeishia Darasa la Saba atakuwa anajua kilimo kwa kiwango fulani. Anayeishia Sekondari atakuwa anajua kilimo kwa kiwango fulani. Kwa utaratibu huo watu watalima kilimo siyo cha chakula tu. Tutakuwa na kilimo cha biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezekani Taifa kama hili tunazungumzia habari ya kumpa leo mtu pikipiki, kumpa Afisa Ugani kipimo. Yale yote tukiyafundisha shuleni tutakuwa na Maafisa Ugani wa kiwango hicho nchi nzima. Lazima watu wetu wafundishwe namna ya kutunza chakula. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Kilimo Bashe, anafanya kazi vizuri sana lakini tumuongezee nguvu kwa kutengeneza mtaala wa elimu ya kilimo ufundishwe mashuleni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine nataka kuzungumza ni kuhusu ahadi za viongozi. Hivi ndugu zangu akiahidi Rais kwa Watanzania nitafanya jambo Fulani, halafu nyinyi watu wa Wizara hiyo hamtekelezi, ndiyo maana mwaka jana nilisema na leo narudia, tuweke kwenye kitabu kimoja ahadi za Marais, ziandikwe kwenye kitabu cha peke yake ili mwakani anaposimama

hapa Waziri Mkuu anatueleza katika ahadi za Marais walizoahidi sehemu fulani imetekelezwa hii, imetekelezwa hii, imetekelezwa hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa utaratibu huu wa kwenda pamoja hivi tutakuwa tunatoka kwenye reli. Wananchi wanashangaa Rais anaahidije jambo lisitekelezwe? Sasa wasubiri nani aahidi? Rais alishaahidi kutengeneza barabara ya Mvumi kwa lami. Alishaahidi kujenga pale barabara ya Mvumi kwenda kuunganisha na barabara ya Iringa, leo ni hii mwaka wa 10 huu ni Mbunge nazungumzia ahadi ya Rais. Sasa watu wanauliza hivi akisema Rais kuna nani mwingine tena mkubwa wa kuzuia? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivyo Marais wameahidi kwa Wabunge karibu wote. Tutengenezeeni kitabu hata Ilani, tutengenezeeni kitabu cha ahadi za Marais waliopita na zilivyotekelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la MSD Rais alishalitolea maamuzi suala hili. Rais ameagiza kwamba MSD ifanyiwe *overhauling,* sasa Wabunge kuanza kueleza nani alikuwa anafanya kazi vizuri. Nani aaah! siyo kazi ya Bunge, tusubiri hiyo *overhauling* inafanyikaje, tumuache Rais atengeneze pale ili utaratibu uweze kwenda. Rais amesema haraka kwa hiyo nina hakika kabisa *soon* mambo yatakaa sawa pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie jambo kidogo hapa, kuna maneno yanazungumzwa mitaani kuhusu Mheshimiwa Waziri Nape kuzunguka kwenda kuhamasisha anuani za makazi. Hapa ndipo panatuonesha wapi lipo tatizo. Tatizo lilipo siyo kwa Nape. Mheshimiwa Nape ameona kazi iliyofanyika mpaka sasa hivi ni asilimia 68 bado asilimia 32 na muda umeisha. Nategemea kwamba baada ya kumaliza ziara Mheshimiwa Nape hili jambo tutakuwa tumelikamilisha kwa asilimia 100. Kuna viungo vyetu havifanyi kazi sawa sawa. Tuna Wakurugenzi, tuna Wenyeviti, tuna Watendaji, tuna Ma-DC kwa hiyo, tuna uhakika akirudi hapa atatuambia wapi panavuja ili tuweze kusukuma nchi iweze kwenda. Kwa hiyo tusilaumu tu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Lusinde, nilikuongeza dakika Mbili nazo zimekwisha, ahsante sana kwa mchango wako. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa namuita Mheshimiwa Ester Bulaya, Mheshimiwa Halima Mdee, Mheshimiwa Salim Mussa Omar na Mheshimiwa Rashid Abdalla ajiandae.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza hoja aliyoongea Mheshimiwa Lusinde ni ya msingi. Ni kweli mtaani hali mbaya, ni kweli jambo hili Serikali mnatakiwa mlichukulie kwa udharura wake. Mliotoka Mikoani mnajua na maeneo

mengine mnajua hali siyo nzuri ya upandaji wa mafuta pamoja na bidhaa mbali mbali. Kwa hiyo, ni jambo la msingi wananchi wana hali mbaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Wabunge, kama wawakilishi wa wananchi kuna wajibu mkubwa wa kulitafakari kwa kina suala hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesoma hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba nijielekeze ukurasa wa 44. Mheshimiwa Waziri Mkuu amesema Serikali ina mpango wa kuagiza ndege zingine ili zifike 16. Ni jambo jema sana na hakuna mtu anayepinga ununuzi wa ndege.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa tunazungumzia hapa, hivi tunaendaje kufufua Shirika la Ndege? Kununua ndege peke yake ni kulifufua? Hili shirika kuna mipango madhubuti ya uendeshaji wa kibiashara? Je, tumeweka mikakati ya kuhakikisha ufufuaji wake utaongeza Pato la Taifa na uchumi kwa Taifa letu? Hayo ni mambo ni mambo ya kujiuliza, lakini suala la ndege kila Mtanzania anaona umuhimu wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, 2016 wakati Shirika la Ndege linafufuliwa kwa Bombadia mbili ilikuwa na mtaji hasi Shilingi Bilioni 146, leo ina mtaji hasi Shilingi Bilioni 240, ukilinganisha mtaji na madeni ya takriban Shilingi Bilioni 371 haviendani! Sasa sawa tunaleta ndege hali ya Shirika la Ndege ni mbaya na Mheshimiwa Rais pia alisema linatakiwa lifanyiwe utaratibu liweze kujiendesha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunaleta ndege na matokeo yake ni nini, shirika hatujalipa mtaji, hatujaliwekea mikakati ya kibiashara, tumenunua ndege hatujalipa madeni ya ndani na nje ya nchi, ndege zinakamatwa, Serikali walichofanya wakakabidhi ndege kwa wakala! Wakala ni wa Serikali haizuii ndege kukamatwa, bado ni mali ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbaya zaidi wakati wanakabidhi wakala wa ndege *(TGFA)* lengo kubwa lilikuwa moja tu ni kwamba ndege zikinunuliwa zisikamatwe na wakasahau yule ni wakala wa Serikali wala hakukuwa na mpango wa biashara, bado tu ndege zilikamatwa!

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaongeza gharama za uendeshaji, tunaongezea mzigo *ATCL* bila sababu na sababu siyo kukwepa ndege zisikamatwe sababu hapa kumaliza tatizo ni kulipa madeni na kuliongezea shirika mtaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ndiyo naifananisha wakati tunasema mifuko ya hifadhi ya jamii ina hali mbaya wakaona walete sheria waiunganishe badada ya kulipa madeni kwenye mifuko ya hifadhi ya jamii, ndiyo kinachotokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna madeni ndani na nje ya nchi hatutaki ndege zikamatwe tukapeleka kwa wakala haikuzuia ndege zinakamatwa kwa sababu yule wakala bado ni wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo hapa ni kuweka mikakati dhabiti ya uendeshaji wa shirika letu tulipe madeni ndani, nje ndege zetu ziruke, tuitangaze nchi yetu na huku uchumi ukue. Sasa hii taarifa ni ya Serikali yenyewe wanasema hata Serikali ilivyohamisha umiliki kwa wakala *TGFA* bado haijaleta ufanisi na gharama za uendeshaji zimepanda zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitolee mfano unapozungumzia matengeno ya ndege *ATCL* wao wenyewe wanatengeneza ndege kwa gharama kubwa kwenye kukarabati injini kwenye karakana zao. Lakini hapohapo wanalazimika kutoa tozo kulipa tozo za ukarabati kwa wakala, siyo sawa! Imeshafika zaidi ya takribani Shilingi Bilioni 99 madeni juu ya ukarabati wa ndege kwa wakala lakini wao wenyewe pia matengenezo makubwa wanayafanya kupitia karakana zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuwezi kwenda hivi, shirika haliwezi likawa na tija, lazima tujitafakari na uzuri hatujachelewa ni shirika letu wote tunapenda kuona fahari ya ndege, tukae tujipange namna bora ya kuendesha shirika letu la ndege. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano nikutolee mfano kwa miezi Minne ile ya *COVID-19* ilivyopamba moto, ndege hazikusafiri, lakini kwenye tozo peke yake ililipwa Shilingi Bilioni 15 ndege hazikuruka, kwenye ukarabati Shilingi Milioni 17 ndege hazikuruka miezi minne, sasa tunajiuliza kwa nini, hivi vyote tunafanya kwa ajili ya nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini tusiokoe hizi pesa zikaenda kutekeleza miradi mingine tukapunguza hali ngumu kwa wananchi wetu. Kwa nini haya madeni hizi hasara ambazo zinatengenezwa ambazo sasa hivi zimeshafikia zaidi ya Shilingi Bilioni 130 tungeenda kumaliza ahadi ngapi zilizotolewa kwenye majibu yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini tunaendelea kulazimisha mkataba kwa wakala ambao ndege zinajiendesha bila faidi, zinajiendesha kwa hasara ambazo hizo hasara tungeweza kupunguza tukaenda kumaliza matatizo ya maji kwenye majimbo yetu tukamkomboa kumtua mwanamke ndoo kichwani? Ni sisi tu wenyewe kupanga ni kuchagua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesoma pia ukurasa wa 39 wa Mheshimiwa Waziri Mkuu amesema wameweza kulipa pesa za mifuko ya hifadhi ya jamii zaidi ya Shilingi Bilioni Mbili kutumia hati fungani, sawa na hii ni ile ya *Pre-98* sasa mimi niulize hii tu mmetumia miaka 22 ya *Pre-98* hizi. Je, mtahitaji miaka mingapi mlipe madeni ya fedha za mifuko ya hifadhi ya jamii pesa ya wastaafu ya kuanzia mwaka 1999 kwenda mbele mnahitaji miaka mingapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa hizi hela mnakuwa kama mnazichukuwa tu hamlipi kwa riba, lini mlikopa kwenye mabenki mkalipa bila riba? tukisema hizi pesa za wastaafu wetu mnazitumia ndivyo sivyo, ndiyo maana wanakaa zaidi ya miezi sita zaidi ya mwaka hawajalipwa viinua mgongo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana tu wakati napitia simu yangu nikapata meseji, wastaafu wazee wangu kwenye Maktaba Kuu ya Taifa hawajalipwa na pesa zingine ile ni Maktaba ya Serikali Mwajiri hajapeleka michango wamepunjwa kwenye kiinua mgongo chao, kwa nini tunafanya haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana pesa za wastaafu zisichukuliwe poa! siyo sawa hawa wametumikia nchi yao kwa jasho na damu, mmekaa na hela za watu miaka 22, leo hapa Waziri akasema tunalipa kwa hati fungani hizo nyingine mtatumia miaka mingapi mliochukuwa kwenda kuwekeza kwenye viwanda na bado havijalipa vinatengeneza hasara. Mmechukuwa mkaenda kuwekeza kwenye majengo ambayo hayafanyi kazi hayajalipa, mtatumia miaka mingapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je watumishi wa Taifa hili waelewe nini wanayoipenda nchi yao, hawavumilii hawana wa kuwasemea ndiyo sisi tunakuja kuwasemea na bado wanafanya kazi kwa sababu wanajua kufanya kazi kuilinda nchi yao ni jukumu la kila Mtanzania, tuwatie motisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wafanyakazi hatujawaongeze mishahara hatujawapandishia madaraja na bado pesa zao za hatma ya uzeeni hatujui zinafanya nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Sasa namuita Mheshimiwa Halima Mdee aweze kuchangia.

**MHE. HALIMA J. MDEE**: Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Mheshimiwa Bulaya anapitia shirika letu la *ATCL* nimejaribu kupitia taarifa ya *CAG* ambayo imedondoshwa asubuhi hii, unajua tunajaribu kuwa *current* kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *CAG* anasema mapitio yangu ya utendaji wa kifedha wa Mashirika ya Umma yalibaini kuwa masharika 10 niliyoyakagua mwaka huu, yakiwemo mashirika mawili ya kibiashara katika sekta ya umma, kampuni ya ndege na kampuni ya … yalikuwa na mtaji hasi kama inavyooneshwa kwenye Jedwali Namba 6.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaenda kwenye jedwali Na. 6 anasema, ni maoni yangu kuwa kuwa na madeni mengi kuliko mali kuna tia shaka iwapo mashirika hayo yanaweza kuendeleza huduma zao na kutimiza

wajibu wao katika siku zijazo. Ukienda Jedwali la Sita mashirika ya umma yenye mtaji hasi katika mashirika yote kampuni yetu pendwa ya ndege iko Namba Moja, jumla ya mali Milioni 295, jumla ya madeni Milioni 535, mali hasi Bilioni 239.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni shirika ambalo kati ya maeneo ambayo naweza nikasema manne wakati wa Awamu ya Tano na ya Sita yaliyotengewa fedha nyingi sana kuliko maeneo mengine. Kwa tuliokuwepo kipindi hicho tulisema tumeanzisha shirika hili, tumenunua ndege wakati shirika halina mpango wa biashara!

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulisema tukapuuzwa lakini leo taarifa za Serikali zinaonyesha bayana kwamba wakati tunatoa Shilingi Trilioni 1.5 mwaka 2016 ndiyo wakati ule huo huo mpango wa muda mfupi wa biashara unatengenezwa. Matokeo yake ni nini? Mtaji hasi aliouzungumzia. Tunanunua ndege Serikali kama Mwanahisa Mkuu haweki *capital* halafu unategemea eti ndege ndiyo zijiendeshe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati huo huo, unajiuliza kuna maneno nikiyatumia hapa sipendi kukera watu. Unamtumia wakala wa ndege eti mapacha wawili mnapangia dili ya biashara! Yaani wewe na mtoto wako, Serikali *ATLC* ni mali ya Serikali, wakala wa ndege ni mali ya Serikali, eti wakala wa ndege ana mkodisha *ATLC* ndege ambayo iko dhoofu *bin* hoi! Sasa matokeo yake ni nini? Matokeo yake ni kwamba huyu mtu ambaye hamjampa mtaji, huyu mtu ambaye ana madeni nimesema hapa zaidi ya Shilingi Bilioni 500 sasa hivi, anaongezewa madeni mengine eti na mtoto mwingine wa Serikali anaitwa wakala wa ndege, jamani hizi ni akili jamani! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaongea kwa sababu Mheshimiwa Rais alihutubia Bunge hapa na wengine tulisema tulipinga *from the beginning* siyo ufufuzi wa shirika ila namna lilivyofufuliwa. Mheshimiwa Rais akasema, tutafanya utaratibu Mheshimiwa Samia tufanye maboresho ya shirika letu tulipunguzie mzigo, sasa leo deni nimezungumza hapa Shilingi Bilioni zaidi ya 500.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia mpango wa biashara wa *ATLC,* ngoja niwatajie safari zake walikuwa na mpango wa kwenda Johannesburg, safari za kimkakati za biashara Nigeria, walikuwa wanataka kwenda *London* na maeneo mengine ya Bara la Ulaya, lakini sasa ukija huku ndugu zangu kwa mujibu wa hotuba ya Waziri Mkuu sasa Arusha, Geita, Mtwara, Songea, Bunjumbura, Entebe, Harare, Lusaka, halafu wameanzisha vituo vitatu vya kimagumashi hivi Lumbumbashi, Guangzhou**,** Mumbai. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *why* tuna-*divert* kwenye mpango wa biashara? tunaogopa kwenda mbele watakamata ndege zetu, *with due respect* ni kweli ni faida kuwa na ndege 16 hadi zinapaki pale *airport good!*

yaani *we are so proud, very proud* lakini unakuwaje na ndege ambazo hazikuletei tija? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanasema hapa hivi unafikiria kwa sababu eti mmempa wakala wa ndege ambaye anamuongezea mzigo *ATLC* ndiyo mkienda 'mtoni' hamkamatwi? Hizi ni mali za Tanzania. Tutibu tatizo tulipe madeni, Serikali ndiyo mwanahisa Mkuu wa Shirika, weka mtaji maisha yaendelee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna viwanja 15 vya ndege nchi hii, katika viwanja 15 viwanja Vinne ndiyo vinaweza kufanya kazi masaa 24 *my friend!*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo tunapozungumza haya …

**MWENYEKITI:** Taarifa Mheshimiwa Waziri wa Fedha

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe taarifa mchangiaji kwamba utaratibu unaotumika wa Wakala, Serikali pamoja na Shirika hauhusiani na masuala ya madeni. Serikali ilishalipa madeni, ndege zetu hazina *risk* ya kukamatwa popote duniani, haya mambo yanayohusiana na madeni madeni yote yalishalipwa. Hakuna sehemu ndege ya Tanzania itaenda ikamatwe kwa ajili ya madeni na zitakuja na ndege za mizigo zitafanya safari zote za mizigo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi kama kuna eneo lolote, ndege ya Tanzania haijaenda zitakuwa ni *logistics* tu za mambo ya kufungua anga kutokana na mambo ya *COVID-19* yaliyokuwa yanatokea, lakini siyo kwa masuala ya madeni, madeni yote yalishalipwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna deni lolote ambalo linaiweka nchi yetu kwenye *risk* ya kukamatiwa mali yeyote ya Tanzania, na taarifa zingine hizo zitakuwa taarifa ambazo zinaendelea kukamilisha taratibu tu ambazo ni za masuala ya kianga na maeneo tofauti baada ya *pandemic* ya *covid.*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mdee unapokea taarifa.

**MHE. HALIMA J. MDEE**: Mheshimiwa Mwenyekiti, nina taarifa hapa ya shirika lenyewe kwa Kamati ya *PAC* inasema hivi ukurasa wa 10, naweza nikakupatia Mheshimiwa Waziri, inawezekana ulitoa hela zikaishia katikati. Inasema madeni ya *ATCL* na Serikali yanaathiri biashara na utendaji wa *ATCL* kwa kushindwa kutekeleza mipango ya kibiashara na kuhofia kukamatwa kwa ndege. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano safari zilizoanzishwa za *Johannesburg* zilisitishwa wakati mipango ya kuanzisha safari za kimkakati za

kibiashara za Nigeria, London na maeneo mengine. Hii ni nyaraka inaonesha ukurasa wa Kumi nitakupatia hii nyaraka.

**MHE. SIMON S. LUSENGEKILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa wapi?

**MHE. SIMON S. LUSENGEKILE:** Nipo hapa.

**T A A R I F A**

**MHE. SIMON S. LUSENGEKILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimtaarifu mchangiaji ya kwamba taarifa anayoisema ni ya hesabu za fedha za mwaka 2019/2020, na tayari Kamati ya *PAC* mimi nikiwa mjumbe wa Kamati ya *PAC* deni la awali lilishalipwa Shilingi Bilioni 120 ambazo ziliripotiwa katika mwaka wa fedha husika.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Halima Mdee unaipokea hiyo taarifa?

**MHE. HALIMA J. MDEE**: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa niliyonayo mimi ni ya tarehe 31 Januari, 2022 juzi na imesainiwa na Afisa Mtendaji Mkuu Mhandisi Ladislaus Matindi. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunasema haya unajua mimi nashindwa kuelewa tunapozungumza haya mambo hakuna anayemvizia mwenzie hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa natamani huo uchungu ambao wote tunao huo wa kupanda kwa mafuta na natarajia kipindi cha bajeti ya Nishati hapa ama kipindi cha Bajeti Kuu hapa, kama mzizi wa fitina wa mafuta, kama mzizi wa fitina wa vyakula kupanda bei, haujatafutiwa ufumbuzi pachimbike na ndiyo nitajua kweli sisi ni Wawakilishi wa wananchi *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiroho safi Tanzania ni yetu, siyo kwa ubaya! kwa hiyo ninaposema wakati wa taarifa ya Waziri Mkuu inaonesha tuna miruko ya ndani, katika viwanja 15 vya ndani, vinavyoweza kuruka masaa 24 basi hata tutendee haki ndege zetu ni viwanja Vinne *my friend*! Nilidhani Waziri wa Fedha ataniambia, Halima wakati tunaanza kupata kwenda huko mbele tutahakikisha viwanja vyote 15 vya ndani vinafanya kazi masaa 24 *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Sasa namuita Mheshimiwa Salim Mussa Omar, Mheshimiwa Rashid Abdalla na wakati huo Mheshimiwa Shamsia Mtamba anajiandaa.

**MHE. SALIM MUSSA OMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza kabisa napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu muumba mbingu na ardhi na vilivyomo kwa kutujaalia tumefika hapa tukiwa hai na wazima. Pili, ninakushukuru wewe kwa kunipa nafasi ya kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee leo nitajikita katika suala zima la maafa katika ukurasa 69 na ukurasa wa 70 wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka juzi mwaka 2019 nilipata fursa ya kwenda kutembelea *museum* tatu nchini Marekani, ikiwemo ya *Titanic Museum* iliyoko pale Branson, pamoja na *World Trade Centre* iliyoko pale New York pia JF Kennedy iliyoko Texas.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matukio haya yalinipa msisimuo wenye mfanano sawa na baadhi ya matukio yaliyotokea ndani ya nchi yangu ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikianza na janga la *Titanic* lilotokea na kupelekea kufariki kwa watu takribani 1,500. Tukio hili linafanana na ajali ya boti yetu ya *MV Spice* iliyotokea Zanzibar na kuondoka kwa Wazanzibari wasiopungua 1,370. Hali kadhalika tukio hili la *Titanic* linafanana sana na ajali iliyotokea ya MV Bukoba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu kama Mbunge, napenda kuishauri Ofisi ya Waziri Mkuu ni wakati sasa wakutengeneza *museum* za *digital* ambazo zitapelekea kizazi kijacho kuweza kuwa na kumbukizi na Taifa kuweza kujipatia kipato katika *museum* kama hizi, haswa nilipoona kwamba kiingilio katika *museum* ile ya *Titanic* ilikuwa ni takribani Shilingi Laki Moja sawa na Dola ya Kimarekani 49.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaamini kama tutakwenda katika muundo kama huu yanapotokea maafa makubwa kama haya na kuweza kuyawekea *museum* maalum, tunaweza hata kukusanya kipato ambacho kinaweza kikasaidia hata angalau kuwasomesha wahanga wale ambao wazee wao waliathirika kwa kiasi kikubwa, katika Taifa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiachana na majanga kama haya pia yaliyojitokeza nilijionea pia mfanano mkubwa sana niliyoiona katika *museum* ya JF Kennedy na tukio lilotokea pale Zanzibar tarehe 7 Aprili, 1972 la kupigwa risasi hadharani Rais wetu wa kwanza wa Zanzibar Hayati Mzee Karume.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili jambo bado halijatengenezewa *museum* hasa yakuweza kutueleza ilikuwaje na unaweza ukakuta hata mwanafunzi wa Chuo Kikuu sasa hivi asiwe na picha halisi ya kukueleza namna gani lile tukio lilitokea siku ile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ipo haja sasa Mheshimiwa Waziri Mkuu ofisi yako iweze kutengeneza *museum* mahsusi ya kuweza ku-*display* hasa historia muhimu kama hizi. Ukienda Zanzibar leo pale ofisi kuu utamkuta Mzee Baraka Shamte atakuelezea ilikuwaje lakini Mzee Baraka Shamte hataishi milele, tutengeneze *digital museum* ambayo itaweza *ku-display* matukio muhimu ya kihistoria kama haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo hata ile *museum* yetu iko pale kwa Mwalimu Nyerere Butiama pia tuangalie namna gani ya kuweza kuitengeneza iwe katika hali ya kidigitali zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema mchango wangu uende katika masuala hayo ya maafa ili tuweze kuwa na rekodi ambazo zitakuwa kumbukizi ya muda mrefu ili na watoto wetu, wajukuu zetu waweze kuja kujionea hasa nini nchi imepitia, athari zilizojitokeza zilisababishwa na nini ili kuweza *ku-overcome* hizo *situation* zisiweze kujirudia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Salim Mussa Omar, sasa namuita Mheshimiwa Rashid Abdalla aweze kuchangia.

**MHE. RASHID ABDALLA RASHID:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia uzima na pumzi ya kuweza kunifanya leo kuchangia hotuba hii ya Waziri Mkuu, kipekee nimpongeze Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mama Samia Suluhu Hassan pamoja na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Hussein Ali Mwinyi, kwa kazi nzuri anayowafanyia wananchi wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu wa kwanza naomba nijielekeze kwenye fedha hizi za *UVICO-19* ambako Zanzibar nayo ilipata mgao wake na kwa Jimbo langu nami nimnufaika mkubwa katika fedha hizi ambapo zaidi ya madarasa 40 nimepata yenye thamani Shilingi Bilioni Tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha hizi zimefanya kazi vizuri kwa sababu katika *Ward* yangu ya Muhambe kuna shule ambayo kwa Zanzibar ni ya kipekee ambayo ilikuwa inaenda mikondo mitatu, sasa fedha hizi zimesaidia kuondoa mikondo ile mitatu kwa kupata madarasa 29 ya ghorofa ambapo itasaidia sana wananchi wa Jimbo langu watoto wetu kusoma vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni mwendelezo wa majengo ambayo tulishayaanzisha wenyewe kwa nguvu zetu wenyewe, fedha hizi zimeingia na majengo sasa hivi Wakandarasi wako kazini kazi inaendelea vizuri, kwa hili lazima tuipongeze Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa

kupeleka mgao kule Zanzibar na Zanzibar nao ikafanya mgao ule na wengine tukanufaika katika fedha zile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu wa pili uende kwenye *TASAF*. *TASAF* vilevile kwenye jimbo langu ni mnufaika mkubwa, nimepata kituo cha afya chenye thamani ya Shilingi ya Milioni 400 kazi inaendelea, kituo hiki kitanufaisha Majimbo mengine mawili ya Chambani na Mtambile kwani ni kituo kikubwa ambacho kitaweza kusaidia kupunguza gharama za wananchi kutoka katika vituo vyetu vidogo kutumia masafa na gharama kwenda katika hospitali kubwa ya Mkoa ya Abdallah Mzee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kituo hiki ninachoomba ni Serikali iongeze tena fedha kwa ajili ya kupata *x-ray* pamoja na *theater* ambapo nimshukuru Waziri Mkuu mwenyewe mbali na kuahidi katika hotuba yake lakini kituo hiki yeye ndie ambaye aliweka jiwe la msingi na akaona kazi inavyoendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanakamati wa kituo hiki kama tunavyojua kwamba fedha hizi kuna asilimia 20 ni nguvu za wananchi, wananchi kupitia kamati ambayo wameiteua wanafanya kazi kubwa, waliacha kuvuna karafuu, waliacha kulima msimu wa kilimo wakasimamia kituo hichi na kituo sasa kiko katika hatua ya rangi. Kwa hiyo, lazima tuipongeze Serikali kwa kazi kubwa ambayo wanaifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu bado naendelea kuomba Serikali kutuingizia tena fedha ili tukamilishe *X-Ray, theater* pamoja na uzio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho ni suala zima la vijana katika uhifadhi wa mazingira. Katika Jimbo langu kuna vikundi zaidi ya 35 ambavyo vimeshajisajili na vinafanya kazi kubwa ya kutunza mazingira katika maeneo yao. Ninaomba kwamba vijana hawa au vikundi hivi viwezeshwe kwanza kwa kupatiwa mafunzo lakini na fedha kwa ajili ya kufanya kazi zao za upandaji wa mikoko na utunzaji wa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maneno yangu hayo na maombi yangu hayo na kwa ajili ya kutunza muda, naunga mkono hoja hii ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Rashid Abdalla. Sasa ninamuita Mheshimiwa Shamsia Azizi Mtamba wakati huo wafuatao wanajiandaa. Mheshimiwa Eng. Ezra Chiwelesa, Cecil David Mwambe na Mheshimiwa Subira Mgalu.

**MHE. SHAMSIA A. MTAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi ili nami niweze kuchangia katika hotuba hii ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya nzuri na leo hii nikaweza kusimama katika Bunge hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilizungumza bajeti ya mwaka jana kuwa changamoto kubwa ambayo inatukabili hasa katika Jimbo langu kwenye masuala ya barabara ni barabara ya ulinzi ambayo imepita Kilambo – *border* kuelekea Kitaya mpaka Tandahimba. Barabara hii ni barabara muhimu mno hasa kwa usalama wa watu wetu pamoja na vyombo vyetu vya ulinzi. Hivyo, nilikuwa naiomba sana Serikali iingalie barabara hii kwa umuhimu wake na tunatambua hali ambayo inaendelea katika mipaka yetu kule, niiombe sana Serikali iweze kujenga barabara hii muhimu kwa kiwango cha lami ili vyombo vyetu vya ulinzi vinapofanya doria katika maeneo yale basi viweze kufika kiurahisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tuna barabara ya uchumi ambayo inatoka Mtwara Mjini kuelekea Msimbati ambapo kuna mitambo na visima vya gesi, barabara hii nayo imesahaulika. Barabara hii ni mbovu sehemu ambapo tuna mitambo ya gesi kule barabara ni mbovu na haipitiki kabisa hasa kipindi cha masika. Hivyo, ninaiomba sana Serikali iangalie barabara hii ya uchumi ijengwa kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miongoni mwa changamoto kubwa ambazo zinatukabili wananchi wa Mkoa wa Mtwara ni suala la maji, suala hili la maji bado limekuwa sugu sana katika Mkoa wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna chanzo kikubwa cha maji chanzo cha Mto Ruvuma, niiombe sana Serikali itumie chanzo hiki cha maji cha Mto Ruvuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2015 uthamini ulishafanyika kwa wananchi, wananchi wangu wa Mtwara Vijij,ini hawaelewi wamenituma niwaulize chanzo hiki cha maji mtatumia lini na lini mradi huu utaanza? Maana wananchi wanashindwa kuendeleza maeneo yao kutokana na kutokulipa fidia mpaka leo.

Mheshimiwa Waziri wa Maji ninakuomba utakapokuja mbele kwenye majumuisho utueleze mradi huu ni lini utaanza na lini wananchi hawa watalipwa fidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee suala la bandari. Bandari ya Mtwara ipo Tanzania wala haipo nchi jirani, lakini kwa masikitiko makubwa sana bandari hii imesahaulika bandari hii imesahaulika. Serikali imewekeza fedha nyingi sana katika bandari hii ya Mtwara lakini imesahaulika na haifanyi kazi ipasavyo. Hivyo, ninaiomba sana Serikali katika msimu wa mwaka huu tunataka kuona bandari ya Mtwara inafanya kazi ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunataka kuona korosho yote ya msimu ya mwaka huu inatumia bandari yetu ya Mtwara. Pia tunayo kila sababu ya kuitumia bandari hii kwa sababu tuna mizigo, mizigo ambayo itatoka Malawi inaweza kupitia bandari hii ya Mtwara, pia tuna *cement* ya Dangote inaweza kutumia bandari hii ya Mtwara. Leo hii barabara ya Lindi – Dar es Salaam ni mbovu kila siku inafanyiwa matengenezo kutokana na uharibifu wa malori ambayo inaharibu barabara hii. Serikali kama mngekuwa mnatumia bandari ya Mtwara leo hii barabara yetu isingekuwa inatengenezwa mara kwa mara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bila kupepesa maneno nimshukuru sana Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kwa kutuletea viuatilifu kwa wakati kwa wakulima wetu wa korosho. Nimpongeze pia Mheshimiwa Waziri naye sitamtendea haki kwa kulisimamia suala hili mpaka leo hii kutuletea viuatilifu vya korosho kwa wakati kwa wakulima wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri kitu kimoja tupange utaratibu wa kugawa viuatilifu hivi ili kuondoa mkanganyiko ambao ulijitokeza kwenye msimu uliopota. Ninaiomba Serikali ni lazima kuwe na takwimu katika ugawaji wa viuatilifu hivi na takwimu maalum za kila mkulima ili wakulima wote waweze kupata viuatilifu hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya nikushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Shamsia Mtamba kwa mchango wako. Namuita Mheshimiwa *Engineer* Ezra Chiwelesa kama nilivyosema Mheshimiwa Mwambe na Mheshimiwa Mgalu wajiandae.

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi pia na mimi niweze kuchangia kwenye hotuba hii ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nami niungane na wenzangu waliotangulia kumshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa miradi mikubwa ambayo inaendelea kwenye Majimbo yetu, miradi ya barabara inaendelea vizuri, miradi ya maji na ujenzi wa vyumba vya madarasa ambao umepita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa ziara ambayo aliifanya Mkoa wa Kagera tarehe 29 mwezi uliopita, ziara ambayo imetoa ufumbuzi wa kilio cha muda mrefu cha wakulima wa kahawa katika Mkoa wa Kagera, kutuondolea tozo 42 kati ya tozo 47 ambazo zilikuwa zinatunyonya na kututesa sasa tumebaki na tozo tano ambazo zimeleta unafuu wa kuweza kuendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya nitaongelea sehemu kama tatu. Sehemu ya kwanza ni mfumuko wa bei, sehemu ya pili itakuwa ni *issue* ya ajira na kama nitapata muda kidogo nitaongelea habari ya *TARURA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukirudi kwenye habari ya mfumuko wa bei nimekuwa najiuliza kitu kikubwa kimoja ambacho nimekuwa nacho. Kwanza tunamshukuru Mwenyezi Mungu kwamba hili Taifa wakati wa janga la Corona limeipiga dunia Taifa hili tulisimama na Mungu kama tulivyosema na mambo yetu yalienda vizuri hatukuwa na *lockdown,* hatukuwa na nini na kila kitu kiliendelea kwenda sawa, hatukuona changamoto yoyote ile katika shughuli zetu za kiuchumi, lakini sasa baada ya hili janga kuwa limetukumba wenzetu walipokuwa wamejifungia baada ya kurejea kwenye shughuli za kawaida kunakuwa na uhaba sasa, *supply and demand* inaongezeka kwamba vitu vingi vinahitajika kwa wakati mmoja kwa wakati huo huo kwa hiyo, wafanyabiashara wanachukua *advantage* ya kupandisha baadhi ya bei ili waweze kujinufaisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii haianzii hapa tu inaanzia duniani huko imeshuka mpaka sasa imekuja imetukumbuka. Kitu kimoja ambacho nimekuwa najiuliza, kwa hali ya nchi sasa leo hapa tunaposimama huko nje ni mbaya sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge wengine wameshatangulia kusema hali ya wananchi ni mbaya mno, vitu vimepanda bei sana kupita kiasi. *Statement* ya nyanya kupanda bei, vitunguu kupanda bei, tukaanza kusema ni vita ya Ukraine mimi hiki kitu sikubaliani nacho! Nadhani tunakosa *control* kwenye nchi, kama Taifa ni lazima ifikie *stage* tujue jinsi ya kufanya *control* ya bei kwenye nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuwezi kuwa na Taifa ambalo watu wanajiamulia kupanga bei wanavyojua wao kwa kisingizio cha vitu vingine hakuna mtu anayeenda kuuliza, halafu tunakuja kuishauri Serikali kwamba tutafute hela ya kukopa na ku-*inject* kule, uta-*inject* mara ngapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona kwenye pesa ya *UVIKO,* Mama ameleta hapa 1.3 trilioni lakini matokeo yake mabati yalipanda bei, *cement* ilipanda bei, vitu vingi vilipanda bei, lakini baada ya vitu vile kupanda bei hakuna mtu ambaye amerudi nyuma akawaambia wale watu washushe bei.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Biharamulo bati linaenda Shilingi 38,000 la *gauge* 28, limeshafikia Shilingi 38,000 lakini kabla ya ujenzi ule mabati yalikuwa yapo chini ya Shilingi 35,000. Sasa unaweza ukaona kwamba tabia ya wafanyabiashara wa nchi hii kila wanapopata fursa ya kupandisha bei hata yale mambo yakimalizika bei huwa hazirudi nyuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, jambo la kwanza lazima kama Taifa tusimame tujue jinsi ya kujikwamua kutoka hapa, tusikubali ongezeko la bei kwenye kitu chochote kile, hiyo ndiyo itakayoweza kusaidia wananchi, kwa sababu tutakapokuja na wazo la kukopa na ku-*inject* pesa mzunguko unakopa anaelipa ni nani? Ni Watanzania walewale hakuna unafuu ambao unao wasababishia, kwa sababu watalipa kwenye kodi hakuna mfanyakazi ameongezewa mshahara, tunajua tarehe 01 Mwezi wa Tano kilio cha wafanyakazi Mama anatakiwa ajibu, sasa Mama atajibu mambo mangapi? Anatakiwa aongeze mshahara huku tukiwa tunalia na vitu vingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *idea* ambayo mimi ninayo, maoni yangu mimi ni lazima…

**MHE. ISSA J. MTEMVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa kutoka wapi, aah! Mheshimiwa Mtemvu.

**T A A R I F A**

**MHE. ISSA J. MTEMVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampa taarifa mzungumzaji kwamba asishangae bidhaa nyingine kupanda bei ilihali ni eneo moja tu analoliona yeye malighafi ya mafuta kupanda bei. Malighafi ya mafuta inasababisha *multiplayer effect* katika maeneo yote. Hoja kubwa hapo ni kuendelea kumuomba sana Waziri Mkuu anayeisimamia Serikali kuendelea kusimamia matumizi ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi sasa wanalia huko barabarani wanalia kwenye vyombo vya mitandao kwamba matumizi ni makubwa sana yanayoendelea kwa Viongozi wetu wa Serikali.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Chiwelesa Injinia unapokea taarifa.

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa naipokea na huko ndiko nilikokuwa naelekea kwenye *solution*, kwa sababu kazi yangu ni kuongea tatizo halafu baadae tuende kwenye kutafuta ufumbuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *idea* ambayo ninayo ni moja, hii ni ripoti ya *BOT* kwenye *issue* ya *Treasury Bond,* tulipokuwa tunapewa ripoti hapa kipindi kilichopita tulipewa ripoti, tulikuwa tunaanza kuuza *bond* mwezi huu nadhani kesho zilikuwa zinauzwa. Kesho tulikuwa tunauza *bond* ya *20 years* kwa asilimia 15.4, *BOT* wameshusha leo ipo asilimia 12.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 27 tulikuwa tunauza *bond* ya *seven years* kwa asilimia 9.48 leo wameshusha imeenda asilimia 10 na nyingine asilimia 10 leo wameshusha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kimoja ambacho ninacho, unilindie muda wangu. Kitu kimoja ambacho ninacho ni kwamba ni lazima sasa kama Serikali imejitafakari upande wa *BOT* tumeanza kushusha hizi hisa na *interest* ambazo zipo ni lazima turudi nyuma tukae na mabenki, unajua unapotaka wafanyabiashara washushe bei, mfanyabiashara yupo tayari ku-*adjust* kwenye faida yake, lakini wafanyabiashara wengi wamechukua *working capital* kutoka kwenye mabenki na wakati wote wa *CORONA* mabenki yaliendelea kutoza *interest* ileile na wafanyabiashara wameendelea kufanya biashara katika *interest* zilezile zinatoka kwenye mabenki.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Msongozi, taarifa.

**T A A R I F A**

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. ninampa taarifa mchangiaji anayechangia sasa, kwenye suala ambalo analifanya la kuishauri Serikali juu ya masuala ya uchumi. Mheshimiwa Mbunge anachokiongea ni sahihi kabisa na hata Bunge lililopita tumemsikia Mheshimiwa Mbunge akitekeleza majukumu yake alipokuwa anashauri namna ambavyo wenzetu wa Egypt wanachimba chima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Endelea Mheshimiwa Ezra.

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilindie muda wangu. Nilichokuwa nasema ni kwamba, hatuwezi kuwa na Taifa ambalo kila mmoja anajipangia vitu anavyovitaka. Tukumbuke tumetoka katika athari ya uchumi sasa wakati ule wa *lockdown*, vitu vingi sana vilisimama lakini katika Taifa letu mambo yalienda vizuri. Kwa hiyo ushauri wangu kwa upande wa Serikali, Serikali irudi nyuma, kwanza iongee na *Commercial Banks* zishushe riba kwa ajili ya wafanyabiashara ambao wamekopa mikopo ya kibiashara. Benki zikishashusha riba turudi sasa kwa wafanyabiasha tukawaambie kwamba, kwa sababu Serikali imewa-*favor* kwenye upande wa biashara iweze kushusha riba hali kadhalika wafanyabishara watengeneze faida ndogo lakini ile faida ndogo iweze kushusha bei ya bidhaa vinginevyo hali itakuwa mbaya na uchumi wetu unaenda kuathirika kwa sehemu kubwa.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, kengele yako ya pili imepigwa Mheshimiwa Ezra.

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nina dakika 10 hapa nilizihesabu sidhani kama zimetimia au umenichanganya na wa dakika tano?

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Injinia Ezra Chiwelesa kwa mchango wako mzuri. Mheshimiwa Cecil David Mwambe.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana na mimi kwa kunipa nafasi ya kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze moja kwa moja kwa kuipongeza sana hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ambayo imejikita kwenye kuona namna ya kutatua na kusuluhisha matatizo yanayowakabili watanzania, ninaamini tukietekeza hii kama ilivyo tutafanikiwa kwa kiasi kikubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza sana Mheshimiwa Rais pia kwa namna ambavyo tumepata miradi mingi kwenye maeneo mbalimbali kwenye Majimbo yetu. Jimbo la Ndanda sasa limechangamka zaidi ukilinganisha na miaka mitano iliyopita wakati ule hatuna Ilani ambayo tulikuwa tunaisimamia na sasa tupo tunakwenda mstari imara wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi, wananchi wamechangamka na bado wanaahidi watakichagua tena Chama cha Mapinduzi ili kuweza kujipatia maendeleo wenyewe.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo ambalo ninapenda kulisema pamoja na pongezi hizo ni kwamba nimpongeze pia Mheshimiwa Waziri wetu wa Kilimo kwa namna ambavyo juzi tu hapa tulikuwa na kikao kwa ajili ya wadau wa korosho kuangalia na kufanya tathmini ya msimu uliopita. Kuna baadhi ya mambo tumeyajadili, kwanza kabisa nimpongeze kwa kuhakikisha *export levy* kile kiasi cha pesa ambacho kilitengwa kwa ajili ya kusaidia wananchi hasa zaidi kwenye masuala ya pembejeo kimerudi tena na Serikali imeridhia kwamba pesa hiyo itatoa ili kupunguza nakisi ya bei ya pembejeo ili kuwasababishia wakulima waweze kuzalisha kwa gharama nafuu zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo nimuombe sasa Waziri wa Fedha ahakikishe jambo hili analileta kwenye *Finance Bill*, lisiwe tu kwamba ni matakwa ya Waziri walikutana huko wakaonana lakini liwe kisheria kabisa ili kila mwaka sasa hiyo pesa iwe inarudishwa isiwe maamuzi ya kipindi kimoja kimoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ninaomba pia Mheshimiwa Waziri wa Kilimo yeye mwenyewe alete sheria itakayokuwa inasimamia masuala ya kilimo. Tumesikia hapa juzi wakati wa uzinduzi, wakati wa ugawaji wa pikipiki zile kwa ajili ya wenzetu Maafisa Ugani ameongea mambo mengi sana mazuri kwa ajili ya kuboresha kilimo, hata hivyo mambo haya hayapo kwenye sheria, afanye namna nzuri aweze kuleta sheria hapa tumsaidie kuipitisha ili iweze kuwa kama dira ya shughuli anazotaka kuzifanya kwenye Wizara ya Kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa wa Waziri ya Kilimo, naweza nikakukumbusha mambo machache ambayo tuliyaongea wakati wa kikao chetu cha wadau wa korosho, na nafanya hivyo makusudi ili iingie kwenye *Hansard* uone na wewe namna ya kuyashughulikia.

Kwanza kabisa tulikushauri kwamba kuna mambo mawili, sasa hivi tunayo Bodi ya Korosho mpya na tunaona inafanya kazi yake vizuri kabisa chini ya Mwenyekiti wetu Mzee wetu Mzee Mwanjile wanafanya kazi nzuri sana, lakini tulikushauri na mimi nilitoa ushauri nikakuambia kwamba tunae Mkurugenzi wa Bodi ya Korosho ambaye ameshakaa pale ndani zaidi ya miaka mitatu akiwa anakaimu, tukakuomba kama inawezekana fanya mambo mawili ili aweze kufanya kazi zake kwa uhakika, ama umthibitishe kwa sababu amekuwepo Bodi ya Korosho muda mrefu au umuondoe ulete mtu mpya ambaye anaweza akafanya kazi vizuri zaidi ya huyu aliyepo kwa sababu kwa kipindi kirefu hamjamhibitisha, sasa hatuelewi tatizo ni nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo jingine ni kwamba kumekuwa na migogoro mingi ndani ya Bodi ya Korosho na wewe kama Waziri nafahamu labda mingine imekufikia, migogoro ya watumishi, migogoro ya wanunuzi kwa mfano kuna Kampuni moja inaitwa *TF Commodities* wanadai *Bond* yao ya Milioni 50 zaidi ya miaka mitatu sana. Tunaomba kwa sababu wale watu wanachajiwa *interest* kwenye mabenki au warudishiwe au wakatwe hicho kiasi ambacho kinachotakiwa kukatwa *balance* yake apewe ili aweze kuendesha maisha yake na hii itawapa *comfort* wanunuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuliongea pia suala la usambazaji wa viuatilifu, tunakupongeza sana kwa sababu kiasi fulani kimeshafika kwenye maeneo yanayotakiwa yasambazwe. Hata hivyo tunakuomba kwamba kuna migogoro mingi ya upatikanaji wa *tender* hizi ambazo zinasimamiwa na bodi ndogo ambayo inaitwa Bodi ya Pembejeo lakini na yenyewe haipo kisheria, kazi wanazozifanya haziwapi amani sana watu wengi wanaosambaza pembejeo kwa sababu imekuwa na aina fulani ya upendeleo, badala ya kuangalia *performance* wameangalia kama mambo ya kujuanana nayo tunaomba uichunge uone namna ya kusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naomba sasa nijikite kwenye mchango wangu rasmi. Nianze kwa kusema kama Wabunge wote tunakubaliana kabisa kimsingi kwamba kuna *inflation,* kuna ongezeko kubwa sana la bei ya bidhaa mbalimbali. Jana tulimuona Mheshimiwa Waziri wa Fedha akiongea kuhusiana na suala hili la ongezeko la bei, tulimuona pia Waziri wa Viwanda na Biashara nae akiongea kuhusiana na suala la ongezeko la bei. Kwa nafasi zetu kama Wabunge tuna wajibu wa kuishauri Serikali ili iweze kuangalia namna bora tutakavyoweza kupata *solution* ya kuwapunguzia wananchi ukali wa maisha uliopo sasa hivi kutokana na ongezeko kubwa la bei ya bidhaa, kuanzia bidhaa za ujenzi mpaka bidhaa za chakula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana Mheshimiwa Waziri wa Fedha wakati anaongea alisema kwamba anataka kuona namna bora ili kuweza kupunguza bei ya kodi ya sukari. Ameangalia tu *element* moja ya sukari, lakini nazani suluhisho lingekuwa kuangalia zile tozo mbalimbali zilizoko kwenye mafuta ya magari na kuzipunguza, kwa sababu zaidi ya asilimia 50 ya bei ya mafuta sehemu kubwa ni tozo za Serikali. Kwa hiyo wakaziangalie hizi tozo ili waweze namna ya kuzipunguza.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala jingine ambalo tulikuwa tunaliongea kila mara kupitia Waziri wetu wa Viwanda na Bishara lakini Waziri wa Fedha nawe ulifahamu. Kulikuwa na kitu kilikuwa kinaitwa *electronic tax stamps (ETS)* na chenyewe kilikuwa kinalalamikiwa muda mrefu sana na wafanyabiashara nadhani Kamati yetu ya Viwanda na Bishara kwenye taarifa yake itakuwepo, lakini pia Kamati ya Bajeti na yenyewe taarifa yake itakuwepo. Oneni namna ya kukaa na wafanyabiashara tupate *solution* ya uhakika kwa sababu ongezeko la shilingi mbili au shilingi tatu kwenye bidhaa yoyote ya kinywaji kwa mfano, soda *Coca-Cola* itakapoongeza shilingi 30 kwa ajili ya kupitisha hiyo stempu wao hawawezi kuongeza shilingi 30 kwenye kinywaji watakwenda kuongeza kati ya shilingi 50 mpaka shilingi 100, kwa hiyo inaongeza gharama kubwa. *(makofi)*

Kwa hiyo, kama tunasema tunataka kuangalia kurekebisha *inflation* tuangalie vile vitu vidogo vidogo vinavyoongeza gharama kubwa za uzalishaji ili kuweza kuwasaidia wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo jingine kwenye suala la Wizara ya Nishati. Wizara ya Nishati ina mpango wake wa *REA* ambao kwa Mkoa wa Mtwara sasa hivi kidogo imesuasua na hatufahamu sababu ya msingi ni nini, tutaomba atakapokuja hapa Waziri basi atueleze. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nililotaka kusema kubwa ni kwamba Mkoa wa Mtwara na Mkoa wa Lindi ndiko inapozalishwa gesi. Tunashangaa sana watu tunaotokea maeneo haya, gesi ni uchumi wa Kusini kama ambavyo ilikuwa miaka ya huko nyuma na maeneo mengine, lakini kwa kiasi kikubwa mikutano yote inayohusiana na kutaka kufanya mikataba ya *LNG*, mikataba ya gesi inakwenda kufanyikia eneo la mbali kabisa na maeneo haya. Sasa watu tunaotokea maeneo haya tunanufaika na nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatakiwa tuanze kuona tunanufaika tokea mapema. Mikutano inayuhusiana na masuala ya gesi ya *LNG* pamoja na haya mazao kwa mfano korosho na mengine ifanyike eneo la Mtwara na Lindi ili wafanyabiashara wa kwetu wa maeneo haya waweze kunufaika na mikutano hii. Kwa sababu watu watanunua chakula kwa Mama Lishe, watu watakwenda kulala kwenye *lodge* hizi zilizopo kwenye maeneo haya ili waanze kuona wananufaika mapema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa nafasi uliyonipatia, ahsante kwa muda huu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Cecil David Mwambe kwa mchango wako. Nilitamka mapema sasa namuita Mheshimiwa Subira Mgalu wakati huo Mheshimiwa Kwagilwa Reuben, Mheshimiwa Benaya Kapinga na Mheshimiwa Ritta Kabati wanajiandae.

**MHE. SUBIRA K. MGALU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi kuchangia katika Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Awali nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kazi nzuri anayoifanya ya kumsaidia Mheshimiwa Rais, nampongeza pia Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri inayoendelea kufanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mjadala mkubwa kuhusu kupanda kwa bei za bidhaa mbalimbali ambao pia Mheshimiwa Waziri Mkuu amejielekeza kwenye ukurasa wa 16. Ningependa kwanza niwapongeze Waheshimiwa Mawaziri, Waziri wa Fedha na Waziri wa Viwanda na Biashara na Uwekezaji kwa taarifa waliyotoa jana, ufafanuzi mzuri na nishauri taarifa ile tungepewa Wabunge wote lakini pia ingewasilishwa kwenye mamlaka mbalimbali za Kiserikali. Kwa sababu imeanisha hatua mbalimbali za muda mfupi, muda mrefu na muda wa kati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na matumaini ambayo Mheshimiwa Waziri wa Fedha ametupa namna gani ya kulekea bajeti ya 2022/2023 Serikali itafanya nini katika kushusha bei za bidhaa mbalimbali. Kwenye bidhaa ya mafuta ninaomba nitoe ushauri kwa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuliona jitihada za Mheshimiwa Rais Mwezi wa Oktoba, tarehe 05 alifuta zile tozo za taasisi na kiasi cha Shilingi Bilioni 102 ziliondolewa lakini unafuu haukupatikana. Kwa hiyo, ninaishauri Serikali kwa mwenendo waliyoonesha kwenye bei hii ya mafuta kabla ya UVIKO, wakati wa UVIKO na baada ya vita hii inaonesha bei inaendelea kuongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali itakapokuja kwenye Bajeti Kuu iangalie utaratibu wa kutoa *subsidy* kwenye bidhaa hii ya mafuta, kama zilivyofanya nchi za jirani Afrika Mashariki. Ifanye tathmini na tafiti, tambua hatulingani kwa hali zetu za kiuchumi lakini pengine inaweza ikaendelea kusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo pamoja na hatua zingine ambazo zitachukuliwa, ninakuomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha maoni mbalimbali ya wadau wa sekta binafsi uyatilie maanani ili kusaidia kupungua kwa bei hizi kwa sababu kweli hali ni tete katika maeneo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu wa pili pia utajielekeza, jana kuna maoni yalitolewa hapa kwamba Taifa letu hili halina maono na Marais wetu kila mmoja akiingia anafanya kwa kadri anavyoona yeye inafaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nijielekeze kwamba Taifa letu hili maono yake yanatokana na Dira ya Maendeleo ya Taifa ya Mwaka 2025 na dira hii iliandaliwa mwaka 2000 na utekelezaji wa Dira hii wa Maendeleo ya Taifa ulipangiwa mkakati wa miaka 15, kila baada ya miaka mitano unaandaliwa mpango wa Maendeleo ya Kitaifa ambapo kwa Ilani zetu za Chama cha Mapinduzi, chama ambacho kiko madarakani inatohoa Ilani zake kupitia mipango mbalimbali kwa mujibu wa Dira ya Maendeleo ya Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na hali hiyo moja ya kipaumbele kwenye Dira ya Maendeleo ya Taifa ilikuwa ni kuwepo kwa jamii inayoelimika. Kwa hiyo nataka nitoe mfano hapa, kwa kipindi cha Rais Marehemu Benjamin Mkapa aliboresha elimu, kwa elimu ya msingi na sekondari kupitia *MEM* na *MES*. Kipindi cha Rais wa Awamu ya Nne ujenzi wa shule za sekondari kila Kata ni maono, kipindi cha Rais wa Awamu ya Tano kutoa elimu bure ni maono, kipindi cha Rais wa Awamu ya Sita kuwezesha kupatikana kwa madarasa zaidi ya 15,000 na miundombinu mbalimbali, ujenzi wa Maabara nayo ni maono ambayo yameanza kutolewa kwenye Dira ya Maendeleo ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kana kwamba haitoshi ujenzi wa *SGR* wazo au mikakati ilianza tangu Awamu ya Tatu, Awamu ya Nne, Awamu ya Tano utekelezaji wake ulianza na Awamu ya Sita hii Mheshimiwa Rais Mama Samia Suluhu Hassan anaendelea kutekeleza nayo ni maono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama haitoshi ujenzi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere, wazo lilianza tangu wakati wa Mwalimu Nyerere, hata Awamu ya Nne pia ilikuja na mkakati ndiyo maana mwaka 2012 Rubada iliingia mkataba na Kampuni ya *ODRICH* ya Brazil, hatimae Awamu ya Tano chini ya Uongozi wa Hayati Daktari John Pombe Magufuli mradi huu ulitekelezwa na sasa hizi chini ya Uongozi wa Rais Samia mradi huu unaendelea kutekelezwa vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata ukiangalia ujenzi wa miundombinu mingine, kwa mfano mwendokasi Dar es Salaam ni utekelezaji wa Awamu mbalimbali. Kwa hiyo, kuliaminisha Taifa kwamba hatukuwa na mpango wowote au hatuna maono mimi nadhani siyo sawasawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umefika wakati pengine kama Taifa kutazama sasa kama ushauri ulivyotolewa maono ya baada ya miaka 50 na miaka 100. Tunavyolinganisha lazima tuangalie uchumi wa nchi zetu na tuwatie moyo Viongozi wetu walioongoza nchi hii, kwamba kila mmoja ameongoza amefanikisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia kwenye sekta ya afya pia tulikuwa na maono ya ujenzi wa Zahanati kila Kijiji, maono ya ujenzi wa Vituo vya Afya kila Kata. Tumeona utekelezaji wake, tumeona enzi ya Awamu ya Nne uboreshaji wa Hospitali ya Muhimbili, ujenzi wa Hospitali ya Mloganzira, uanzishaji wa Kitengo cha Moyo, Awamu ya Tano imejenga zaidi ya vituo vya Afya 300, ujenzi wa Hospitali mpya za Wilaya, Awamu ya Sita nayo imejenga vituo 233 kwa muda mfupi, imejenga Hospitali za Wilaya 28 mpya, inamalizia Hospitali za Wilaya 66. Kwa hiyo Serikali zote kwa kuwa zimeongozwa na Chama Cha Mapinduzi na Ilani hii ya mwaka 2025 imejielekeza ukurasa wa Nane itazisimamia Serikali zake sasa kuandaa dira nyingine ya Taifa kuelekea 2050. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, naomba ieleweke nchi yetu ina maono, Marais mbalimbali wametekeleza wajibu wao na tunavyoendelea.

Inawezekana sasa kwa mazingira ya dunia inavyokwenda kuja na Dira nyingine ya Taifa kuelekea 2050 au kuelekeza 2100 lakini Awamu zote hizi tumeona. Licha ya changamoto zilizopo zifanyiwe kazi lakini Serikali inapoendelea kutekeleza ilani hii sasa ya 2025 tunaomba ijielekeze kupunguza mfumko wa bei. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaipongeza sana Wizara ya Kilimo naamini nayo itatoa *input* nyingi katika kuwezesha bei ya bidhaa inapungua. Tumeona maono ya Mheshimiwa Rais ya kuanzisha Mfuko wa Mazao pia ahadi ya kutoa *subsidy* kwenye masuala ya mbolea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaishukuru sana Serikali mimi ninatoka Mkoa wa Pwani kwa namna ambavyo tumepata viuatilifu vya zao la korosho. Naomba kuunga mkono hoja, naipongeza Serikali iendelee kutekeleza ilani yetu kama ilivyokuwa katika Serikali zilizopita. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Subira Mgalu kwa mchango wako. Namuita Mheshimiwa Kwagilwa Reuben kama nilivyokuwa nimemtaja hapo awali na wale wengine wajiandae.

**MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa fursa hii ya kunipa kuchangia kwenye ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii nimpongeze sana Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kwa uelekeo huu wa bajeti ambazo tumezijadili kwenye Kamati zetu na sasa tunazijadili kwenye Bunge hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2011 tulitunga Sheria ya Manunuzi ya Umma na baadae tukaifanyia marekebisho mwaka 2013. Sheria hii ya Manunuzi ya Umma ni sheria muhimu sana kwa sababu zaidi ya asilimia 70 ya fedha zote tunazopitisha hapa kwenye bajeti, tunakwenda kuzitumia kupitia Sheria hii ya Manunuzi ya Umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria hii ya Manunuzi ya Umma tunamuomba Mheshimiwa Waziri Mkuu na Serikali walete Muswada tuifanyie marekebisho kwenye kipengele cha ununuzi wa madawa. Sheria hii tulivyoitunga ni *cross-cutting,* kununua mabati tunatumia sheria hii, matofali sheria hii, kununua vifaa vingine ni sheria hii pia. Ni lazima sheria hii tuirekebishe ili kipengele cha ununuzi wa madawa kiwe na *focus* yake, kiwe na umuhimu wake, kiwe na utofauti wake, nitaelezea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria hii kwenye ununuzi wa madawa inatoa mianya mitatu mibaya. Mwanya wa kwanza unaitwa *price rigging* au *price curtailing.* Sheria kwa jinsi ilivyo tunapokwenda kuitekeleza kupitia mtandao wa *TANePS*, hasa ukizingatia kwamba *MSD* inanunua madawa asilimia 90 tunayaagiza kutoka nje. Kwa hiyo, sheria hii inaitaka *MSD* kutangaza *tender* kupitia mfumo wa *TANePS* na hapa hushindanisha wazabuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wazabuni hawa kwa mara nyingi kumekuwa na tabia ya watu kujipanga, wakijipanga anayechukuliwa ni yule mwenye bei ya chini, kiuhalisia ukiangalia bei ya chini, ambayo wao wanaiita *lowest evaluated bid* ukiangalia hii inayoitwa bei ya chini siyo bei ya chini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitatoa mifano *MSD* walipotangaza kununua mashine inayoitwa *Hematology Analyzer* mzabuni *aliye-tender* bei ya chini *ali-tender* kwa Shilingi Milioni 117 wakati bei ya soko halisi ni Shilingi Milioni 20. Nitatoa mfano wa pili, *MSD* walipotangaza *tender* ya mashine inayoitwa *immunology analyzer,* mzabuni *aliye-tender* kwa bei ya chini *ali-tender* kwa Shilingi Milioni 149 ilhali mashine hii bei ya soko inauzwa Shilingi Milioni 37. Nitatoa mfano wa tatu, *MSD* ilipotangaza kununua mashine ya kuchakata maji kwa ajili ya kutumika katika kusafisha damu, mzabuni *aliye-tender* bei ya chini *ali-tender* kwa Shilingi Milioni 129 ilhali bei halisi ya mashine hiyo ni Shilingi Milioni 32. *(Makofi)*

**MHE. TWAHA A. MPEMBENWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa Mheshimiwa Mpembenwe.

**T A A R I F A**

**MHE. TWAHA A. MPEMBENWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe taarifa mzungumzaji kwamba kidonge cha kilo moja cha kuweza kutengeneza dawa ya kutoa madoa yaani ile *JIKI* soko halisia inauzwa kwa Shilingi Milioni Nne lakini *MSD* wamenunua kwa Shilingi Milioni 262 na ushahidi upo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Unapokea taarifa hiyo Mheshimiwa Kwagilwa?

**MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa hii naipokea na ninataka nisisitize kidonge kimoja cha kilo moja cha

kutengeneza *JIKI* bei sokoni ni Shilingi Milioni Nne na *MSD* kidonge hiki wamepelekewa bei ya Milioni 262! *(Makofi)*

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili halikubaliki duniani wala mbinguni. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa subiri kidogo Mheshimiwa Kwagilwa kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Ummy Mwalimu, Waziri wa Afya.

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe taarifa mchangiaji. Ni kweli Sheria ya Manunuzi ya Umma inaweza ikawa na changamoto lakini bado haizuii *MSD* kununua dawa moja kwa moja kutoka kwa wazalishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2016 Rais Magufuli alituelekeza tuachane kununua dawa kutoka kwa madalali, tununue kutoka kwa wazalishaji, mwaka 2017 angalieni vyombo vya habari. Tulifanya *press* tuliweza kushusha bei za dawa kwa zaidi ya asilimia 40, kidonge cha *Amoxicilline* kilichokuwa kinauzwa Shilingi 11,000 tulikinunua kwa Shilingi 4,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mashuka kutoka Shilingi 22,000 tuliyashusha mpaka Shilingi 11,000. Tatizo lililopo *MSD* siyo tu Sheria ya Manunuzi ya Umma, mipango mibaya ya utekelezaji wa manunuzi ya umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *MSD* hiyo hiyo kwa Sheria hii ilianza kufanya vizuri. Kwa hiyo, hiyo ni taarifa nataka kusema sheria ipo lakini tunaweza tukabadilisha sheria, lakini kama hatuna mipango mizuri ya *procurement* ya dawa, vifaa na vifaa tiba tatizo la *MSD* litaweza kuendelea. Mheshimiwa Rais alishatoa maelekezo Wizara tunayafanyia kazi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Waziri kwa taarifa. Mheshimiwa Kwagilwa unapokea taarifa?

**MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaipokea taarifa kwa maana moja nzuri sana kwamba Mheshimiwa Waziri…

**MWENYEKITI:** Haya na ninakuongezea dakika moja na nusu kwa kumalizia hoja yako.

**MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri anakubaliana kwamba lipo tatizo, kama tunataka kumsaidia

Mheshimiwa Rais, ambaye amekwishatoa maelekezo ya kwenda kumulika *MSD* tumsaidieni sisi kwa sababu sehemu yetu ni kutunga sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria hii inayo shida, shida hii inatupeleka hata Bima yetu ya Afya haifanyi kazi. Huwezi kuwa na Bima ya Afya inayohudumia vifaa ambavyo viko *overpriced*. Madawa yapo *overpriced*, vifaa vinavyotumika viko *overpriced*, Bima yako ya Afya itashindwa *ku-cover* haiwezi! Siyo tu hivyo, namuongelea mwananchi wa Kata ya Kwamagome anayeumwa figo akafanye *diagnosis* kwa Shilingi 300,000 haiwezekani! Shilingi 500,000 haiwezekani! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamuongelea mwananchi wa Kata ya Malezi, namuongelea mwananchi wa Kwaluala, mwananchi wa kwa Sindi haiwezekani! *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa!

**MWENYEKITI:** Taarifa kutoka wapi?

**MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri Daktari Godwin Mollel una taarifa?

**T A A R I F A**

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti…

**MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilindie muda wangu umechukuliwa. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri wa Afya ameshalielezea vizuri, jambo lenyewe liko *straight forward* na akasema Rais wetu wa Awamu ya Tano alishaeleza kwamba tuendeni viwandani. Kwa hiyo, anachochangia ni kizuri sana hatuna shida, lakini tukishatoka tukaelekea upande wa viwanda tumekata huo mzizi wa fitina, na vyombo vyetu vingine vikifanya kazi vizuri kuhakikisha wanasimamia hakuna namna yoyote hayo yanayosemwa wakati hii Nchi ina vyombo vyake ninakuhakikishia hakitatokea hicho. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri wa Afya ameshatoa maelekezo na kazi hii inaendelea.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Mollel kwa taarifa yako. Mheshimiwa Kwagilwa unapokea taarifa?

**MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, jitihada zote hizi za Serikali inaonesha kwamba lipo tatizo. Ninachotaka niseme ni nini?

Mimi nitamshangaa sana Mtanzania yeyote ambaye haelewi hiki ninachokisema hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazungumzia kwamba Mheshimiwa Rais amepeleka Shilingi Bilioni 200 *MSD* na bado Watanzania hawana madawa kwenye hospitali! Mheshimiwa Rais amepeleka shilingi bilioni 200 na bado hazitoshi kununua dawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fikiria mazingira ambayo mwongozo uliotolewa na Serikali… *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Kwagilwa kwa mchango wako sasa namuita Mheshimiwa…

**MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Benaya Kapinga wakati huo Mheshimiwa Ritta Kabati na Mheshimiwa Abubakari Asenga wanajiandaa.

**MHE. BENAYA L. KAPINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi hii ya kuchangia Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami niungane na Wabunge wenzangu kutoa pongezi nyingi sana kwa Serikali hii ya Awamu ya Sita kwa namna inavyofanya kazi. Siyo kwa kufanya kazi tu lakini kwa namna inavyosikiliza kero, inavyosikiliza hoja za wananchi kupitia sisi Wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni tu yamefanyika mambo mengi na mabadiliko makubwa na Serikali hii ya Awamu ya Sita ilipokwenda kusikiliza hoja za Waheshimiwa Wabunge naipongeza sana Serikali hii ya Awamu ya Sita. Kipekee nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa namna anavyofanya kazi. Karibuni tu tulikuwa na mgogoro mkubwa kule Ngorongoro, lakini kwa utulivu mkubwa suala hili limeshughulikiwa nampongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo hapo tuwe wakweli, Waheshimiwa Wabunge naomba tuwe wakweli na wa wazi kabisa katika suala hili la mfumuko wa bei.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wamezungumza wenzangu hapa ni kweli kabisa kuna vita ya Ukraine na Urusi ambayo hadi leo ina siku 36, lakini suala hili la mfumuko wa bei halikuanza siku hizo. Amesema hapa Injinia Ezra mwaka jana Disemba, 2021 vitu vilianza kupanda bei, malalamiko yalianzia

kwenye mbolea, yakafika kwenye vifaa hivi vya ujenzi, yamefika mafuta ya kupikia vita hakuna. Vita imeanza Februari hapa!

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo kweli tukajivika kwenye suala hili la mafuta na vita ya Ukraine, hapa pana jambo Serikali inapaswa kufanya kitu! siyo tu kukimbilia kwamba sasa mafuta yamepanda basi na vitu vitakwenda kupanda, nasema siyo sahihi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tunakumbuka vizuri Waziri Dkt. Ashatu aliwahi kusema hapa tumeunda Tume inapitia huko itakuja na taarifa, hivi wenzangu ile taarifa mliipata? Kwa hiyo, lazima tuende vizuri, tukubaliane vizuri. Serikali ina jambo la kufanya hapo pamoja na vita hii ina jambo la kufanya.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa wapi? Mheshimiwa Waziri wa Fedha.

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba Serikali ina fursa ya kujibu lakini ni vizuri majibu ambayo wananchi wangetamani kuyapata muda ule ule yatolewe muda ule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza ambalo ningependa na Wabunge wote pamoja na wananchi waelewe, hakuna mtu Serikalini aliyesema jambo lililosababisha bei za bidhaa kupanda ni vita peke yake hakuna! Hakuna mtu aliyesema hivyo!

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mtiririko wa vitu zaidi ya kimoja ambavyo vimesababisha bei za bidhaa ziweze kupanda. Jambo la kwanza ambalo lilitangulia kabla ya yote ilikuwa ni *COVID*-19 na madhara ya *COVID*-19 kiuchumi siyo ya siku ile ile jamani hiki ni kitu cha kawaida. Usipozalisha leo utakula ulichozalisha jana ila siku ambapo unatakiwa ule kile ambacho ulizalisha jana kwa kuwa jana hukuzalisha ndiyo hakitakuwepo. Madhara ya *COVID* yasingetokea mwaka 2019, madhara ya *COVID lockdown* ya mwaka 2019 inatokea mwaka 2020/2021 hivyo ndivyo uchumi unavyokuwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hapa mtu asipolima mwaka jana hapati njaa mwaka jana ule ambao hakulima, anapata njaa mwaka ambao unafuata. Kwa sababu, ndiyo unapotakiwa kuvuna. Kwa maana hiyo, madhara ya bei kupanda siyo tu vita peke yake yamelundikana kuanzia *COVID* hilo la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili; kwetu hapa Tanzania wengine wanasema sasa mbona imetokea vita kule mbona na alizeti mafuta yake yamepanda bei? Tukumbuke mwaka jana Wabunge angalieni *Hansard* zetu

hapa mwaka jana Mikoa yote haikupata mvua katika kipindi ambacho kinatakiwa kiwe hili wala siyo vita ni ukame. Mikoa yote, kote mnakotokea mvua hazikuanza kama ambavyo huwa zinatakiwa kuanza.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la tatu sasa ndiyo imekuja hiyo ya vita, baada ya vita imepandisha vitu vingine vyote kwa sababu ya masuala ya mafuta, lakini hata ile *demand* tu imekuwa kubwa katika maeneo mengine yote yale. Baada ya *demand* kuwa kubwa ndiyo inasababisha *pressure* ya bidhaa zingine zote, hiyo inakuwa *spiral* yaani inaongezeka *inaji-fuel.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata sasa hapa tunapoongea hivi tulipo hapa…

**MWENYEKITI:** Ahsante sana kwa ufafanuzi Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Benaya Kapinga endelea kuchangia.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana tunachukua hatua kidogo kidogo ambazo zinasaidia…

**MWENYEKITI:** Hapana. Nimekuita Mheshimiwa Benaya Kapinga endelea kuchangia. Mheshimiwa Waziri wa Fedha naomba sasa uketi. Mheshimiwa Kapinga endelea.

**MHE. BENAYA L. KAPINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na nashukuru kwa maelezo mazuri ya Serikali na mimi sikatai lakini nasema tuna jambo la kufanya zaidi ya tulivyofanya sasa hivi. Kama nilivyosema mwezi Januari Serikali ilisema kuna Tume imeundwa inafuatilia hayo malalamiko ya bei ya bidhaa kupanda, nimehoji hapa ile taarifa ilipatikana na ilifanyiwa kazi ipi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nilindie muda wangu kwa sababu dakika kadhaa zimekwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale Jimboni kwangu kuna shida nimempongeza hapa Mheshimiwa Waziri Mkuu kafanya kazi nzuri Ngorongoro, Serikali imejipanga vizuri, wananchi sasa kwa utaratibu mzuri kabisa wanahamishwa au watahamishwa kutoka Ngorongoro kuja maeneo mengine yaliyopangwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale Jimboni kuna mradi wa panda miti kibiashara, mradi huu ni mzuri sana. Mradi huu utekelezaji wake niliusema hapa mwaka jana na ninaendelea kuusema leo, mradi huu ulipotekelezwa ni maeneo ya wananchi ni maeneo ya wakulima. Wakulima wale walikuwa wanamiliki maeneo yale kihalali kabisa kwa miaka yote ya nchi hii, lakini

bahati mbaya sana imefika sehemu sasa umeanzishwa mradi ukawapuuza wale wananchi. Wananchi wale wamebaguliwa hawana chao, wamekalishwa tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maeneo hawana haki tena, hivi sasa hivi kuna risasi zinapigwa pale, hivi sasa hivi kuna mapanga yanapigwa pale, wananchi wale hawana haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuomba unilindie muda sijui hiyo ni kengele ya ngapi?

**MWENYEKITI:** Nimekuongeza dakika moja malizia hoja yako.

**MHE. BENAYA L. KAPINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa hiyo naiomba Serikali kama ilivyofanya Ngorongoro, naiomba Serikali vivyo hivyo iende pale Jimboni eneo la Ndika ikasuluhishe hili. Kwa sababu maeneo yale ni haki ya wakulima wale. Wamepanda miti sawa sijui ni ya nani haieleweki kwa sababu kila mtu anasema mara ya Kijiji, mara ya mtu fulani, mara ya *TFS* hakuna anayejulikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru sana Mkuu wa Wilaya ameunda Tume na sasa hivi wanaendelea na mchakato, lakini bahati mbaya sana kasi yake sio ile ya kutoa majibu haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ni suala la Madiwani. Madiwani hawa wana kazi nyingi sana pale wanapokuwa katika maeneo yale lakini malipo yao hasa kwenye eneo la posho za kujikimu. Upo Waraka wa tarehe 02 Januari, 2019 unaosema fedha za kujikimu atapewa Diwani anayelazimika kulala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina hakika Wabunge Waraka ule nasi unaweza ukafanya kazi, sina hakika. Kama sivyo kwa nini kwa Madiwani kuwe na Waraka unaosema fedha ya kujikimu apewe yule anayelazimika kulala, wakati maeneo ya vijijini ulazima wa kulala upo tu. Mtu anaweza akaja sasa hivi kwenye kikao, kikao kikaisha Saa 10 hakuna usafiri wa kurudi kwenye eneo lake lazima atalala. Lakini tafsiri ya wale wanaotafsiri ule Waraka wanasema posho ya kujikimu atalipwa yule Diwani anayelazimika kulala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waraka huu ni wa kibaguzi kama kwa upande wetu hautumiki ningependekeza Serikali ifute Waraka huu, kwa sababu unawabagua. Wote ni viongozi wa kisiasa Madiwani ni wanasiasa na Wabunge ni wanasiasa na viongozi wengine. Kama hautumiki hapa kwa maana ya kwamba, kwa sababu kuna Wabunge wanaolazimika hata wasilale, lakini kama hautumiki hapa basi hata kwa Madiwani Waraka huu ufutwe. Madiwani wale walipwe posho zao za kujikimu kama wanavyolipwa wengine wanaolazimika kulala. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. BENAYA L. KAPINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ninamuita Mheshimiwa Ritta Kabati wakati huo Mheshimiwa Abubakari Asenga na Mheshimiwa Aloyce Kamamba wanajiandaa.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa na mimi nafasi niweze kuchangia hoja iliyopo mezani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimtangulize Mwenyezi Mungu katika mchango wangu. Pia, niwatakie Ramadhan Karim Waislam wote pamoja na Wakristo wote ambao wamefunga katika mwezi huu Mtukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami niungane na wote ambao wameweza kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kazi nzuri ambazo amekuwa akizifanya na hotuba yake, vilevile niendelee kuwapongeza wote waliompongeza Mheshimiwa Rais wetu Mama Samia. Kwa kweli anafanya kazi nzuri na anatekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa vitendo. Naomba Watanzania wote hasa akina Mama na akina Baba tumuunge mkono ili kazi iendelee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze hoja yangu kwa kuzungumzia jambo kubwa lililopo katika Mkoa wetu wa Iringa, kuhusiana na ukatili wa kijinsia dhidi ya watoto. Hili ni janga la Taifa. Tulipopokea taarifa katika *RC* tuliona karibu matokeo 439 kwenye Mkoa wetu yameripotiwa ya ukatili wa kijinsia. Kuna Wabunge wamechangia kuhusiana na huu ukatili, hili jambo ni zito mno. Mimi naomba Serikali iangalie, hili ni tatizo kubwa ambalo tunatakiwa tuungane na tunatakiwa sasa tuanze kulifanyia kazi na itengwe bajeti kuhakikisha kwamba hili janga katika Tanzania tunaanza kulitatua ili tutengeneze watoto ambao watakuwa kizazi kizuri katika nchi yetu. Hili ni tatizo kubwa ambalo tunatakiwa tuungane na tunatakiwa sasa tuanze kulifanyia kazi na itengwe bajeti kuhakikisha kwamba, hili janga katika Tanzania yetu tunaanza kulitatua ili tutengeneze Watoto ambao watakuwa kizazi kizuri katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo mambo ambayo niliyabaini nilipofanya ziara katika Mkoa wa Iringa na Wilaya zake zote. Sasa hivi kwanza watoto wameanza kubakana wao kwa wao, wanalawitiana wao kwa wao. Tatizo kubwa ambalo lipo hasa watoto wadogo ambao wanasoma Shule za Msingi, unakuta kwamba shule zetu nyingi za msingi hazikarabatiwi, hazina vyoo, hazina uzio kwa hiyo, unakuta watoto wanashindwa kwenda chooni wanakwenda kuomba kwa majirani, wanakwenda kwenye milima kujisaidia wao kwa wao kwa hiyo, huko ndiko ambako wanabakana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tumeshaona kwenye vyombo vya Habari sasa hivi tunaona kwamba, karibu kila Mkoa hili janga lipo. Kwa hiyo, naiomba Serikali hebu tutenge bajeti ya kutosha tuhakikishe shule zetu za msingi zinakuwa na vyoo, shule zetu za msingi zinakuwa na uzio kulinda hawa watoto wetu ambao sasa hivi hili limekuwa ni janga kubwa ambalo linahitaji maombi hata viongozi wa dini sasa hivi watusaidie pengine ni pepo kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo jingine ambalo nilikuwa nataka kulizungumza, nilitaka kuzungumza taharuki ambayo imejitokeza katika Mkoa wetu wa Iringa na Njombe. Tunaona Mheshimiwa Chumi alizungumza kuhusiana na *TANESCO* kuanza kuagiza nguzo kutoka nje, leo hii tumemuona Mbunge wa Njombe Mjini na yeye ameielezea hiyo taharuki na mimi kama Mbunge wa Iringa katika hiyo Mikoa miwili, niombe kwanza kabla sijazungumza kwamba Waziri mwenye dhamana hebu akae na Wabunge, Waziri mwenye dhamana ikiwezekana hata tuende tukafanye mikutano mikubwa kwenye Mikoa yetu ya Iringa na Njombe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri Mkuu ulikuja Iringa, ulishuhudia wewe mwenyewe ulifungua nembo yetu, ile *Iringa Woodland,* kama ambavyo labda wenzetu Mwanza wana *Rock City* sisi tuna *Woodland*. Kwamba, Mkoa wetu wa Iringa kipato kikubwa kinatokana na mazao ya misitu. Sasa hivi Halmashauri zetu nyingi zinategemea misitu na tuna viwanda zaidi ya 18 kwenye Mikoa hii miwili, kuna ajira nyingi sana imetengenezwa kupitia nguzo. Sasa tunaomba Mheshimiwa Waziri Mkuu hebu uangalie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile mapato ya Halmashauri kwa sababu, hizi asilimia 10 unaona akina Mama, Vijana na Watu Wenye Ulemavu walipata mikopo mikubwa hata Mheshimiwa Ummy alivyokuja pale Iringa kutokana na mapato makubwa yaliyopatikana kutokana na mazao ya misitu ambayo ni nguzo. Kwa hiyo, tunaomba kabisa hili jambo lisipuuziwe tukahikikishe kwamba, tunakaa ili kutatua hili tatizo ili Mikoa hii iendelee kutumia misitu au hizi nguzo. Kama kuna changamoto kwa nini Wizara ya Viwanda isilete ile teknolojia ikafundisha katika viwanda vyetu ili nguzo ziwe na kiwango? *(Makofi)*

**MHE. NEEMA W. MGAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa!

**MWENYEKITI:** Kuna Taarifa wapi? Aah! Mheshimiwa Neema Mgaya, taarifa.

**T A A R I F A**

**MHE. NEEMA W. MGAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumpa taarifa Mheshimiwa Ritta kwamba, kinachosikitisha zaidi nguzo hizo hizo ambazo zinatoka Njombe na Iringa na maeneo mengine ya Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini, zinatoka tu nje ya Tanzania zinakwenda zinarudi tena kwa mlango mwingine zije kuuzwa kwa bei kubwa, wakati nguzo ni za kwetu wenyewe Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, Mheshimiwa Ritta napenda kukwambia kwamba, Mheshimiwa Waziri kuna haja ya kukaa na Wabunge wa Nyanda za Juu Kusini, hususan Wabunge wa Mkoa wa Iringa na Njombe ambao tunalima mbao hizi na kutengeneza nguzo hizi ili kuweza kuisaidia Tanzania kutotumia gharama kubwa katika gharama za nguzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile…

**MWENYEKITI:** Ahsante kwa taarifa Mheshimiwa Neema Mgaya. Mheshimiwa Ritta Kabati unapokea taarifa?

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naipokea taarifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huo ndiyo kweli kabisa. Isitoshe *TFS* inazalisha nguzo kwa kiwango kikubwa sana, sasa na yenyewe itakosa mapato kwa sababu ni taasisi pia ya Serikali, vilevile wanawake, vijana na wananchi wa Iringa wamehamasika kwa kiwango kikubwa kuhakikisha kwamba wanalima miti ya kutosha katika Mkoa wetu wa Iringa. Hiki ndiyo kipato chetu na sisi kama ambavyo wengine wanasema kuhusu korosho, wengine wanazungumza kuhusu makinikia, nasi makinikia ya Mkoa wa Iringa ni misitu yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nguzo zetu hazina kiwango ndiyo hivyo nimesema kwamba, Wizara ya Viwanda ilete hiyo teknolojia ili tuzalishe nguzo zenye viwango ili tuweze kupata pato kubwa katika kutumia misitu yetu. *TBS* wapo na wenyewe waangalie wanatumia teknolojia gani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nataka kulizungumzia ni kuhusiana na hizi asilimia 10 ambazo zinatolewa katika Halmashauri zetu ambazo wanapewa Vijana asilimia Nne, akina Mama asilimia Nne, na Watu Wenye Ulemavu asilimia Mbili. Mimi naiomba Serikali waboreshe hii mikopo badala ya kupatiwa pesa unaona katika taarifa vijana wengi sana bado kuna pesa ambazo hawajazichukua, ni kwa nini Serikali isianze kutoa vifaa au mashine ili tuwe na viwanda vidogovidogo katika Halmashauri zetu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikitoa mfano labda kwa vijana. Vijana ambao wamesomea wanaweza wakapewa mashine za kufyatua tofali na wameshajifunza na hapohapo Halmashauri ile ikaweza kuchukua tofali kwa vijana wetu. Mimi naomba kwa kweli, jambo hili liangaliwe na nitaliandika

kwa vizuri zaidi ili hii mikopo ya akina mama, vijana na wanawake iweze kuwasaidia vijana, iweze kurudi iwe *revolving fund. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho naomba niunge mkono hoja, niseme tuungane wote kuhakikisha tunamsaidia Mama yetu Rais, ili kazi iendelee. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Sasa namuita Mheshimiwa Abubakari Asenga, wakati huo huo Mheshimiwa Aeshi na Mheshimiwa Kamamba wanajiandaa.

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kupata nafasi hii ya kuchangia hoja iliyopo mezani ya hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Nami kama walivyosema wenzangu kwa kanuni ile ya kibinadamu, usipomshukuru mtu basi hata Mwenyezi Mungu huwezi kumshukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru Serikali ya Awamu ya Sita na Viongozi wote wa Serikali kwa miradi mbalimbali ambayo wananchi wa Jimbo la Kilombero, Mkoa wa Morogoro wameendelea kuipata. Tunamshukuru Mkuu wetu wa Mkoa Mheshimiwa Martin Shigela na viongozi wake wote na Wakuu wa Wilaya kwa usimamizi mzuri unaoendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika vitu unatakiwa kuviomba katika mjadala huu wa kupanda bei ambao unaendelea katika Bunge lako ni kuiomba Serikali na kumuomba Mwenyezi Mungu kwamba, miradi ya Serikali na mipango na mikakati yote ambayo imesomwa kwenye hotuba ya Waziri Mkuu isije ikakwama, kwa sababu Serikali ilishajipanga kutuletea maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo tulipambana katika corona baadhi ya miradi haikukwama, tumuombe sana Mwenyezi Mungu miradi yetu isikwame.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasi kama Wabunge tunatoa mawazo yetu hapa, lakini kama walivyosema baadhi ya Wabunge tusisahau kumtanguliza pia Mwenyezi Mungu mbele, tumuombe Mwenyezi Mungu atusaidie janga hili tuvuke salama. Semeni Amina. *(Makofi)*

**WABUNGE:** Amina. *(Makofi)*

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mwenyezi Mungu awajalie viongozi wetu busara na hekima tushikamane wakati huu Watanzania, semeni amina!

**WABUNGE:** Amina. *(Makofi)*

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu katika ukurasa wa 29. Ni imani yangu kuwa Mheshimiwa Waziri Mkuu atanisikiliza, ukurasa wa 29 ametoa taarifa ambazo napenda Waziri wa Kilimo azisikilize.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na tatizo hili la kupanda bei lakini kama wananchi wetu wanaendelea kuzalisha halafu katika kuzalisha huko wanakutana na vikwazo, tunazidi kuongeza uchungu mara mbili. Mheshimkiwa Waziri Mkuu katika ukurasa wa 29 anasema, katika vyama vya ushirika 6,013 vilivyokaguliwa vyama vyote hati mbaya, hati chafu, kasoro vyama 300 tu vya ushirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nataka kusema hapa vizuri kabisa, kama Mheshimiwa Waziri Mkuu katika hotuba yake ameona katika vyama 6,013 vya ushirika vilivyokaguliwa na *CAG,* vyama 2,674 Hati yenye Shaka, vyama 1,253 Hati Isiyoridhisha, vyama 1,729 Hati Mbaya kasoro vyama 300 tu. Mpaka tunavyozungumza hivi huko kuna wakulima wanauza mazao yao kupitia ushirika, Warajisi wa Ushirika wapo maofisini wanaendelea kula bata, biashara kama kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri wa Kilimo nina imani naye ananisikiliza kwamba, tunaomba mabadiliko. Kwa mfano, Mkoa wa Morogoro tumeshalalamika sana kuhusu Mrajisi wa Mkoa. Tumeshalalamika sana kumhusu Mrajisi wa Kanda na nimesikiliza baadhi ya Mikoa hapa wamelalamika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi hii ni moja. Mimi nilikuwa *DAS* Rombo na wewe ulikuwa *DAS* Arusha unakumbuka, tumeondoka Kilimanjaro tuna malalamiko ya Mrajisi wa Mkoa. Tumefika hapa aliyekuwa Waziri wa Kilimo wakati ule akatumia siku tatu kufanya mabadiliko ya Warajisi wa Mkoa. Kwa nini Kilombero hawafanyi mabadiliko na Mkoa wa Morogoro haufanyiki mabadiliko?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaeleza sababu na Mheshimiwa Waziri nimemtumia mpaka *video* na sauti kwamba, kuna watu kule wanasema mua na sukari ni dhahabu nyeupe, wanafanya wanavyotaka. Sasa mwananchi akizingatia huku kuna bei zinapanda, huku ana mua wake kiwandani, hapewi nafasi ya kwenda kuuza hasira inapanda mara mbili. Tunaomba Waziri wa Kilimo mmezindua kilimo vizuri sana vijana wameanza kupenda kilimo, lakini ushirika utawavuta nyuma na ushirika unaweza ukawa kama dude ambalo limewashinda Mawaziri wengine huko nyuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fanyeni mabadiliko Kilombero na katika Mkoa wote wa Morogoro. Kwa nini Mrajisi huyu haondolewi malalamiko yote tumeyasema? Kwa nini huyu Mrajisi wa Kanda sijui anaitwa Ndugu Mshumba?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa nitakuomba nita-*play* sauti ya mwananchi mmoja kati ya wananchi 20 walionipigia simu kumlalamikia huyu mtu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanapandikiza Wakandarasi, wanafanya mambo yao, wanavuruga kilimo na kilimo cha mua ni muhimu katika nchi yetu. Kilimo cha mua ni muhimu kwa wananchi wa Kilombero. Kilimo cha mua kinatusaidia kujitegemea katika sukari, lakini Warajisi wanafanya madudu wanavyotaka wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wanaenda kwenye Mkutano Mkuu wanavunja Bodi wao wanalazimisha kuleta watu wa bodi wanaowataka wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa sishangai Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kusema vyama vyote vya ushirika vilivyokaguliwa ni hovyo, wala sishangai kwa sababu ya Warajisi hawa ambao tunawalea. Nimemuona Mbunge wa Katavi hapa Kaka yangu Kakoso analalamikia mambo ya ushirika, kwa hiyo naomba ichukuliwe hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba ni-*play* sauti mojawapo ya mwananchi ukiniruhusu, tusikilize hapa mwananchi analalamika kuhusu mambo ya ushirika ili Mheshimiwa Waziri aweze kuchukua hatua.

**MWENYEKITI:** Hapana Mheshimiwa, haujaruhusiwa kufanya hilo jambo.

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante nashukuru sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Asenga unatakiwa uombe na Kiti kikikuruhusu ndiyo uendelee. Endelea kuchangia.

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ni-*play* sauti ya mwananchi akitoa malalamiko yake kuhusu…

**MWENYEKITI:** *Table* Mezani halafu itapokelewa.

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sawa. Naomba kuendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kumaliza suala la ushirika nataka kuzungumzia kidogo kwenye suala la ujenzi. Ni imani yetu hapa kwamba, Mawaziri watakapokuja watatusaidia kujibu baadhi ya changamoto. Nimeona kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu amejaribu kuzungumza baadhi ya miundombinu inayojengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Wilaya ya Kilombero tuna changamoto moja kubwa ya barabara ya Ifakara – Kidatu. Sasa hivi tumekuwa wataratibu na wapole kwa sababu, tunaona dhamira ya dhati ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Katibu Mkuu wa Wizara Injinia Aisha Amour na Meneja Mkuu wa *TANROADS* Injinia Mativila. Tuna imani kwamba, Waziri atakapokuja hapa atatuambia ule mkwanziko wa *settlement* na Mkandarasi kikao kitafanyika lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba ukija hapa Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi atatusaidia kujua ahadi ya Mheshimiwa Rais katika eneo la Mang'ula Kona aliyotupatia itaisha lini? Fidia za wananchi waliotoa kuhusu ile barabara zitaisha lini? Na kwa nini Kilombero ilirukwa katika taa za barabarani? Nafikiri tutapata majibu hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema katika ujenzi nataka kuzungumza katika Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kidogo, nina imani Mawaziri wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa watakuja hapa. Sisi kama wananchi wa Kilombero katika Bunge hili la Bajeti tunatarajia tulitoa wazo kwamba, kama ilivyofanyika katika Wizara ya Maji, Mheshimiwa Rais amenunua miundovifaa vya kupima maji na kuchimba maji, tulitoa wazo *TARURA* ni vizuri Serikali ikanunua vifaa kama ma-*grader, excavator,* kwa baadhi ya Wilaya ikazipatia vifaa hivi ili kupunguza gharama kubwa za ujenzi wa barabara ambazo sasa hivi hali yake ni mbaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wamesema hapa upande wa Wizara ya Afya nami nataka kuchangia kidogo. Wakati nimesimama hapa nazungumza nilimpa Naibu Waziri wa afya juzi ki-*memo* changu kumwambia hospitali yetu, kituo chetu cha Kibaoni-Ifakaraka ambacho tunakitumia sasahivi kama hospitali ya Wilaya hakina dawa kiasi kwamba, wamama wajawazito wanarudishwa nyumbani bila dawa. Sasa Wabunge wengi wamesema hapa kuhusu mambo ya *MSD* na mimi naomba Serikali na Mheshimiwa Waziri Ummy wachukue hatua za haraka iwezekanavyo kuhakikisha wanakabiliana na suala la dawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la maji. Tuna imani Waziri wa Maji atakapokuja hapa tunataka kusikia habari ya Miji 28. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais Samia ametaja miradi ya Miji 28 na Ifakara, Kiburubutu, ipo ndani ya miradi ya Miji 28. Imani yetu ni kwamba Waziri wa Maji atakapokuja hapa atatupa picha na muda gani mradi wetu ule unaenda kutolewa majibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, sitaki useme. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Abubakari Asenga. Sasa namuita Mheshimiwa Aloyce Kimamba, wakati huo Mheshimiwa Aeshi Khalfan Hilaly anajiandaa.

**MHE. ALOYCE J. KAMAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nikushukuru kwa kunipa nafasi kuchangia hotuba ya Waziri Mkuu. Katika hili nianze tu kumshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa huduma ambazo amezitoa hasa katika Wilaya yetu ya Kakonko. Mama Wilaya ya Kakonko tumemuona katika madarasa, Mama Wilaya ya Kakonko tumemuona katika hospitali, na kadhalika, tunamshukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwetu Kigoma barabara ndiyo siasa, lakini bahati mbaya Mkoa wa Kigoma kwa nchi hii ndiyo Mkoa haujaungwa katika Mikoa mingine, kwa maana ya kuunganishwa na mikoa mingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatujaunganishwa Mkoa wa Kigoma kutoka Katavi, hatujaunganishwa Mkoa wa Kigoma kutoka Tabora, hatujaunganishwa mkoa wa Kigoma kutoka Kagera. Ni aibu kwa Serikali naweza nikasema. Katika hotuba ya mwaka jana Serikali ilisema kwamba, kuna hatua zinafanywa na wataalam wako kule, lakini kazi inayofanyika si njema. Ninaiomba Serikali ichukue hatua ya kusukuma mafundi ili waweze kukamilisha barabara katika Mkoa wetu wa Kigoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo nimezungumza, ipo barabara ambayo inatuunganisha Wilaya yetu ya Kakonko na nchi ya Burundi ambayo inaanzia Kakonko kwenda Kijiji cha Kinonko kwenda Nyakiyobe kwenda Gwarama kwenda Kabale mpaka Muhangi. Mpaka ule Serikali imejenga soko kubwa sana, lakini soko lile halina huduma, halitoi huduma vizuri kwa sababu hatuna barabara ya kuweza kutuunganisha pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana nilichangia na nimeomba sana muda mwingi, hebu Serikali chukueni hatua ya kuijenga barabara hii ambayo itaongeza uchumi kwa nchi hii. Pale maji yapo, pale umeme upo, lakini shida ni hiyo barabara. Naiomba sana Serikali itujengee barabara hiyo ambayo ni barabara ya kimkakati, itatusaidia kama nchi kuweza kupata fedha katika mpaka ule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo ahadi za Serikali. Mheshimiwa Lusinde amezungumza hapa, kila Mbunge akisimama atasema darasa langu halijakamilishwa, daraja langu halijakamilishwa, alisema Waziri Mkuu, alisema Mheshimiwa Rais. Kwa nini usifanywe utaratibu miradi yote, ahadi zote za Viongozi zikaweza kuorodheshwa na tukaambiwa Wabunge wote kuona kwamba, mimi ahadi yangu ambayo alitoa Rais, mimi ahadi yangu alitoa Waziri Mkuu, mimi ahadi yangu aliyotoa Makamu wa Rais imewekwa kwenye orodha, ili wote tujue kwamba, ahadi ambazo zimetolewa na viongozi zimeorodheshwa na hivi kila Mbunge ataweza kuridhika kwa sababu,

atakuwa na uhakika kwamba, ahadi iliyotolewa na kiongozi kwenye eneo lake ipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba ikishafanywa hiyo tuanze na ahadi ambayo ilitolewa na marehemu Magufuli katika Mji wa Kakonko. Katika Mji ule tuliahidiwa kilometa tatu ambazo ziko ndani ya Mji wa Kakonko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikwambie kwamba, mpaka muda huu ndani ya miaka Sita tumeweza kujengewa kilometa 0.63. Kwa hiyo, niombe Serikali inapochukua hatua ya kuiorodhesha miradi yote, basi namba moja uwe mradi huo wa ujenzi wa barabara ya lami katika Mji wa Kakonko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo barabara za Mji wa Dodoma. Mji wa Dodoma unakua, hatutegemei kwamba Mji wa Dodoma sasa utakuja urudi kuwa Manispaa au uje kuwa Mji wa kawaida ni Jiji sasa, lakini Serikali hatuoni mbanano wa magari kwenye Mji huu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii kutoka Kisasa kuja hapa mpaka Bungeni ni shida kweli. Polisi wakishafunga barabara, labda Waziri Mkuu anakuja au Makamu wa Rais anakuja kwenye shughuli mbalimbali, inakuwa ni mtafutano kwelikweli. Ninaiomba Serikali ichukue hatua ya kujenga barabara ambayo itaruhusu malori badala ya kuingia Mjini katikati Dodoma, basi malori yaweze kupita kule pembeni, nina hakika itasaidia Mji katikati kubaki wazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ipo huduma ambayo inatolewa kwa upande wa miamala ya fedha. kutoa fedha kutoka kwenye *account* kwenda kwenye mitandao tofauti-tofauti mfano, tiGO Pesa, M-Pesa, na kadhalika ili uweze kupata huduma hiyo lazima uwe na shilingi 1,000. Inaweza ikatokea kwamba, wakati uko kwenye utaratibu wa kutoa huduma hiyo *network* ikakata, Shilingi 1,000 imeshachukuliwa, utakaporudia usifanikiwe 1,000 imeshachukuliwa, ukirudia na kadhalika utastukia kwamba, Shilingi 5,000 zimekwenda lakini huduma ile haijatolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Serikali ifuatilie hilo, kuona uwezekano wa kwamba kama huduma haikuweza kupatikana basi hizo fedha zisiweze kutoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa mitandao ya simu Wilaya yangu ina shida sana ya mtandao wa simu, shida ipo kubwa sana katika Kata ya Nyamtukuza, Kata ya Nyabibuye, Kata ya Gwarama, Kata ya Rugenge, Kata ya Mugunzu, Kata ya Katanga, Kata ya Kanyonza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata mimi nikiwa nyumbani siku ukinitafuta usinipate ujue kwamba niko nyumbani mawasiliano hadi nyumbani kwangu hayapo, ninaiomba Serikali ichukue hatua hasa kwenye Mikoa ya pembezoni na Wilaya za pembezoni ziweze kupata huduma ya mitandao ya

simu ili tuwe na uhakika kwamba kila Mtanzania anaweza akafurahia mawasiliano ya simu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu upande wa umeme, bado kuna shida ya umeme katika Mkoa wa Kigoma. Muda huu tunaambiwa kwamba kuna ujenzi wa *lane* ya umeme kutoka Nyakanazi kwenda Kigoma, hao mafundi hatuwaoni ninaomba Serikali ichukue hatua ya haraka kuona kwamba Kigoma nasi tunapata umeme kwa ajili ya maendeleo ya Mkoa wa Kigoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Aloyce Kamamba. Sasa ninamuita Mheshimiwa Aeshi Khalfan Hilaly wakati huo Mheshimiwa Fakharia Shomari na Mheshimiwa Toufiq Turky wanajiandaa.

**MHE. AESHI. K. HILALY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Awali ya yote naomba niipongeze Serikali, nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa anayoifanya pia nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa wenyeviti wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina hoja mbili tu, kwanza nilitaka nilikumbushe Bunge siyo kila mtu anayechangia humu ndani kwa maslahi ya Taifa inaonekana kuna jambo limepita au kuna mtu amenunuliwa au kuna rushwa imefanyika ni lazima kama Wabunge tuko hapa kwa ajili ya kuwakilisha wananchi, lile ambalo tunaliona haliendi sawa tuna umuhimu wa kuja kulisema hapa na Serikali iweze kulifanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile upande wa Waheshimiwa Mawaziri pale wanapoona kuna tatizo basi walisimamie hili jambo liweze kuisha kuliko kuwa na uwoga wa kutokulisimamia jambo ambalo tunaona haliendi sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge lililopita nilikuwa Makamu Menyekiti wa Hesabu za Serikali, tulikuwa na mgogoro wa uwekezaji kule Kigamboni katika mradi wa *Dege ECO Village*. Spika aliagiza na baada ya kuagiza Kamati ikakaa na baada ya Kamati kukaa, ikaunda Kamati ndogo kufuatilia jambo hili, majibu yakaja ndani ya Bunge, Bunge likapitisha Azimio lakini cha kushangaza baada ya Bunge kuvunjwa Mkurugenzi wa *NSSF* pamoja nafikiri na Waziri labda anaweza kuwa anahusika sina uhakika sana, ikachukuliwa maamuzi ya kumkamata Mwekezaji na kumuweka ndani siku 21 na kumnyang'anya kila kitu ambacho alikuwa amewekeza katika mradi ule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ule mradi ni mkubwa sana, Serikali imewekeza fedha nyingi sana katika mradi wa *Dege Eco Village* ambao uko Kigamboni. Sasa matokeo yake mradi ule umekuwa magofu haujulikani uko wapi, ukienda Serikalini kuuliza wanakwambia mradi huu tumeuchukua umeuchukua kwa njia gani, haijulikani!

Mheshimiwa Mwenyekiti, wasiwasi wangu ni kwamba tumemkamata Mwekezaji tukauchukua kwa kumlazimisha, leo Serikali imechukua ule mradi unatafuta Mwekezaji mwingine uweze kuuza, wasiwasi wangu na angalizo langu ni kwamba mwakani au baada ya muda mchache Mwekezaji anaweza kwenda Mahakamani na akashinda kesi ile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninaiomba Serikali ije na majibu mazuri. Kwanza ituambie ni njia ipi iliyotumia kuweza kumnyang'anya mwekezaji *share* zake. Pili, mradi ule ulikuwa na Wakandarasi wako *site,* wale Wakandarasi wanalipwa na nani? Mradi umechukuliwa lakini wale Wakandarasi wanadai fedha zao. Je, Serikali italipa au ndiyo wanadhulumiwa moja kwa moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili linasikitisha sana kulikuwa na Wakandarasi zaidi ya 20 pale, yuko Mkandarasi Mkuu wako ma-*subcontract* wengi sana walikuwa wamefanyakazi pale. Lakini mpaka leo hawajalipwa pesa na mradi umechukuliwa na Serikali sasa nani atakayelipwa ninamuomba Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa sababu hii taasisi iko chini yake, aweze kutuletea majibu anapokuja kufanya majumuisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine kubwa zaidi ambalo nimeliona ni vizuri Serikali ikafahamu, Mheshimiwa Waziri Mkuu ameongelea suala la *SGR* hapa kwamba ni mradi mzuri unakwenda vizuri tumeanza na loti namba moja tumekuja na loti namba mbili na sasa hivi tunaelekea loti namba tatu na tunaelekea kumaliza na loti namba nne mpaka namba tano na namba sita, naomba niipongeze sana Serikali kwa kazi kubwa sana iliyoifanya. Lakini ninaona kuna changamoto na changamoto hiyo nisipoiongelea nitakuwa siyo mzalendo wa nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeweza kujenga loti namba moja, tumejenga loti namba mbili tukaruka tukaenda kujenga loti namba tano. Mimi ni mjumbe wa Kamati ya Miundombinu, Wajumbe wa Kamati wenzangu wengine wako hapa, tulipoenda kukagua maeneo yote tumeridhika kabisa na maeneo namba moja na namba mbili tumeenda namba tano tumekuta hali si shwari, Mkandarasi wa pale amejenga kwa asilimia Nne tu mpaka sasa na ana muda wa mwaka mmoja na miezi minne lakini hakuna jambo lolote lililofanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hoja yangu inakuja tumetangaza *tender* nyingine loti namba sita ambayo inatoka Tabora kwenda Kigoma hapa kuna harufu mbaya sana ya rushwa, Waziri anatumia madaraka vibaya ya kutumia neno linaitwa *single source* kugawa kazi kwenye makampuni ambayo hayana sifa. Mkandarasi aliyeshinda nafasi hiyo ambayo amepewa *tender* ya kujenga barabara ya kutoka Tabora kwenda Kigoma, Mkandarasi huyu ndiye anayejenga loti Namba *Five* ambaye amejenga

asilimia Nne, na sasa hivi wanampa kujenga loti Namba Sita kwa *single source*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii *single source* nataka niijue inatumia vigezo gani ili kuweza kumpa Mkandarasi aweze kuendelea na mradi mwingine.

**MHE. MIRAJI J. MTATURU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**T A A R I F A**

**MWENYEKITI:** Taarifa.

**MHE. MIRAJI J. MTATURU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimpe taarifa anayezungumza sasa hivi Mheshimiwa Mbunge, kwamba wakati tunakagua mkandarasi huyu wa China katika loti hiyo ambayo anaisema ya Isaka Mwanza, tuligundua mapungufu makubwa sana mojawapo ikiwa ni matatizo ya kiusalama kwa wafanyakazi hata *First Aid Kit* hakuna, *ambulance* zinazotakiwa ziwepo hakuna, hata sasa hivi kama unavyosema muda aliopewa hadi sasa ni asilimia Nne tu. Kwa hiyo, maana yake ni kwamba angekuwa na sifa ya kupewa hiyo *single source* ni yule aliye *perform* vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, nataka nimpe hiyo taarifa.

**MWENYEKITI;** Ahsante na muda wako ndiyo kama hivyo Mheshimiwa Aeshi.

**MHE. AESHI. K. HILALY:** Hapana!

**MWENYEKITI:** Basi hitimisha hoja yako kwa dakika moja Mheshimiwa.

**MHE. AESHI. K. HILALY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ngoja niendelee, nimeipokea taarifa

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa nitapunguza taarifa kwa sababu muda upo mwishoni halafu wachangiaji lazima wamalizie wale wawili, malizia Mheshimiwa Aeshi kwa dakika moja.

**MHE. AESHI. K. HILALY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napokea taarifa, lakini la msingi hapo ninataka kusisitiza ni kwamba Mkandarasi huyu ambaye ameshindwa ku-*perform* amepewa tena *tender* ya kujenga kutoka Tabora kwenda Kigoma. Hoja ya *single source* ni pale Mkandarasi anapo-*perform* vizuri, anapofanyakazi vizuri ndiyo apewe kazi nyingine. Sasa mtu ambaye amejenga kwa asilimia Nne, hatujajua anajenga kwa kiwango gani tunamuongezea kazi nyingine ambayo hii hata asilimia 10 hajafika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo ni kwamba kuna vitu havifanyiki sawa, nasi Wabunge hatutakiwi kukaa kimya.

**MWENYEKITI:** Ahsante. hata hivyo muda wako umekwisha.

**MHE. AESHI. K. HILALY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaanza kusababisha watu kutaka kutoa rushwa, hatuwezi kukubali. Ninaiomba Serikali ije sasa na majibu mengine au iangalie upya utaratibu uliofanyika hauko sawa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri wa Fedha taarifa.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatambua mchango anaosema Mheshimiwa Mbunge, Mheshimiwa Aeshi nilitaka nitoe taarifa kwamba loti Namba Tano tangu ianze ilikuwa haijawahi kupata *financing,* fedha iliyokuwa inatoka ilikuwa ni fedha ambayo ilikuwa inawekwa akiba toka Serikalini. Hivi ninavyoongea ndiyo tunamalizia *evaluation* ya *financing* ya loti yote kuanzia Namba *Three*, Namba *Four* na Namba *Five*. Kwa hiyo, kwa sababu *financing* yake haikuwepo ni dhahiri kwamba kusinge kuwepo na kasi kubwa sana ya loti Namba Tano kwa sababu hakukuwahi kuwa na *financing* ambazo ziko *attached* na loti hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine hili ambalo amelisema nadhani ni michakato ndiyo inaanza hamna mtu ameshapewa kazi nadhani ni michakato ambayo inaendelea.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu!

**MWENYEKITI:** Nimekuona Mheshimiwa Esther Matiko.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Michakato ikiwa inaendelea hatuwezi tuka-*conclude* kwamba kuna tatizo kwamba kuna mtu amepewa.

**MWENYEKITI:** Kuhusu utaratibu kwa Kanuni gani?

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama tu kuhusu utaratibu.

**MWENYEKITI:** Kanuni namba ngapi Mheshimiwa Esther Matiko?

**MHE. ESTER MATIKO:** Kuhusu utaratibu ni Kanuni ya…

**MWENYEKITI:** Ahsante naomba uketi, Kanuni 75 endelea.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapokuwa tunachangia hapa Bungeni Mawaziri wanakuwa na muda wao baadae wa ku-*wind up,* lakini imekuwa ni utaratibu wakati tunachangia Waziri anasimama kuhusu taarifa anaongea zaidi ya dakika mbili, tatu akitoa

ufafanuzi. Sasa siyo vizuri na siyo utaratibu, Mawaziri wanapewa muda wao mwishoni, siyo utaratibu wanapewa muda wao dakika 10, dakika 15 za ku-*windup* wawe wanasubiri.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Esther Matiko, Kanuni uliyoitaja inakutaka utuambie Kanuni iliyokiukwa Kanuni Namba ngapi? Kanuni iliyokiukwa ehe?

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kuhusu utaratibu Kanuni ya 77 ukitoa taarifa unatoa kwanza *in a very brief manner,* lakini Mawaziri wamekuwa wakisimama wanajibu zaidi ya dakika mbili, dakika tatu wana muda wao maalum vinginevyo wakisimama wanatoa taarifa *in just* kidogo, taarifa ni nyingi.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Esther Matiko, niwakumbushe Waheshimiwa Wabunge kanuni yetu 75 inamruhusu Mbunge kusimama na kueleza Kanuni iliyokiukwa. Kifungu cha Pili kinasema Mbunge aliyedai utaratibu umekiuka atalazimika kutaja Kanuni au sehemu ya Kanuni iliyokiukwa sawa? malizia Mheshimiwa Aeshi.

**MHE. AESHI. K. HILALY:** Nimalizie.

**MWENYEKITI:** Malizia Mheshimiwa Aeshi

**MHE. AESHI K. HILALY:** Taarifa ya Mheshimiwa Mwigulu siipokei, kwa sababu haiingii akilini mtu ambaye amejenga kwa asilimia Nne hata kama fedha haijapatikana, halafu mtu huyo huyo mnaanza mazungumzo naye tena ya awali ya kumpa kazi nyingine ambapo kazi ya kwanza hajaifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sifa ya ukandarasi lazima awe na uwezo, kama uwezo anao angeanza kujenga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka hili uliweke sawa, kuna jambo hapa haliko sawa kabisa. Mheshimiwa Waziri anataka kuhalalisha jambo ambalo halipo, bado dakika moja nilikuwa nahesabu hapa.

**MWENYEKITI:** Hitimisha hoja yako sasa.

**MHE. AESHI K. HILALY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninahitimisha. Ninaiomba Serikali iangalie upya utaratibu huu wanaotaka kuufanya, utaratibu huu wa *single source* unataka kutumika vibaya, unataka kuhalalisha vitu ambavyo hatutoweza kukubali wala kuvifumbia macho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Sasa namuita Mheshimiwa Fakharia Shomar wakati mchangiaji wetu wa mwisho atakuwa ni Mheshimiwa Toufiq

Turky na kwa kuwa muda umekwenda sita *entertain* taarifa kwenye wachangiaji hawa wawili. Endelea Mheshimiwa.

**MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza sina budi kumshukuru Mama Samia ambaye ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Alhaj Hussein Mwinyi - Rais wa Zanzibar, Makamu wa Rais, Waziri Mkuu ambaye tayari ameweka hotuba yake ya bajeti mezani na Watendaji wake, pamoja na Mheshimiwa Spika na Naibu Spika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaanza na *TASAF*. *TASAF* imefanyakazi nzuri kwa Zanzibar, kwanza nitaizungumzia Unguja kwa sababu mimi ndiyo niliko *TASAF* kuna Shehia 126 zote zimefanya kazi nzuri wameweza kutoa ruzuku vizuri, wametoa ruzuku za vijana au watoto waliokuwa chini ya umri wa miaka 18 ambao wazee wao hawajiwezi, wametoa ruzuku kwa watoto wa chini ya miaka mitano kwenda kliniki, wametoa ruzuku kwa watoto wa kimaskini ambao wanaosoma Sekondari na *Primary,* wamewasaidia walemavu kwa ruzuku, wamewasaidia hata wajasiriamali, *TASAF* kwa Zanzibar tunaishukuru Serikali ya Muungano imesaidia vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile imechukua vijana wanaofanyakazi ofisi ya Makamu wa Rais Zanzibar ambao ndiyo wanasimamia *TASAF* wamewapeleka masomoni ili kwenda kuongeza ujuzi waweze kusimamia mazingira ya *TASAF*. Jambo likiwa nzuri likinafanywa na Serikali ya Muungano ikishirikiana na Serikali ya Zanzibar inabidi kulishukuru na kuliangalia vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba itakapokuja *TASAF* nyingine ya nne ifanyekazi vizuri zaidi ya hii iliyofanya sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuja na changamoto za Muungano ambazo Mheshimiwa Waziri Mkuu ziko kwenye ukurasa wake wa 72. Kwanza Muungano ni tunu kwa Tanzania na Muungano wetu unaendelea vizuri, lakini kwenye changamoto walituambia kwamba 11 tayari zimefanyiwa kazi na zishamalizika kabisa na Serikali zote mbili hoja hizo Tisa tayari wamekubaliana kwa kuandikiana na tayari zimeisha. Mbili ziko katika utendaji lakini mimi bado naona hakuna tunalolifanya kwanini niulize.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto hizi Wabunge tuliopo humu ndani msimamishe mmoja tumuulize hakuna hata atakayeelezea nini na nini kimetendeka na kwa sababu gani, baada ya kuisha kuzifanya au kutanzuliwa zimo katika makaratasi au mafaili, hazijasambazwa kama kutengenezewa vipeperushi au kutengenezewa vitabu au kwenda ofisini kwa viongozi wakati unamsubiri kiongozi ukakuta juu ya meza yake pale vipo ukawa unasoma au mashuleni mwetu, kwa sababu kuna vijana humu siyo wazalendo hizi changamoto kila siku wanazirejea hizo hizo kwa sababu hawazijui.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utakuta kila siku bandarini gari yangu imekamatwa kwa sababu hatuelewi nini kinachoendelea, sasa ninaomba Ofisi ya Waziri Mkuu changamoto zote ambazo mlikubaliana na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ziweze kuwekwa bayana kila mmoja azijue, vijana waliopo vijiweni, vijana waliopo shuleni, na vijana ambao watatumia hizi changamoto wakati wakitaka manufaa yao kuzorotesha au kufarakisha nchi anatumia hizi changamoto. Mheshimiwa Waziri Mkuu tuwe waungwana kwa kuweza kuzisambaza kila mmoja azipate. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la ukurasa wa 44 na 45 unazungumzia viwanja vya ndege na usafiri wa anga. Suala hili ni zuri na amesema ndege zetu zitatimia 16 ni jambo jema lakini kuna kitu kidogo ningeomba kiangaliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unajua hizi ndege zina *route* na *route* zake mpaka Zanzibar zinafika lakini mkae mkijua Zanzibar kuna Wabunge, wafanyabiashara, wafanyakazi wa Serikali na Wafanyakazi wa Chama wanakuja *direct* Dodoma. Sasa wakati mtu unataka kuja Dodoma kwa ndege lazima ukasubiri ndege Dar es Salaam ndiyo ufike Dodoma. Kwa nini *route* moja tusiifanye kwenye wiki *direct* Zanzibar *to* Dodoma unaitoa Dar, Dar inakuja Zanzibar, Zanzibar to Dodoma au unaitoa Mkoa wowote….

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Fakharia Shomari. Ahsante muda wako umekwisha.

**MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS:** Ahsante naunga mkono hoja na mimi nilikuwa nishamaliza.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Toufiq Turky atakuwa mchangiaji wetu wa mwisho kwa *session* yetu ya asubuhi.

**MHE. TOUFIQ SALIM TURKY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwanza naomba nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu *Sub-hanau Wataallah* kutujaalia mwezi huu Mtukufu wa Ramadhani uwe salama na baraka kwa Taifa zima, pia nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri anayoendelea kuifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge lililopita tulikuwa tunahojiana sana katika suala la tozo, kila mmoja anapiga kelele tozo lakini sasa hivi toka tumekuja wote wamekaa kimya kwa sababu zile neema za tozo kila kona ya Tanzania zimefika. Hivi tunavyoongelea mpaka mimi kupitia Jimboni kwangu nina Skuli ya Sekondari sasa hivi hapa nina meremera na *speed* yake kali, kwa hivyo ninaipongeza sana kwa ubunifu na nakiri kuzitumia hizi pesa ipasavyo kwa kila Mtanzania kupata zahanati na skuli kila kona. Kwa hiyo, tunampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa maamuzi hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nataka niipongeze Serikali kwa kuja na suala la *postcode* na suala la sensa, mataifa yaliyoendelea haya masuala mengi pengine watu hawaelewi kwa nini hizi *postcode* na sensa ina umuhimu wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *postcode* tunapata kujua kama kuna kifaa mtu yeyote unataka kumpelekea unajua njia gani, mtaa gani, nyumba gani, unampelekea unapata ile *postcode* na kwa kupitia sensa unajua ndani ya nyumba ile kuna watu wangapi, wana mahitaji ya aina gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kupitia hizi mbili ndiyo mataifa mengi yameweza kuendelea. Sasa hoja yangu au mchango wangu uko sehemu moja kwamba tunaweza tukawa na sensa tunaweza tukawa na *postcode* lakini kama hatuna mfumo wa kuwezesha watu kuitumia hizi *postcode* tutapata athari kubwa sana. Wenzetu sasa hivi wana *database* kupitia hii *database* ndiyo *service industries* wanapata kodi, leo kila siku tunatafuta tunabuni kodi kwa ajili ya mradi ndiyo maana vifaa bidhaa zinapanda bei, lazima sasa hivi tuondokane kwa mlaji tu tuende katika *services.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi ukitizama kuna mitandao ya *booking.com* kuna *Airbnb,* hatuna mfumo wa kuweza *direct* kupata hizi kodi. Watu wanalipa wanapata pesa zao Serikali inakosa kodi zile kwa kupitia watu kukodishwa.

Hali kadhalika kuna mataifa makubwa ya *Google*, *Facebook* wanafanyabiashara na watu wengi sana, sasa hivi tunafanya *online purchase* lakini kinachofanyika Serikali inakosa kodi zao. Ninachoomba sana tutafute mfumo wa kuhakikisha tunadhibiti kodi zetu kuweza kuzipata na hayo yote haitowezekana kama hatujawekeza katika elimu ya *artificially intelligence*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliongelea Bunge lililopita na safari hii naongea tena, jamani dunia inapoelekea inaenda katika *digital* hakuna jambo hata moja linalotumika bila *artificial intelligence,* bado elimu yetu hatujawekeza katika *artificial intelligence.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi Rwanda wameanza kwa kuwa wanataka kuwa ni sehemu ya *market* ya *AI* sisi tuko wapi? Leo mpaka unamaliza *University* somo la *coding* hatujalianzisha wenzetu kuanzia Darasa la Sita *coding* inakuwa ni *compulsory,* lazima watu wafundishwe *coding* wanajua dunia ijayo haitakuwa na mikono tena itakuwa dunia ya akili lazima tuwekeze elimu yetu katika *digitalization* ni ombi langu mahsusi hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia tuna wenzetu walemavu wa kuweza kuzungumza na kusikia, tunafurahi sana kuwa sasa hivi *television* zote wanakuwa wanaweka sehemu kwa ajili ya watu kufahamu. Lakini ni lazima pia tuanzishe katika madarasa japo zile *sign* ndogo ndogo za kuweza

kuongea nao mtu ana mahitaji yake haiwezekani mtu ana mahitaji leo, mahitaji yake mpaka akufanyishe kwa mkono hivi haipendezi tunawanyanyapaa! Kwa hivyo ninaomba sana kupitia sekta ya elimu tuanzishe *at least* kuwe na *curriculum* ya kuwa na masuala ya *sign language* lakini suala la *artificial intelligence* siyo tena suala la kulipuuza ni lazima lipewe kipaumbele chake, dunia ndipo inapoelekea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana naunga hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWONGOZO WA SPIKA**

**MWENYEKITI:** Mwongozo!

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama kwa Kanuni ya 76 Mbunge atasimama baada ya kutakapokuwa Mbunge hayupo anayezungumza. Ninaomba Mwongozo wako, wakati mjadala ulipokuwa unaendelea tumeshuhudia Mawaziri kui-*interfere* michango ya Wabunge ilihali wana muda wao wa kuja kujibu hoja za Wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wamevunja utaratibu ndani ya Kanuni zetu. Kanuni ya 77 inatueleza kwamba Mbunge yeyote atasimama na kutoa taarifa isizidi dakika mbili, lakini tumeshuhudia Mawaziri wakitoa taarifa kwa dakika tano, na dakika hizo zinazo kwenda kupunguza muda wa Wabunge kutoa mawazo yao na namna ya kuishauri Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako ni kwa nini kitendo hiki kinaendelea kwa Mawaziri, kuendelea kutumia fursa ya Kanuni ya 77 ya Taarifa, halafu wanachangia badala ya kutoa taarifa ndani ya muda ambao umepangwa kwa mujibu wa Kanuni. Nakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, amesimama Mheshimiwa Kunti akiomba Mwongozo wa Spika akitumia kifungu cha Kanuni 76 na aki-*refer* pia Namba 77 na hoja alizojenga ni kwamba; Je, inaruhusiwa Wabunge kuchangia kwa zaidi ya dakika mbili na akim-*site* Mheshimiwa Waziri.

Waheshimiwa Wabunge, nitautoa baadaye mwongozo ili kurudi kwenye *Hansard* kupima hoja aliyoisema halafu baadaye tutaweze kuitolea mwongozo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tumefika kwenye tamati ya *session* yetu ya asubuhi Saa Tatu mpaka Saa Saba Mchana, Bunge litarejea hapa Saa Kumi Jioni na watakaoanza kuchangia ni pamoja na Mheshimiwa Josephine Genzabuke, Mheshimiwa George Malima, Mheshimiwa Ally Kassinge na Mheshimiwa Joseph Mkundi hao ndiyo watakaoanza kuchangia kwa Jioni.

Waheshimiwa Wabunge, ninaahirisha shughuli za Bunge mpaka Jioni Saa Kumi.

*(Saa 7.05 Mchana Bunge Lilisitishwa hadi Saa 10.00 Jioni)*

*(Saa 10.00 Jioni Bunge Lilirudia)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae. Katibu!

**NDG. PAMELA PALLANGYO - KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Oofisi ya Waziri Mkuu kwa mwaka wa fedha 2022/2023**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na uchangiaji Ofisi ya Waziri Mkuu. Niliwataja Mheshimiwa Josephine Genzabuke, Mheshimiwa George Malima, Mheshimiwa Ally Kassinge na Mheshimiwa Joseph Mkundi kwa ajili ya kujiandaa. Sasa namwita Mheshimiwa Josephine Genzabuke ili aweze kuchangia. *(Makofi)*

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia hoja iliyopo mbele yetu. Kwanza kabisa napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu mwenye wingi wa Rehema kwa kunijalia afya ya kuweza kusimama ndani ya Bunge lako Tukufu ili kuchangia hoja ya Waziri Mkuu. Nianze kwa kuunga mkono hoja ya Waziri Mkuu kwa asilimia 100. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda niipongeze Serikali ya Chama Cha Mapinduzi inayoongozwa na Mama yetu, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Makamu wa Rais, Waziri Mkuu na viongozi wote waliopo Serikalini kwa jinsi wanavyofanya kazi na kupita maeneo mbalimbali wakihamasisha shughuli za maendeleo. Nitakuwa mwizi wa fadhila nisipoishukuru Serikali ya CCM. Unapopata kidogo ni lazima ushukuru. Ninaishukuru sana Serikali ya CCM kwa kuweza kuendelea kuufungua Mkoa wetu wa Kigoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya kutoka Kabingo – Kibondo mpaka Buhigwe yenye urefu wa kilometa 260 inaendelea kujengwa. Sasa, niiombe tu Serikali iongeze fedha ili barabara hiyo ikamilike mapema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze mama yetu mpendwa kwa kutupatia fedha ya *COVID*-19 kwa ajili ya ujenzi wa madarasa nchi nzima na kila jimbo; tunamshukuru sana mama yetu. Mwaka huu hakuna mtoto ambaye amemaliza *form IV* na anatakiwa kwenda shuleni ambaye amebakia nyumbani, wote wameweza kwenda shule. Wapo wengine ambao walisafiri kwenda maeneo mbalimbali kabla ya matokeo kutoka. Niwaomba wazazi wao wawahamasishe watoto hao ili waende shule kusoma kwasababu nafasi zipo na madarasa yapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile niwaombe viongozi wa elimu waliopo kwenye majimbo na Wilaya zetu, kuhakikisha watoto wote waliochaguliwa kwenda Sekondari waweze kwenda Sekondari. Nisiishie hapo, niendelee kuipongeza Serikali kwani zahanati, vituo vya afya pamoja na hospitali za Wilaya zimejengwa na nyingine zimekarabatiwa; kwakweli tunamshukuru sana Mama yetu mpenzi kwa kazi kubwa anayoendelea kuifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nitachangia katika maeneo mawili. Eneo la kwanza ni kuhusu nishati ya umeme na eneo la pili ni kuhusu kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ipo mikoa ambayo bado haijaunganishwa kwenye *grid* ya taifa, mikoa hiyo ipo minne, ambayo ni; Mkoa wa Kigoma, Mkoa wa Kagera, Mkoa wa Katavi pamoja na Rukwa. Niiombe, kwasababu mikoa hiyo ipo pembezoni, Serikali ifanye kila namna kusudi mikoa hiyo nayo iweze kufaidi matunda ya taifa kwa kuunganishwa kwenye *grid* ya taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mkoa wa Kigoma zipo njia mbili. Njia ya kwanza ni *grid* ya taifa kutoka Tabora kuja Kigoma kwa *KV* 132. Ninaomba, mradi huu ambao tayari umeanzishwa ukamilike, kwasababu mpaka sasa hivi mradi ule unasuasua. Kwa hiyo, nilikuwa ninaomba *TANESCO* waongezewe bajeti ili iweze kukamilisha mradi huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upo pia mradi wa kutoka Nyakanazi – Kigoma nao tena unatakiwa kukamilika kwasababu mwanzo Serikali walisema kwamba ungeweza kukamilika 2022. Kwa hiyo tunaomba juhudi ziongezeke ili miradi hiyo ikamilike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, umeme ukishapatikana Mkoa wa Kigoma utafunguka. Hii ni kwasababu Mkoa wa Kigoma ni lango kuu la uchumi, ni Mkoa ambao umepakana na nchi za *DRC*, Burudi na hata wakati mwingine Zambia. Kwa hiyo basi umeme ukishapatikana wawekezaji watakuja kujenga viwanda Kigoma, na kwasababu watu wa nchi hizo zinazotuzunguka wanachukua bidhaa kutoka Kigoma; kwa hiyo hawatakwenda mbali, watachukulia bidhaa kutoka katika Mkoa wetu wa Kigoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Kigoma tuna Bonde la Lwiche. Kama umeme ukipatikana tunaweza kufanya kilimo cha umwagiliaji;

kusaidia juhudi za Serikali za kuhamasisha kilimo; kwasababu tutaweza kusukuma mitambo ya kumwagilia mashamba yetu kwasababu umeme utakuwa wa uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru Serikali kwa kuweka mpango wa kuhakikisha mbolea ipatikane kwa bei rahisi, kama mbolea ikipatikana kwa bei rahisi wananchi wetu wataweza kuzalisha kwa wingi zaidi wakiwemo na wanawake. Mimi ni mama, ninawakilisha wanawake. Ni kwamba, wanawake wa taifa hili ni wazalishaji wakubwa, ni wakulima wazuri sana. Kwahiyo, wakipata mbolea wataweza kuzalisha kwa wingi, watapata chakula na kuongeza kipato kutokana na uzalishaji wa mazao watakayokuwa wamelima.

Mheshimiwa Mwenyekiti,niendelee kumshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa sababu amefanya kazi kubwa ya kuhamasisha kilimo cha Mchikichi Mkoani Kigoma, tunamshukuru sana, kazi aliyoifanya inaanza kuonekana, michikichi baadhi inaanza kutoa matunda. Kwa hiyo tunaomba Serikali iendelee kutuangalia Mkoa wa Kigoma katika zao letu la Michikichi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wameweza kuendelea kuelewa maana ya…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE: …**Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru…

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE: …**naunga Mkono hoja (Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Josephine Genzabuke kwa mchango wako. Mheshimiwa George Malima.

**MHE. GEORGE N. MALIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja hii ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Lakini kabla sijachangia na mimi naomba kushiriki kumshukuru sana Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi nzuri sana ambayo amenza kuifanya tangu alipoingia madarakani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi wa Mpwapwa, kama unavyojua Mpwapwa ina majimbo mawili, tumepata madarasa mengi, madarasa takriban 103. Madarasa 20 ya shule za msingi na madarasa 83 shule za sekondari, ni kitu ambacho hakijawahi kutokea, kwa hiyo tunamshukuru

sana. Lakini pia kwa ujumla wetu kwenye haya majimbo mawili, ya Kibakwe na Mpwapwa, tumepata vituo vya afya vitatu, shule za sekondari zinazojengwa na nguvu ya Serikali ni tatu, na pia barabara zote za vijijini zimefunguka. Napenda nimshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa ajili ya kufanya kazi hii nzuri. Naamini majimbo yote yamenufaika na fedha hii ambayo Mama Mheshimiwa Rais wetu ametoa

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia nimshukru Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa ajili ya uongozi wake mzuri sana hapa Bungeni. Mtu mnyenyekevu, ambaye ameongoza Bunge hili kwa kipindi kirefu akisimamia mambo ya Serikali katika Bunge hili, nampongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ningependa nianze kuchangia mambo matatu. Kwanza naomba nizungumzie habari ya barabara. Sera ya Serikali ni kuunganisha miji yote ya mikoa na wilaya kwa barabara za lami, lakini bahati mbaya sana katika Jimbo letu la Mpwapwa na Kibakwe sisi barabara haijaunganishwa kwa lami. Tuna kipande kinachotoka njia panda ya Kongwa kuelekea Mpwapwa Mjini, lakini pia kutoka Mpwapwa Mjini mpaka Chipogolo. Barabara hiyo ni kati ya ahadi za Mheshimiwa Rais Marehemu Magufuli, aliahidi kwamba ingejengwa katika kiwango la lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mji wa Mpwapwa ni mji mkongwe lakini umedumaa sana kimaendeleo kwasababu ya tatizo la barabara hii. Hakuna mwekezaji ambaye anaweza kuthubutu kuja kuwekeza Mpwapwa kwasababu ya barabara mbaya. Na kutokuwa na wawekezaji wa kutosha katika mji wa Mpwapwa kiuchumi hatuwezi kukua. Kama mnavyojua uwekezaji ndio unazalisha ajira nyingi sana kwa vijana wetu, kwa hiyo suala la ajira kwa vijana wa Mpwapwa, kama ile barabara haitawekwa lami, itabaki kuwa historia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba sana barabara hii Serikali mwaka huu wa fedha 2022/2023 basi tukumbuke, kutokee muujiza tupate barabara ya lami. Waheshimiwa Wabunge walionitangulia wote wamepiga kelele; tangu uhuru kipande hiki hakijawekwa lami, ni kama kilometa 40. Kwahiyo wananchi wa Mpwapwa wanaendelea kuteseka na hali ngumu ya uchumi kwasababu hawana *interaction* na watu. Ukiwa hauna barabara watu hawawezi kufika kwako.hata katika maisha ya kawaida nyumbani kwako kama hakuna njia safi ya watu kupita kuja kukusalimia hawatafika, kwa hiyo hautakuwa na *interaction* na watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo lingine ambalo ningependa kuzungumza ni madaraja. Pale Mpwapwa tuna madaraja matatu ambayo yana umuhimu mkubwa sana, yote yanaunganisha majimbo yote mawili. Kuna daraja la Godegode, daraja la Gulwe na Daraja moja la *TANESCO,* lipo mjini. Mheshimiwa Waziri Simbachawene anashindwa kwenda kule kwenye Jimbo lake kwasababu madaraja yote yamevunjika. Ukipita njia hii ya Godegode daraja limevunjika, ukipita njia hii ya Gulwe daraja limevunjika.

Sasa utasikia watu wanamtafuta hawamuoni, lakini atapita wapi? Kwa hiyo ninaomba sana madaraja haya pia yaangaliwe kwa karibu sana *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo lingine nizungumzie sekta ya kilimo. Wengi tumezungumza; katika Wilaya ya Mpwapwa wilaya nzima ina maeneo mengi mazuri sana kwa ajili ya Kilimo cha umwagiliaji. Kwa mfano Kata za Chunyu, Mlembule, Lumuma, Mbuga pamoja na Nduga ni maeneo ambayo yana maji; lakini shida tunayoipata kule hata kilimo kile kinachofanywa na wakulima wetu pale hakina tija kwasababu hakuna miundombinu. Mimi ningeshauri Serikali; kwamba tukitaka ku-*emphasize* kilimo lazima tuangalie sana kilimo cha umwagiliaji, kilimo ambacho hakitegemei mvua za msimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano mwaka huu mvua hapa Dodoma haijamalizia, kwa hiyo mazao mengi yanakauka sasa. Lakini tungekuwa tunamwagilia maana yake tungekuwa na uhakika wa chakula. Kwa hiyo ninaomba sana Serikali iwatengenezee hawa watu miundombinu barabara zimefunguka lakini wakipata Kilimo wakalima kwa mfano kule tulilima vitunguu sana, vitunguu vile vinaweza kusafirishwa kutoka kwenye maeneo yao kwenda kwenye masoko, kwenda Dar es salaam ama kuja Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa sasa hivi wanalima kidogo sana. Tumesema ajira kubwa katika nchi hii inapatokana kutokana na kilimo, asilimia 65 ya ajira inapatikana kutokana na kilimo, lakini je, ni asilimia ngapi ya hizi ajira? Hawa watu walioajiriwa na kilimo ni asilimia ngapi wanapata tija halisi inayotakiwa na Kilimo? Utakuta asilimia kubwa ni watu wanaolima kilimo cha kujikimu tu, hawapati mazao yanayotakiwa kwasababu ya ukweli kwamba miundombinu ya umwagiliaji haipo; na mimi ningependa sana Wizara ya Kilimo ijikite sana kwenye miundombinu ya umwagiliaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tatizo la mazingira pale Mpwapwa Mjini. Mji wa Mpwapwa umepitiwa na korongo kubwa sana. Lile korongo limeleta athari nyingi kwa miaka mingi sasa. Maisha ya watu yamepotea na nyumba zimechukuliwa. Hata mwaka huu nilimletea picha za athari zilizotokea Mheshimiwa Waziri wa Mazingira. Tunaomba sana Serikali iangalie namna ya kutatua hilo tatizo la mazingira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya naona kengele ya pili imegongwa naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Malima kwa msisitizo wa barabara na madaraja ambayo yanakwenda mpaka kwa Mheshimiwa Simbachawene. Sasa namwita Mheshimiwa Ally Kassinge wakati huo Mheshimiwa Joseph Mkundi, Mheshimiwa Josephat Kandege pamoja na Mheshimiwa Oran Njeza anajiandaa.

**MHE. ALLY M. KASSINGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nami nianze kuchangia hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kuipongeza Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Mama Samia kwa juhudi ambazo imeendelea kuzitekeleza kiasi kwamba Watanzania wanashuhudia kwa macho na wenye kusikia wanasikia shughuli mbalimbali ambazo zinatekelezwa, ikiwa ni pamoja na utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge lako hili la 12 katika Mkutano wake wa nne liliazimia kwamba sekta ya kilimo ni sekta ambayo inatakiwa ipewe kipaumbele namba moja katika mpango huu wa tatu wa maendeleo. Na nitumie fursa hii kuipongeza sana Serikali kupitia Wizara ya Kilimo kwa kile ambacho imeanza kukifanya, kitu ambacho kinaleta matarajio makubwa sana kwa Watanzania hususan wakulima ambao ndio wazalishaji wa mazao yetu ya kilimo, kwa maana ya mazao ya biashara lakini pia mazao ya chakula katika nchi yetu ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozungumzia sekta ya kilimo kabla hatujawagusa wenyewe wakulima tutakuwa tunatwanga maji kwenye kinu. Ni lazima tunapozungumzia kilimo tubainishe maeneo ambayo kweli yatamsaidia mkulima mmoja mmoja na pia kwa vikundi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini katika kilimo kuna suala la ushirika ambalo kimsingi ndilo eneo pekee litakalomsaidia Mkulima. Niishukuru sana hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu katika ukurasa wake wa 29 na 30 amegusia kidogo ushirika na pale ambapo mambo hayakwenda vema Serikali imechukua hatua, na ninaomba ninukuu sehemu ya hotuba hii.

*"Hatua mbalimbali za kisheria zimechukuliwa dhidi ya wote waliohusika na ukiukwaji wa taratibu za uendeshaji wa vyama vya ushirikia ikiwemo vitendo vya wizi wa mali na fedha za ushirika"*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hongera kwa Serikali kwa hatua hii. Lakini wakati hatua hizi zinachukuliwa kwa masikitiko makubwa nielezee kilio cha wakulima wa Nanjilinji katika Jimbo langu la Kilwa Kusini wanaotokana na Chama cha Msingi cha Nanjilinji 'A' ambao kwa msimu wa kilimo uliopita wa 2021/2022 wamedhulumiwa mazao yao, mpaka tunazungumza katika Bunge hili wakulima hawa bado hawajalipwa mazao yao. Wmezalisha kiasi cha zaidi ya tani 40 lakini hawajalipwa mpaka leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbaya zaidi kumekuwa na matumizi mabaya ya nafasi za watu ikiwemo viongozi wa chama cha msingi wakishirikiana na viongozi wa ushirika au watendaji wa Idara ya Ushirika Wilayani; ambapo wameandikia hati hewa watu ambao hawahusiki katika kulipwa mazao haya. Mbaya zaidi hizi hati hewa ambazo zimekwenda kwenye malipo hewa zinawagusa viongozi na watendaji wa Serikali, na mpaka sasa

tunavyozungumza wakuliwa hawa wapatao 40 wameendelea kulalamika na hawajasaidiwa mpaka leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayo heshima kutoa taarifa hii, na wakulima hawa walipwe fedha zao za msimu uliopita mara moja ili waweze kujikimu na kuanza tena shughuli za Kilimo kwa msimu ujao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikitoka kwenye sekta ya kilimo nije katika sekta ya afya. Niendelee kuipongeza Serikali ya Awamu ya Sita ya Mama Samia, wote tumeshuhudia namna ambavyo Vituo vya Afya vimeboreshwa, katika baadhi ya maeneo, kadhalika zahanati zimeboreshwa, lakini katika wilaya mpya hospitali za wilaya zimeendelea kujengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo hili nipongeze, katika Jimbo langu la Kilwa Kusini kuna Hospitali yetu ya Wilaya, ipo Kilwa Kivinje, inaitwa Kinyonga. tumepata Shilingi milioni 300, fedha kwaajili ya jengo la *emergence,* na kwakweli ujenzi unaendelea vizuri; tunaendelea kuipongeza na kuishukuru Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini katika eneo hili niiombe Serikali, kwamba Hospitali hii ya Wilaya ya Kilwa Kinyonga ni Hospitali chakavu, ni ya tangu miaka ya sitini na kwa maana hiyo miundombinu yake si ya kuridhisha. Wakati tunaendelea kuboresha miundombinu katika maeneo mengine katika mpango huu niombe kabisa kwamba ifikirie kutenga fedha za kutosha kwaajili ya ukarabati na uboreshaji wa miundombinu katika Hospitali ya Wilaya ya Kinyonga pale Kilwa Kivinje.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ningeweza kupongeza ni mwendelezo wa ujenzi wa barabara nchi nzima; na hapa kwa upekee wake kabisa nipongeze kwa barabara ile ya mwendokasi inayojengwa kutoka Mbagala Rangi Tatu Dar es Salaam kuelekea mjini. Barabara hii itakuwa ni ufumbuzi na utatuzi wa kero kwa wakazi wa Mbagala ambao sisi watu wa kusini wengi ndio tunaishi maeneo haya. Kwa hiyo, tunaipongeza sana Serikali kwa eneo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini katika eneo hili nisikitike tu kwamba, kuna usumbufu mkubwa ambao unafanywa na mamlaka ya Serikali za Mitaa kwa jina Halmashauri ya Manispaa ya Temeke. Halmashauri hii imelazimisha abiria wanaotoka Kilwa Kivinje na Kilwa Masoko kutumia stendi inayoitwa Biansi kinyume na utaratibu wa kutumia stendi ya mabasi ya kusini iliyopo pale Rangi Tatu, maarufu kama stendi ya mjini. Huu ni utaratibu ambao unaleta usumbufu usio na lazima. Niiombe Serikali iingilie kati jambo ili abiria waendao Kilwa na maeneo mengine ya Mikoa ya Kusini ya Lindi, Mtwara na Ruvuma watumie Stendi ya Mkoa iliyopo pale Mbagala Rangi Tatu na si stendi za pembezoni, ambazo zinaleta usumbufu mkubwa kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho niendelee kuipongeza Serikali kwa kuleta miradi ya kuboresha miji yetu, manispaa na majiji yetu, kama vile mradi wa *TSCP* umeboresha miundombinu ya miji nchini, mradi wa *ULGSP* umeboresha miundombinu ya miji, mradi wa *DMDP* Dar es Salaam inapendeza sasa hivi na sasa hivi tupo katika mradi wa *TACTIC*. Rai yangu katika mradi huu wa *TACTIC* na miradi mingine ya kuboresha miji, itakayoendelea, kuwe na *uniformity* katika nchi, ili isije ikawa unaenda katika miji mingine imedorora haipendezi na miji mingine inapendeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii kutoa mapendekezo, kwamba katika mpango huu wa tatu wa maendeleo miji mingine iliyopo ndani ya nchi yetu ya Tanzania ikumbukwe katika miradi hii ikiwemo Mangaka, Ifakara, Chalinze, Mafinga, Kilwa Masoko, Kilwa Kivinje, Tarime, Mpanda na mingineyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya ushauri huu naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Ally Kasinge kwa mchango wako. Sasa namuita Mheshimiwa Joseph Mkundi wakati huo Mheshimiwa Josephat Kandege anajiandaa.

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa fursa hii nitumie nafasi hii. Kwanza kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kutupa nafasi hii kuweza kujadili mambo mbalimbali yanayotugusa na yanayogusa jamii yetu. Nimshukuru sana pia Mheshimiwa Rais na kumpongeza kwa kazi kubwa sana anayoifanya kwa ajili ya kuleta maendeleo kwenye taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Mkuu na timu yake yote kwa hotuba nzuri iliyowasilishwa ambayo kwa ujumla wake inaota muelekeo wa nini kimefanyika nini kinapaswa kifanyike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nafasi hii nitachangia kwenye maeneo machache. La kwanza, mwaka 2020 Mheshimiwa Waziri Mkuu alifanya ziara pale Ukerewe; haya ni yanayohusu jimbo langu. Tukiwa kwenye Kisiwa cha Ilugwa tuliwasilisha ombi letu kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kutambua changamoto za afya zilizo kwenye eneo lile, tukaomba tusaidie Serikali iweze kutujengea kituo cha afya kwenye Kisiwa cha Ilugwa. Nitumie nafasi hii kuishukuru sana Serikali, kwa hatua ya awali tumepata Milioni 250 na kituo kile kimeanza kujengwa kwa hiyo, tunashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vile vile tuliwasilisha ombi la kusaidia kupandisha hadhi ya Hospitali yetu ya Wilaya ya Nansi pamoja na ile ya Kisiwa cha Ukara. Ombi lile Mheshimiwa Waziri Mkuu alilichukua ,na nashukuru vilevile Serikali imeweza kulifanyia kazi; na hatua iliyopo sasa kwa

ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Nansio tayari mkandarasi amepatikana na Serikali imetupa pesa takriban bilioni tatu, jambo ambalo litasaidia sana kusaidia wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niiombe tu Serikali itusaidie, kwamba maadamu wakandarasi wamepatikana basi mkataba usainiwe haraka na kazi ifanyike kwa mapema ili ianze kutoa huduma kwa wananchi ambao wanaathirika sana na jiografia ya eneo lile kuweza kupata huduma kwenye maeneo ya Mwanza Mjini na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tulimueleza Mheshimiwa Waziri Mkuu alivyokuja pale. Aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Hayati Dkt. Magufuli mwaka 2018 tulimueleza tatizo la barabara kilometa 14 kutoka Lugezi kwenda Nansio Mjini, na akatoa maelekezo barabara ile ijengwe kwa haraka. Alipokuja Mheshimiwa Waziri Mkuu tulimueleza jambo hili akasema atalichukua ili iweze kufanyiwa kazi kwa haraka. Niombe sana Serikali itusaidie kilometa 14 hizi ziweze kujengwa kwa kiwango cha lami zinazotuunganisha kati ya Bunda na Nansio ili kuweza kuboresha uchumi wa watu wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kupitia Ilani ya Uchaguzi, Ilani ilielekeza, na wakati Mheshimiwa Waziri Mkuu anakuja Ukerewe tuliwaahidi wananchi wetu kwamba tutafanikisha upatikanaji wa vivuko, kivuko cha kutoka Bwiro kwenda Bukondo na vilevile kutoka Rugezi kwenda Kisolya. Niashukuru kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ukurasa wa 47 Serikali imedhamiria mwaka huu kulifanyia kazi jambo hili. Lakini niombe tu, pamoja na haya bado kuna maeneo mengine ambayo yanahitaji msaada wa haraka sana. Usafiri wa kutoka Bukindo kwenda Ilugwa pamoja na kutoka Kakukuru kwenda Kisiwa cha Gana ni muhimu sana ukafanyiwa kazi haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu kwenye hotuba ya Waziri Mkuu ni kwenye maeneo mawili sana sana. Kwanza eneo la Afya. Tukiangalia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ukurasa wa 51 inaonesha namna gani Serikali yetu imefanya kazi kubwa sanaya kujenga vituo vya afya. awamu ya tano vimejengwa vituo zaidi ya 300, awamu ya sita mpaka sasa vimejengwa zaidi ya vituo 200, kwa hiyo utakuta kwamba tuna vituo karibu 600. Lakini bado kuna zahanati nyingi zimejengwa; na kwa sera yetu tuliyonayo tunatakiwa tujenge kituo cha afya kila kata, zahanati kila kijiji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilikuwa nina wazo mbadala. Kwamba, badala ya kuendelea kujenga vituo vya afya na zahanati ilhali hizi ambazo tayari zimejengwa hazitoi huduma zile tulizozitarajia kwa wananchi wetu ninaona kama litakuwa si jambo jema sana. Ushauri wangu, ningeshauri kwamba maadam tayari tumejenga vituo hivi zaidi ya 500 tuna zahanati nyingi lakini bado hakuna watumishi, hakuna vifaa tiba na kadhalika, angalau tungeweka *pending* kwa mwaka mmoja ili ile pesa ambayo

tungeendelea kujenga vituo hivi vya afya tuweze kuboresha vituo hivi ambavo tayari tumejenga ili vipate vifaa tiba kwa mfano *x-ray machines, ultra-sound,* darubini na kadhalika. Pia vipate watumishi wa kutosha ili wananchi wetu waliopo kwenye maeneo haya waweze kupata huduma, na baada ya hapo sasa tufanye tathimini nini kinatakiwa tena kiweze kujengwa kama ni kuendelea basi yale maeneo ambayo ni *strategic area* yaweze kuendelea kujengewa vituo vya afya wakati huo haya ambayo tayari yamekwisha pata vituo, vituo hivi viwekwe katika mazingira ambayo yanaweza kusaidia watu wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini eneo lingine ambalo nilitamani kuchangia nii kwenye eneo la elimu. Nimshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa pesa zile za UVIKO *1.3 trillion* angalau kwenye maeneo ya sekondari imesaidia. Sasa niombe, kwamba kilichofanyika kwenye eneo la sekondari kifanyike vilevile kwenye eneo la *primary* kwa kuwa kuna shida kubwa sana kwa sababu hakuna madarasa hakuna nyumba za walimu ikifanyika kwa namna hiyo *one time investment* inaweza kusaidia sana kuondoa changamoto zilizopo vilevile kwenye eneo la shule za msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mkundi kwa mchango wako. Mheshimiwa Josephat Kandege sasa aanze kuchangia.

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa na mimi niweze kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kunijalia na mimi nisimame ili kuweza kuchangia katika hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niungane na Wabunge wenzangu waliompongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi njema, kazi iliyotukuka pamoja na Serikali yake yote kwa ujumla, hakika Mwenyezi Mungu anaiona kazi iliyo njema ataendelea kuibariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijielekeze katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu hususani ukurasa wa 28 ambao unaongolea kilimo. Baada ya kuchagua eneo hilo, nimepitia eneo hilo ninakuta Serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu wametaja mazao ya mafuta ikiwepo alizeti pamoja na michikichi, lakini kwa bahati mbaya sana nilitarajia na zao la soya lingekuwa miongoni mwa mazao ambayo Serikali inatambua na kujua kwamba tunatakiwa kupata mafuta kutoka katika zao hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikafanya *study* nikapitia taasisi moja inayoitwa *the International Institute of Tropical Agriculture* kutaka kujua zao hili la soya likoje. Nimegundua yafuatayo; katika Afrika nchi ambayo

inazalisha zao hili kwa wingi ni Nigeria, kama ambavyo Mheshimiwa Anna Kilango Malecela aligundua kwamba Nigeria pia wanazalisha zao la Tangawizi kwa wingi, hali kadhalika kwenye soya wapo. Lakini *study* inaonesha kwamba baada ya Nigeria wanakuja Afrika ya Kusini wanafuata Zambia pamoja na Malawi, Tanzania hatumo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nipongeze kazi njema sana ambayo imefanywa na balozi wetu aliyepo nchini China Mheshimiwa Balozi Kairuki kwa kusaini mkataba kati ya Tanzania na China kuweza kuuza zao hili ambalo ni zao jema sana kwa uchumi wa taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikafanya utafiti nini faida inayotokana na zao hili. Yafuatayo nimeyabaini; katika zao hili unaambiwa kwamba asilimia 36 ya protini inapatikana kutoka katika zao la soya lakini asilimia 30 tunapata *carbohydrate* lakini pia wanasema *excellent amount of dietary fiber vitamin and mineral.* Pia ina- *consist twenty percent* ya *oil,* kwa maana ya mafuta ya kula na hivyo wana-*recommend* kwamba ni kati ya mazao ambayo yanatakiwa yapigiwe mfano kwa nguvu zote sisi Waafrika kuhakikisha kwamba tunalima ili tuondokane na tatizo kubwa la mafuta. *(Mafuta)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kama haitoshi, zao hili wanasema baada ya kukamua mafuta ile keki yake ambayo inabaki ni chakula kizuri sana kwa ajili ya mifugo, na ninaamini katika mpango mzima wa Serikali wa kuanza kufuga kisasa tutatumia zao hili katika kufuga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini *soya bean is the only available crop that provides inexpensive and high-quality source of protein comparable to meet poultry and eggs;* lakini kama haitoshi wanasema garama yake ni ndogo ukilinganisha na mazao ya nyama pamoja na mayai. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaambiwa kwamba ukilima soya ina uwezo wa kunyonya *nitrogen* kutoka hewani na kurutubisha ardhi. Kwa hiyo, kwa ajili ya matumizi sahihi ya ardhi yetu ambayo imechoka ni vizuri sasa kama Serikali tukahakikisha kwamba tuna *encourage* kilimo hiki kwani pale ambapo tunahitaji mbolea za viwandani tukishalima soya hatutakuwa na haja ya kutumia mbolea za viwandani ambazo sisi sote ni mashuhuda jinsi ambavyo mbolea hii imekuwa ikipatikana kwa bei kubwa na wakati mwingine hata upatikanaji wake unakuwa si wa uhakika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema hayo na kwa utafiti ambao nimefanya na kwa kulima mimi mwenyewe niitake Serikali, *this is high time* ya kuhakikisha kwamba mikoa ile ambayo inahangaika na kilimo cha mazao ya jamii ya mikunde ikiwepo Manyara ambao wamekuwa wakilima mbaazi wanakosa kwa kupeleka, ni wakati muafaka sasa twende kulima soya. Kama haitoshi, wakoloni walitaka reli iende Nachingwea kwa sababu ilionekana ndiyo sehemu ambayo soya inakubali mawazo mazuri haya *its*

*high time* kama Serikali tuhakikishe kwamba tunalima kilimo hiki kwa sababu soko la uhakika lipo lisilotiliwa mashaka hata kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu miongoni mwa mikoa maskini ni pamoja na Mkoa wa Rukwa, ni matumaini yangu makubwa kwamba Serikali itaielekeza nguvu yake kubwa katika kilimo cha soya ili wananchi ambao wamekuwa wakilima mahindi kwa kiasi kikubwa lakini wanaendelea kuwa kwenye lindi la umaskini wanatoka kwenye umaskini.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya uwepo wa *protein,* ni jambo la kusikitisha sana ukiambiwa kwamba akina mama na watoto ambao wanakufa kwa sababu ya kukosekana na virutubisho ikiwemo *protein* wanapatikana katika Mkoa wa Rukwa. Naamini, haya matatizo ambayo yanapatikana ndani ya Mkoa wa Rukwa na kwingine katika Tanzania hali ipo hivyo hivyo. Ni matumaini yangu makubwa sana kwamba Serikali itaenda kufanyia kazi kubwa ili tuhakikishe zao hili linaenda kufanya mapinduzi katika taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nikielekea kuhitimisha naomba niulize Serikari maswali yafuatayo na wanijibu. La kwanza, kwa nini Mkoa wa Rukwa pamoja na kuwa mzalishaji mkubwa wa chakula ikiwepo mahindi lakini imekuwa ni mkoa maskini kuliko mikoa yote Tanzania? Swali la pili, kwanini vifo vya mama na mtoto ndani ya Mkoa wa Rukwa vimekuwa vingi ukilinganisha na mikoa mingine? Swali la tatu, kwa nini katika mradi wa *Agro-connect* ambao unaitaja Mikoa ya Iringa, Njombe, Ruvuma, Mbeya, Songwe na Katavi imeruka Mkoa wa Rukwa? Swali la nne, kwa nini mpango wa kuunganisha Mkoa wa Rukwa na *grid* ya taifa, ilikuwa ikisemwa zamani, sasa hivi hatujui mpango huu umeishia wapi? Swali la tano, kwa nini Mkoa wa Rukwa umekuwa ukifanya vibaya katika ufaulu wa watoto wanaomaliza darasa la saba kwenda kidato cha kwanza? Kwa nini Mkoa wa Rukwa umekuwa na upungufu mkubwa sana wa watumishi ukilinganisha na mikoa yote Tanzania? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja naomba Serikali inijie na majibu ya maswali yangu yote. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Josephat Kandege. Nilimwita Mheshimiwa Oran Njeza wakati huo ajiandae Mheshimiwa Michael Kembaki, Mheshimiwa Sylvia Sigula, Mheshimiwa Deus Sangu, Mheshimiwa Joseph Kakunda.

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana na mimi kupewa fursa hii ya kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwanza kwa kumshukuru na kumpongeza sana Mheshimwia Rais kwa matokeo mazuri sana ya utekelezaji ambayo imepelekea ni nchi pekee katika Afrika Mashariki ambayo ilikuwa na

ukuaji ambao ni chanya. Tulikuwa na ukuaji ambao nchi nyingine zote ukuaji wake ulikuwa na *negative GDP.* Kwa hiyo ningependa sana kumshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa hilo lakini pia na Serikali nzima akiwemo Makamu wa Rais na Waziri Mkuu. Kazi iliyofanyika ni kubwa mno ni nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo yote mazuri lakini sasa hivi tunashuhudia dunia nzima inaingia kwenye changamoto kubwa za uchumi, na huo mdororo wa uchumi umeshaanza kuonekana hapa kwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipokuwa najaribu kuangalia wenzetu hili suala wamelionaje na wamelichukuliaje na sisi Tanzania kama sehemu ya dunia je, tujiweke wapi?

Kwakweli kwa kiasi kikubwa ukiangalia mashirika makubwa ya fedha ikiwemo *IMF* pamoja na *J. P. Morgan* wameonesha ya kwamba pamoja na hizo changamoto lakini kwa nchi kama Tanzania hii ni fursa. Kwa hiyo badala ya kuangalia zile changamoto zilizopo zinazotokana na hii hali sisi sasa tungejipanga kuangalia fursa ambazo zipo kutokana kwanza na athari za *UVIKO* na pia na athari zinazotokana na vita ya Urusi pamoja na Ukraine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuanzia hatua za haraka, nina imani Serikali kupitia Ibara 140 ya katiba yetu na Sheria ya Bajeti Ibara ya 35 mpaka 39 ilichukua hatua hizo ambazo zimeitaka Serikali kuwa na mfuko wa dharura *(contingence fund)*. Kwa hiyo katika hali ya namna hii ninategemea kwamba Serikali itatumia mfuko huo kuchukua hatua za haraka ili tuweze kunusuru hali ya mfumuko wa bei. Lakini siyo mfumuko wa bei tu, vile vile kutakuwa na mfumuko wa mahitaji ya pesa za kigeni ambayo yanaweza kutuweka katika hali ngumu zaidi. Sasa tufanye nini ili tuweze kuondokana na hilo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wewe mwenyewe unajua, kuwa mikopo yetu mingi tunalipa kwa pesa za kigeni. Kama kutakuwa na mfumuko na mahitaji makubwa ya pesa za kigeni, nchi yetu ifanye nini? Nina imani ya kwamba hatuwezi kuahirisha kulipa madeni lakini tutahitaji pesa za kigeni nyingi. Uchumi wetu unategemea kilimo. Nawashukuru sana Wabunge wameongea kwa kiasi kikubwa umuhimu wa kilimo kwa Tanzania. Lakini nchi yetu ina madini, nchi yetu ina utalii, nchi yetu ina bandari. Hivyo vitu vitatu vikipelekewa msukumo na Serikali ikajikita katika hivyo vitu vitatu vinne nina imani tutavuka salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye kilimo unachohitaji ni kuwa na kilimo chenye tija, huhitaji zaidi ya hapo. Kilimo chenye tija. Kwa mfano leo kilimo chetu heka moja ya mahindi tunazalisha tani moja wakati kawaida kabisa heka moja ya mahindi inatakiwa izalishe tani nne. Kwa hiyo tukianzia na hiyo tuu, ina maana tutakuwa tumejipeleka mahali pazuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini namshukuru sana Mheshimiwa Rais kupitia Wizara ya Kilimo anavyofanya mageuzi *(transformation)* kwenye kilimo, nafikiri katika hiyo na motisha walizopata wakulima nina imani ya kwamba kupitia kilimo hili tutaliweza. Kwa hiyo tunahitaji pesa za kigeni kupitia hata nafaka. Nimesema hii ni fursa kwa sababu Ukraine na Russia ndio walikuwa tunaingiza kwa kiasi kikubwa ngano. Lakini nchi za jirani walikuwa wanaingiza mpaka mahindi wanaagiza kutoka Russia. Sasa mahindi yetu yatapata soko kubwa na bei zimeshaanza kuwa nzuri. Kwa hiyo tukijikita kwenye kilimo cha mahindi nina imani kuwa tutaenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye madini tuna fursa kubwa lakini kuna wawekezaji ambao wanahitaji kuwekeza kwenye madini bado wanazungushwa, hawapewi kipaumbele. Mfano mmoja wapo kwa muda mrefu nimesimama hapa Bungeni; tuna madini yanaitwa *Niobium*. Kuna wawekezaji toka miaka ya 2015 mpaka leo wanashindwa kupata leseni. Mpaka *financial institution* wameamua waachane na huu mradi. Wawekezaji nao wanataka kuachana na huu mradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi ombi langu, kwa ajili ya hii hali miradi mingine kama hiyo tuichukue kwa dharura. Tukikosa pesa za kigeni inawezekana tukakosa hata chakula. Hii mbolea tunayoisema tunahitaji pesa za kigeni. Pesa za kigeni tutazipata wapi? Pesa za kigeni hatuwezi kuzipata kwenye kuondoa tuu ruzuku. Pesa za kigeni zitapatikana kwenye uzalishaji wetu kwenye kilimo, madini na utalii. Kwa hiyo ningeomba kwa kiasi kikubwa Serikali ichukue hatua za makusudi. Hii hali tuliyonayo sasa hivi ya uchumi wa dunia ni hali ambayo inaweza kutupeleka mahali pabaya sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vile vile tunahitaji kuboresha miundombinu. Kwa sababu miundombinu nayo inaweza kutuletea *inflation*. Sasa kwa kiasi kikubwa...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Oran Njeza kwa mchango wako.

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana naunga mkono hoja. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Michael Kembaki.

**MHE. MICHAEL M. KEMBAKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia katika mada hii. Kwanza ningeanza kumshukuru Rais wetu, Mama yetu, Mama Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri ambayo anaifanya katika kulijenga taifa letu la Tanzania. Kazi kubwa imefanyika katika Jimbo letu na katika nchi nzima amefanya kazi kubwa ambayo imetukuka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeanza kwa kusema katika Jimbo letu la Tarime Mjini kuna jambo ambalo haliko vizuri ambalo ningependa kulisemea kabla ya kuchangia mchango wangu. Katika Mji wetu wa Tarime kumetokea tatizo pale Mgogoro wa Bugosi na Jeshi la Wananchi wa Tanzania. Mgogoro ule umepelekea ng'ombe wanafuga pale wanakamatwa, na wale ambao wanachunga wanapigishwa mazoezi kweli kweli. Mmoja wao aliniambia siku hizi amenunua buti ili akitoa ng'ombe nje aweze kufanya mazoezi, ameshaanza kuwa mwanajeshi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wale wananchi wanaishi pale na walipaswa walipwe fidia waondoke ili waweze kuendelea na shughuli zao. Sasa kama mtu anaishi pale, anafuga mifugo yake lakini mifugo haipaswi kutoka nje kwa sababu itakamatwa; na pale ambapo inakamatwa wanalipishwa faini siyo chini ya shilingi laki tano. Ningeomba Serikali ione namna gani ya kutatua tatizo hili kwa kuwalipa fidia wananchi wale ili waondoke katika eneo lile ili Jeshi liendelee na sehemu yao kama kawaida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vile vile imetolewa pesa ya kujenga barabara na Halmashauri yetu imepokea zaidi ya shilingi milioni 450 kwa ajili ya kujenga barabara. Tayari wakandarasi wamesaini mkataba na mpaka sasa barabara zile hazijaanza kujengwa. Ningeomba Serikali sasa iingilie kati ili hao wakandarasi ambao wana-*sign* mikataba alafu hawaingii *site* kujenga barabara wachukuliwe hatua ili barabara zile, kwa nia njema ya Serikali ya kutaka barabara zijengwe basi hiyo dhamira itimie kwa kuwabana hawa wakandarasi waweze kujenga barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kuelekeza mchango wangu mwingine upande wa kuajiri wafanyakazi. Taswira ya taasisi ama kampuni yoyote ni wafanyakazi wake. Wafanyakazi namna wanavyofanya kazi, lugha wanayoitumia, namna wanavyojitoa katika kufanya kazi lakini pia namna wanavyojitoa kuhudumia wateja wao inaonesha taswira kamili ya taasisi husika. Na ndipo watu wanaweza kusema kwamba taasisi hii ni nzuri au taasisi hii ina tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa sisi Watanzania tujiulize, kwamba watumishi wa Serikali na watumishi wanaoajiriwa na Serikali wakoje? Hali ikoje katika taasisi za kiserikali? Katika hospitali watumishi hawa wakoje? Shuleni na Katika taasisi zingine kama *TANESCO* watumishi hawa wakoje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lugha zinazotumika katika taasisi hizo za Serikali ikiwemo hospitali haziridhishi; na hii inasababishwa na nini? Hebu turudi nyuma namna watu wanavyoajiriwa Serikalini. Kwa mfano waliomaliza elimu mwaka 2014/2015 wamekuwa nyumbani tangu 2015 mpaka 2021 walipoajiriwa. Katika kipindi hiki chote watumishi hawa ambao wameajirwa walikuwa wanaendesha bodaboda, wengine walikuwa wafanyabiashara. Sasa wanapokuja kuajiriwa baada ya miaka sita miaka mitano unakuta

*knowledge* yake, ufahamu wake, ujuzi wake haupo tena anaenda kuanza upya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii inasababisha utendaji kazi kwa watumishi katika Serikali yetu unakuwa chini ya kiwango; lakini pia hata lugha zile ambazo wanatumia unakuta tayari wameingia wengine unakuta ni bodaboda, wengine ni machinga; kwa hiyo anapoenda pale anaanza kujifunza upya. Mimi ningependa kushauri itungwe sheria, kwamba wahitimu wote wanaotoka elimu ya juu wajitolee katika Idara za Serikali kulingana na idara waliopo. Kwa mfano, kama ni Madaktari wakirudi kwao waanze kujitolea katika hospitali, kama ni Walimu warudi kujitolea shuleni, kama ni Ma-*engineer* warudi kujitolea katika maeneo yao ili kuwasaidia ku-*gain* ujuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kujitolea kunasaidia mtu kuweza kuongeza na kukuza maarifa. Kujitolea ni tendo la huruma, ni tendo la kuonesha fadhila kwa taifa. Lakini vile vile tukitunga sheria hii, Serikali itaondokana na uhaba wa wafanyakazi uliopo katika taasisi zetu. Kwa mfano katika Mji wetu wa Tarime madaktari sita tu kati ya 15 wanaohitajika. Lakini kuna madaktari wengi ambao wako nje ambao wamehitimu elimu lakini hawana kazi. Kwa hivyo wakijitolea, Serikali kwanza itakuwa imepata nguvu kazi itakayosaidia kulijenga taifa letu pamojan na kupunguza matatizo wanayokabiliana nayo kwenye upungufu wa watumishi katika idara mbali mbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia vijana wengi wanaohitimu elimu ya juu unakuta wametumia gharama ya Serikali kama mikopo lakini hawapati nafasi ya kurudisha ile mikopo kwa sababu hakuna ajira. Wakijitolea ninaamini watakuwa wamelipa fadhila kwa kodi ya wananchi wameitumia wakati wanasoma… *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante! Ahsante sana Mheshimiwa Michael Kendaki.

**MHE: MICHAEL M. KENDAKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Sasa namuita Mheshimiwa Sylvia Sigula wakati huo Mheshimiwa Deus Sangu, Mheshimiwa Joseph Kakunda, Mheshimiwa Frolent Kyombo wanajiandaa.

**MHE. SYLVIA F. SIGULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia katika Hotuba ya Waziri Mkuu. Kwanza na mimi niungane na wenzangu kumpongea Rais wetu mpenda Mama yetu Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayoifanya ya kutuletea maendeleo Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimepitia Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu inayohusiana na vijana, ajira na watu wenye ulemavu; na mimi ningependa sana nijikite kwenye ajira. Changamoto kubwa ya vijana ni ajira na sisi wawakilishi wa vijana ajenda yetu namba moja ni suala la ajira kwa vijana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wazi kabisa kuwa hatuwezi kutatua matatizo au kero ya ajira kwa kutegemea asilimia nne za mikopo ya halmashauri, haiwezekani. Kwa hiyo Wizara hii imepewa jukumu kubwa la kusimamia ajira za vijana. Nilitarajia kuona tuna mpango maalum wa namna gani tunakabiliana na hii changamoto ya ajira kwa vijana *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma ukurasa wa 62 wa Hotuba ya Waziri Mkuu, anasema kwamba asilimia 87.8 ya vijana wana ajira; ajira rasmi na ajira zisizo rasmi, *either* wamejiajiri au wameajiriwa. Sasa utaona kama asilimia 87 wana ajira na waswahili wanasema *no research no right to speak* nadhani wataalam wataelewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka kuzungumzia nini hapa? Unaposema asilimia 87 wana ajira ninaamini kabisa ajira ambazo zinakuwa nyingi hapa ni ajira zisizo rasmi. Unapozungumzia ajira zisizo rasmi ziko nyingi, kuna ajira nyingi bodaboda, kuna mama ntilie, kuna baba ntilie, kuna mmachinga na wafanyabiashara wengine wadogo, hawa wanaingia kwenye ajira zisizo rasmi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nina ushauri kwa Serikali. Kwamba, tunapotaka kukabiliana na hii changamoto ya ukosefu wa ajira kwa vijana natamani sana kuona tunawekeza nguvu kubwa katika ajira zisizo rasmi kwa sababu ndizo zinazoajiri watu wengi. Ninaonge haya na nitatoa *reference* kwa kutumia bodaboda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bodaboda ambazo tumeingiza nchini kuanzia 2017 mpaka leo 2022 ni bodaboa Milioni 1,279,455 na tumeweza kuipatia Serikali zaidi ya bilioni 117. Hapa nataka kuzungumza nini, ukifanya takwimu ya vijana ambao wamejiari kwenye bodaboda kwa Mkoa wa Dar es Saalam tu wako vijana 136,431. Ukija Mkoa wa Mwanza wako vijana 86,218. Ukija Mkoa wa Dodoma wako vijana 58,316. Ukija Mkoa wa Kigoma wako vijana 36,411. Sasa, unapofanya rafli ya hawa vijana wa bodaboda nchi nzima ni zaidi ya 2,090 na kuendelea huko. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama sekta hii inaweza ikaajiri vijana wengi namna hii, naona ni muda mwafaka sasa wa Serikali kuweka kipaumbele katika sekta hii. Sekta hii ya bodaboda imeachwa, imeachwa vijana hawanufaiki wanateseka lakini imeachwa Serikali pia haipati mapato kupitia bodaboda. Na hapa nataka nielezee kitu gani? Unapozungumzia vijana milioni 2,092 ambao wamejiajiri kupitia bodaboda hawa ni vijana mchanganyiko; wako vijana ambao wana elimu na ambao hawana elimu.

Hapa kinachotokea kitu gani? Changamoto yao kubwa ni suala la leseni. Ili kijana apate leseni anahitaji kuwa na 83,000. Hali mtaani ni ngumu vijana wanalia, ajira hakuna, abiria hakuna, hiyo 83,000 anaipata wapi huyu kijana? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kukosa hiyo 83,000 lakini anapokuwa hana hiyo 83,000 hana leseni lakini hajapaki yuko barabarani. Nini kinatokea hapa? Badala ya Serikali kukusanya mapato kupitia hizo leseni Serikali haipati mapato na kijana anaishia kutoa elfu tano tano, elfu mbili mbili kwa Askari ili aendelee kuwa barabarani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu kwa Serikali *is either* tupunguze hii bei ya leseni ni kubwa sana, tunaweza kufanya leseni ikawa 40,000 na Serikali ikapata mapato kuliko hivi tunavyofanya sisi, kuwaachia wenyewe wajifanyie. Au tunaweza tukatengeneza mfumo hawa vijana wakalipia leseni kwa *installment* na Serikali ingeweza kupata mapato mengi na vijana wangeweza kunufaika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma *Tax Administration Act* inamtambua mlipa kodi. Unapokuwa na biashara inayoingiza zaidi ya milioni nne unatakiwa usajiliwe kama mlipa kodi. Lakini wapo watu wanafanya biashara hizi za bodaboda, ana bodaboda tatu mpaka nne; lakini kwa sababu Serikali imeacha wazi hawa watu hawalipi kodi na Serikali inazidi kupoteza mapato na vijana wengi wanaendelea kunyanyasika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ustawi wa taifa letu ukisoma ukurasa wa 55 unatambua kabisa kwamba vijana ndio nguvu kazi ya taifa hili kwa asilimi 55. Sasa kama vijana ni nguvu kazi, embu tuwasaidie kuwaokoa na hali wanayopitia. Bodaboda kwa sababu wameachwa wazi tunapata majeruhi wengi Serikali inaingia gharama kuwatibu lakini inaendelea kupoteza nguvu kazi ya taifa. Kwa kuwa tumeshindwa kusimamia suala la bodaboda Serikali inapoteza mapato na bodaboda wanazidi kuteseka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, natambua Serikali imetoa bilioni tano kwa ajili ya machinga lakini tunatoa bilioni tano kwa ajili ya miundombinu. Je, tunashindwa kuwapatia mikopo hiyo miundombinu tunayoianzisha ni nani atakayeenda kuitumia kama vijana hawa hawana mikopo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusidanganyane hapa hatuwezi kuhamasisha vijana wajiari kama hatutawapatia mikopo. Vijana wanahitaji mitaji ili waweze kujiari. (*Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia sasa hivi ukiangalia hospitali nyingi zina wodi maalum kwa ajili ya majeruhi wa bodaboda. Mimi niiombe Ofisi ya Waziri Mkuu isimamie sekta hizi. Bado Wizara ya Mambo ya Ndani haijafanya kazi yake vizuri zaidi ya kutengeneza ugomvi kati ya bodaboda na Askari. Lakini pia kuna haja ya Wizara ya Uchukuzi kusimamia jambo hili ili

kutengeneza kwa sababu hata bodaboda hii iko sehemu ya uchukuzi. Uchukuzi siyo ndege tu na meli… *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana

**MHE. SYLVIA F. SIGULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana kwa mchango wako Mheshimiwa Sylivia Sigula. Sasa namwita Mheshimiwa Deo Sangu aweze kuchangia.

**MHE. DEUS C. SANGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa fursa hii ili na mimi niweze kutoa mchango wangu katika hoja iliyo mezani, hoja ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Kwanza nichukuwe nafasi hii kuipongeza Serikali; mimi binafsi katika jimbo langu kwa mara ya kwanza tumeweza kupata fedha nyingi za maendeleo ambazo zinafikia takribani bilioni tisa. Ni rekodi kubwa, na mimi pongezi zangu za dhati za wanakwela zimfikie Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi hizo nitoe tu ahadi kama Mbunge na Baraza langu la Madiwani tutasimama kidete kuwahakikisha fedha hizi zinafanya kazi iliyokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pili naomba nitoe mchango wangu, na nitaanza kuchangia katika sekta ya bandari. Bandari ni *key driver* ya uchumi ndani ya nchi. Sisi kama Tanzania tuna bahati, upande wa Mashariki wa nchi tuna Bahari ya Hindi ambapo tuna bandari, upande wa Magharibi ya nchi tuna Ziwa Tanganyika ambako ndiko kunapatikana Mikoa ya Kigoma, Katavi na Rukwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kumekuwa na sintofahamu ya muda mrefu. Hapa ameongea ndugu yangu Mheshimiwa Kandege, kwamba kati ya mikoa inayotajwatajwa kuwa na umaskini na hali duni ya maisha ni mikoa ya Rukwa, Katavi Kigoma na sisi tuna Ziwa Tanganyika ambalo tunapakana na nchi ambazo zina fursa ya kufanya biashara na nchi yetu kupitia ile mikoa mitatu. Kule tuna Burundi, *DRC* na Zambia

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe tutaarifa. Juzi tu hapa kuna ugunduzi umefanyika *wa copper* ndani ya nchi ya *DRC* kule Katanga kuna *deposit* ya *copper* ambayo wanaweza wakafanya uchimbaji kwa miaka 100 ijayo. Sasa fursa pekee ambayo tunayo, wao wanategemea kusafirisha *raw materials* katika *extraction* ile ya *copper* ambayo ni *sulphur* ambayo wanaipitishia Bandari ya Dar es salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na kwa taarifa tu ile biashara ya *sulphur* ambayo wanapitisha Bandari ya Dar es salaam imeweza ku-*trigger* namba

za mapato ndani ya mapato ndani ya Bandari ya Dar es salaam. Yale mapato waliyokuwa wanaweza kuyafanya kwa mwaka mzima kwa mwaka huu kwa mara ya kwanza wataweza kufikia ndani ya kota mbili kwa maana ya miezi sita. Ni *achievement* kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa shida ambayo imekuwa ni kikwazo biashara hii tusifanye vizuri na *DRC* ni mzunguko. Wakichukuwa mzigo huo Bandari ya Dar es salaam wanalazimika wapitishe Zambia ndipo waende Lubumbashi. Mzunguko mrefu sana ilhali sisi tuna *short cut* ya kupitia *either* Kasanga, Kalema ama Kigoma kwenda upande wa pili wa *DRC*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa sisi mpaka tunavyoongea mwaka wa tatu tuna bajeti kwamba tunanunua meli. Ziwa Tanganyika hatuna meli, tangu Liemba iondoke kwenye matengenezo, tangu MV Mwongozo iondoke hatuna meli. Sasa, tutaweza ku-*utilize opportunity* hii ya *DRC,* iliyokuja, kwa namna gani? Wataanza kufikiria kutukimbia, wataenda Bandari ya Walvis Namibia au Beila kule Mozambique au wataamua kwenda *Durban South* Afrika. Sasa naomba, Mheshimiwa Waziri Mkuu tumewekeza kwenye Bandari zetu za Kasanga, Kalema pamoja na Bandari ya Kabwe. Sasa zile bandari kazi yake ni nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna jambo hili ambalo hatuwezi pia pamoja kwamba bandari zitakamilika, upande wa pili wa kule *DRC* miundombinu ya barabara ni shida. Kutoka pale Moba upande wa pili kwenda kufika Lubumbashi ni kilometa 700, kilometa hizo hazipitiki. Kwa hiyo kama nchi lazima pia tufanye mazungumzo ya pamoja na nchi ya *DRC* kama wenzetu wa Uganda walivyofanya, tukaingia hata katika ubia wa kutengeneza barabara ili tuwende ku-*utilise opportunity* iliyoko ndani ya nchi ya *DRC*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe sana Serikali, mikoa yetu hii itafunguka; leo hii bodi ya mazao mchanganyiko mmeanzisha ghala kule Lubumbashi, mahindi yetu yataendaje? Ina maana tutapitisha Zambia ndipo tukauze kwenye soko la *DRC*? Haiwezekani, hatuwezi tukategemea boti za watu binafsi kama nchi kusafirisha mizigo yetu ambayo inaenda ku-*trigger* uchumi wa mikoa mitatu kwa pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe tena, Mheshimiwa Waziri Mkuu, jambo ambalo mimi nimekuwa nikipata shida wakati huu, kumekuwa *misconception* ya kuchanganya kana kwamba Mkoa wa Rukwa na Katavi ni mkoa mmoja. Tayari mikoa hii imeshakuwa tofauti. Katavi wanajitegemea na Rukwa inajitegemea. Leo hii kuna mradi huu ambao tumepata *fund* kutoka kwenye *European union agri-connectivity* kwa ajili kutengeneza miundombinu ya barabara ku-*support productivity* kwenye kilimo. Mikoa yote ya Nyanda za Juu Kusini ipo, ikiwemo Katavi, lakini Rukwa wameturuka, sisi Wana-Rukwa tuna shida gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwa hiyo niombe sana, tunapokuwa tunaangalia kwa upana namna ya kuweza, leo hii tumeongelea hapa, nimemsikia ndugu yangu hapa anaongelea habari ya uwanja wa ndege wa Sumbawanga. Ule uwanja wa ndege wa Sumbawanga ni miaka sita sasa, kila bajeti ipo; na nilivyokuwa namwona Mheshimiwa Waziri anajibu hapa nikatikisa kichwa, kwamba na mwaka huu wananchi tunaenda kuwaambia kwamba imo kwenye bajeti tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuwaambie kama inashindikana mwaka huu kutekeleza ni bora tuiondoe kwenye bajeti ili tujuwe kwamba mwaka huu hatuna uwanja wa Sumbawanga. Niendelee kusihi sana asubuhi tulikuwa na jambo la mbolea limeongelewa na Mheshimiwa Waziri amejibu sana. Kama hatutafufua kampuni yetu ya mbolea Tanzania *TFC* tusitegemee kwamba suala la mbolea tutapata suluhu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeongea habari ya ruzuku, ni sawa, lakini mnapowapa nguvu *private operator* kwenye suala la mbolea ambayo ni *sensitive* kwa usalama wa chakula cha nchi ni shida. Hili shirika letu ambalo liko taabani tangia mwaka 2014 limekufa; na hili shirika si la juzi, limeanzishwa mwaka 1968 kwa dhumuni la kusaidia usalama wa upatikanaji wa mbolea ndani ya nchi; lakini tulilitwishwa mzigo wa madeni limekufa halipo kabisa. Kwa hiyo inatakiwa Serikali tuchukuwe hatua ya haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba tumeahidi kwenda kuweka ruzuku ili tupate mbalea nchini, nawasihi sana tuifufue Kampuni ya Mbolea Tanzania ili itusadie Watanzania wakulima maskini ambapo mwaka huu mbolea ni kilio cha nchi. Ukifika kule kwetu tumeenda mpaka 140,000 kwa mfuko mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana kwa nafasi hii. Haya yalikuwa ya kwanga niliyotaka kuchangia katika Ofisi ya Waziri Mkuu ahsante sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI**: Ahsante. Nilikuita Mheshimiwa Florent Kyombo ajiandae Mheshimiwa Neema Mwandabila Mheshimiwa Suma Fyandomo na hatimaye Mheshimiwa Joseph Kakunda.

**MHE. FLORENT L. KYOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa nafasi hii ya kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Na mimi niungane na wenzangu ili kuipongeza Serikali kwa nzuri inayofanyika, na hasa mimi nitajikita katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ukurasa wa 13 na 51 ambao unaongelea suala la afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nishukuru sana kwamba Serikali imeendelea kuboresha miundombinu kwa kufanya ukarabati, lakini pia kujenga

miundombinu mipya ya afya, na hasa tumeona Hospitali za Rufaa za Kanda, za Mikao, Halmashauri Vituo vya Afya na Zahanati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kupongeza tena Serikali tumeona fedha zilizotokana na mkopo wa 1.3 *trillion,* bilioni 466 zote zilielekezwa Wizara ya Afya ili zikanunue dawa na Vifaa Tiba na wananchi wetu waendelee kupata matibabu ambayo ni bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo hili kwenye fedha hizo zinazopelekwa Wizara ya Afya asilimia 60 na 70 ni fedha ambazo zinanunua dawa, na dawa hizo zinatakiwa zisambazwe katika vituo vyote vya kutolea huduma dhamana hiyo imepewa *MSD*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi leo nitajikita katika utendaji kazi wa Shirika letu la *MSD;* na ninaomba kabla sijaongelea sana *MSD* niwape chimbuko kidogo la *MSD*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiangalia Sera ya Afya ya Juni mwaka 2007, naomba kunukuu, kwamba; "Dawa na vifaatiba ni bidhaa muhimu katika kutoa huduma za afya zilizo bora, bidhaa hizo zinahitajika utaalam na umakini mkubwa wakati wa kuagiza, kutunza na kusambaza".

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nasimama mbele yako nikisitika sana, Shirika letu la *MSD* halina mtaalam hata mmoja wa kusimamia haya ambayo yameainishwa katika Sera ya Afya. Ukiangalia katika watumishi 700 walioko ndani ya *MSD* ni asilimia 6 tu ya wataalam wa dawa walioko pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ukiangalia katika kanda zetu 10 zote ambazo *MSD* inasimamia kusambaza dawa kule hakuna mtaalam wa dawa. Serikali imesomesha wataalam wa dawa kwa gharama kubwa sana, na nikisema katika *rank* ya gharama ya kusomesha wataalam tunaanza na *doctor of medicine* tunaenda na *doctor of medicine and surgeon* tunaingia *pharmacist,* ni taaluma ambazo zinasomeshwa miaka mitano na *internship* mwaka mmoja**.** *Pharmacy* inasomwa miaka minne na *internship* mwaka mmoja, ni gharama kubwa kwa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunao *professor pharmacist's* wako 13, leo tunao *PhD holders pharmacist* wako 20, leo tunao *Masters holder*s 167 ambapo kati ya hao wamesomeshwa *procument na supply chain management system;* lakini masikitiko yangu ni kwamba ukienda pale *MSD* leo idara ambayo ni mahususi kwa ajili ya kufanya makadirio ya dawa Tanzania inaongozwa na mtu wa manunuzi tu sifa kubwa ni mwanajeshi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba Serikali mniambie hivi dawa zimegeuka kuwa bunduki au risasi? Ni kitu gani ambacho kinafanya wataalam waachwe pembeni halafu waende kuchukua mtu wa kawaida? Inasikitisha sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na leo tunatarajia matokeo makubwa kutoka *MSD*, haiwezi kutokea; sisi wote kwa imani zetu kila mmoja anaomba afike peponi, pale Mwenyezi Mungu atakapomchukuwa, lakini lazima ufe kwanza. Leo tukitaka *MSD* ifanikiwe lazima tuhakikishe tunabadilisha tunarudi kwenye Sera ya Afya ambayo ilisema inahitaji mtalaam na umakini mkubwa, wataalam wakabidhiwe ile taasisi iweze kuendeshwa. Tofauti na hapo tutakuja kuona *billions of money* zinapelekwa *MSD* zinazama leo nikisimama hapa nikirudi miaka 3 nyuma *MSD* dawa zilizo-*expier* ni bilioni 26 kwa sababu gani hakuna mtaalam**.**

Mheshimiwa Mwenyekiti,

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikuambie mimi bahati nzuri ni mfamasia dawa zinatengenezwa katika ma-*group* nikikuambia group la *fetharisporincy* kuna dawa kama 100 leo ukiniletea dawa ya *cephalexin* na *cephoxine* zote ni *fetharisporincy* lakini kama sina moja kwenye stoo nitakuambia hii *cephalexin* itakufaa, lakini wenzetu kwa sababu hakuna wataalam akiambiwa dawa A kama haipo ni *out of stock,* wanarudi nyumbani kule dawa iliyopo nyingine ina-*expire*. Leo tunapoteza bilioni 26 ambayo ni sawa na zahanati tunazopeleka milioni 50 522.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vituo vya afya vya milioni 500 ni vituo 52 hapa tunaangalia miaka mitatu miaka mitano hadi 10 ijayo ni nini; Mheshimiwa Rais ameliona hili. Wakati anapokea taarifa ya *CAG* alisema *MSD* inatakiwa ifanyiwe *overall,* ifanye maboresho makubwa, na tumsaidie kumshauri kwamba kilichotokea na kinachosababisha *MSD* isifanikiwe ni kwa sababu wameacha utalaam wamepeleka watu wa *interest* ambazo hazijulikani ninaomba Serikali kabidhi taasisi hizi za wataala…

**MHE. TABASAM H. MWAGAO**: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. FLORENT L. KYOMBO: …** ili wataalam hawa weze kufanya kazi ya kitaalam na matokeo makubwa yaweze kuonekana…

**MHE. TABASAM H. MWAGAO**: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa!

**MHE. FLORENT L. KYOMBO: …**lakini kila siku wananchi wataendelea kuachana dawa hazipo na dawa zina-expire…

**MWENYEKITI:** Hakuna Mbunge atakayesimama kuzungumza kabla hajarusiwa endelelea Mheshimiwa Florent.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO**: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa!

**MHE. FLORENT L. KYOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kushukuru kwa kulinda muda

**MHE. TABASAM H. MWAGAO**: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa

**MHE. FLORENT L. KYOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, leo taasisi ambazo zinafanya vizuri kwa sababu ya kusimamiwa na watalaam wake…

**MHE. TABASAM H. MWAGAO**: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa!

**MWENYEKITI:** Haya Mheshimiwa Tabasamu!

**T A A R I F A**

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hawezi kusema ni mtu wa kawaida yule mwanajeshi aliyeko pale ni Daktari Bingwa na aombe radhi namuomba Mheshimiwa Mbunge aombe radhi katika jambo hilo hansard iwe sawa *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kyombo unaipokea taarifa!

**MHE. FLORENT L. KYOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshimu sana kaka yangu Tabasam taaluma ninayoiongelea naongelea *pharmacists*. Nikienda kwenye mifumo ya ufamasia nikakuambia *pharmacokinetics* ya dawa nitakuambia…

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa

**MHE. FLORENT L. KYOMBO:** …nitakuambia *procurement and management supply chain* kwakweli naheshimu taaluma nyingine zote. Na nilikua naenda huko kuhitimisha…

**MHE. JULIANA D. MASABURI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa!

**MHE. FLORENT L. KYOMBO:** …Kwa hiyo mimi ninaposema vile nasema mtu ambaye ame-*specialize* kwenye dawa, si kwenye matibabu daktari ana…

**MHE. JULIANA D. MASABURI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa

**MHE. FLORENT L. KYOMBO:** …ndicho kitu ninachoamaanisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mimi naomba tuishauri vizuri Serikali, tusilete ushabiki, ili twende vizuri Mheshimiwa Rais wetu ikli naye aweze kupumzika kutafuta fedha nyingine kwa ajili ya miradi…

**MHE. JULIANA D. MASABURI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa!

**MHE. FLORENT L. KYOMBO:** … kwamba pale tusiweke watu ambao wanaweza wakakaa na dawa, wakasimamia dawa, wakambaza dawa na zikafika kwa wananchi.

**MHE. JULIANA D. MASABURI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa!

**MHE. FLORENT L. KYOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba nikupe mifano mizuri ya taasisi ambazo zinasimamiwa ambazo zinasimamiwa na taaluma za *pharmancy* ambazo…

**MHE. JULIANA D. MASABURI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa!

**MHE. FLORENT L. KYOMBO:** … zimefanya vizuri tunayo *TMDA,* mamlaka ya chakula…

**MHE. JULIANA D. MASABURI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Spika kaniamba

**MHE. FLORENT L. KYOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mamlaka ya dawa na vifaatiba inafanya vizuri ndani ya nchi na nje ya nchi

**MHE. JULIANA D. MASABURI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa!

**MHE. FLORENT L. KYOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na inatoa gawio hata kwa Serikali.

**MWENYEKITI:** Taarifa Mheshimiwa Masabuli!

**T A A R I F A**

**MHE. JULIANA D. MASABURI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Mbunge anayeongea kwanza afute ile kauli ya kusema yule si mtaalam, ni mtu wa manunuzi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Hiyo taarifa au nikufuta kauli?

**MHE. JULIANA D. MASABURI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, afute kanuni ili

**MWENYEKITI:** Kanuni namba ngapi?

**MHE. JULIANA D. MASABURI:** Mheshimiwa Mwenyekiti ili hansard zikae vizuri…

**MWENYEKITI:** Unasimama kanuni namba ngapi Mheshimiwa Mbunge?

**MHE. JULIANA D. MASABURI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni taarifa.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Kyomba endelea *(Makofi)*

**MHE. FLORENT L. KYOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushuru, tukisikiliza vizuri hoja yangu nimesema mtaalam wa dawa, na nchi hii hakuna mtaalam wa dawa, sijasema *medical doctor,* nimesema mtaalam wa dawa. Naomba tujikite kwenye hoja ili kusaidia nchi hii ili wananchi wetu wawe wanapata dawa na shughuli zote ziweze kwenda kwa mujibu wa taratibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti,

**MBUGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa

**MWENYEKITI:** Taarifa wapi ahh Mheshimwa wa Ulinzi

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante!

**MHE. FLORENT L. KYOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ulinde muda wangu

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa. Taarifa nyingi zimetolewa lakini na mimi nilitaka kuongeza sauti kwamba hatuwezi kusema Mwanajeshi ni mtu wa kawaida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili imeshaelezwa kwamba yeye pamoja na kwamba ni Mwanajeshi ni *professional* yake pia ni udaktari, tatu *Chief Executive Officer* wa taasisi yeyote si lazima awe na taaluma ya fani hiyo, anaweza kufanya kazi akiwa na taaluma nyingine yoyote ilimradi ana wataalam wa kufanya naye kazi kwa hiyo naomba ieleweke kwamba si sahihi kabisa… *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Taarifa ya Waziri wa Ulinzi ni taarifa

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, jenerali kwamba ni mtu wa kawaida. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Unapokea taarifa amesimama kwa kupitia kifungu namba 77 taarifa.

**MHE. FLORENT L. KYOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sijui ambapo sieleweki ni wapi namheshimu sana Waziri wangu mpendwa lakini suala nililosema….

**MWENYEKITI:** Unapokea taarifa au haupokei?

**MHE. FLORENT L. KYOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea.

**MWENYEKITI:** Ahsante, endelea

**MHE. FLORENT L. KYOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninachomaanisha nasema ni mtaalam wa dawa na sijapinga kuwepo kwa brigedia pale, nimesema asilimia sita tu ya wataalam walioko *MSD* ndio wataalam wa dawa, lakini asilimia iliyobaki yote ni watu wasaidizi ni wanasheria ni wahasibu, nikasema katika kanda 10 hakuna mtaalam wa dawa kule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huo ndio mchango wangu. Kwa hiyo naishauri Serikali iweze kuboresha taasisi yetu ya *MSD* ifanya vizuri iwatumie wataalam iliyowasomesha kwa bei kubwa…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. FLORENT L. KYOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, naunga mkono hoja ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Florent Kyombo, Waheshimiwa Wabunge niwakumbushe, kuwa ukisimama kutoa taarifa si sheria, kiti kikuruhusu kuzungumza. Ikimpendeza Spika utapewa nafasi. Kwa hiyo taarifa kama sijakupa nimekusikia, lakini hapa nina-*manage* vitu vingi. Nilitaka nitoe kwanza huo utaratibu ili tuweze kwenda pamoja. *(Makofi)*

Tunaendelea, nilimwita Mheshimiwa Neema Mwandabila sasa wakati anajiandaa Mheshimiwa Suma Fyandomo na Mheshimiwa Daktari Florence Samizi.

**MHE. NEEMA G. MWANDABILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia hotuba hii ya Waziri Mkuu. Niipongeze Ofisi ya Waziri Mkuu na wataalam wake wote na mawaziri wote na viongozi wote ambao wako katika Wizara hii ambayo imekuwa ikiendelea kufanya kazi pamoja na Waziri Mkuu. Na niseme tu tunafarijika na namna wanavyokuwa wakiendelea kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kutoa hoja ambayo nimedhamiria sana kuna mambo ambayo nilitamani niyabainishe, ambayo ningetamani Ofisi hii ya Waziri Mkuu waweze kuona na kuyapa kipaumbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ni kuhusu masuala ya utekelezaji wa miradi. Kumekuwa na uibuaji wa miradi mingi ambayo imekuwa ikiendelea

kutelezeka, lakini mingi unakuta miradi imedolola na imekaa muda mrefu bila kumalizika. Nitatoa mfano wa mradi mmoja ambao tulipitia, Mradi wa Hospitali ya Wilaya ya Mbalali ambao ulianza tangu 2011 na mpaka leo haujaisha. Nilitamani Ofisi ya Waziri Mkuu wawe na mkakati wa kuwa na *timeframe* kwa kila mradi unaoanzishwa, kwamba ndani ya muda fulani mradi huu unakamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kitu kingine ambacho nimekiona na ningetamani kukichangia hapa ni katika masuala ya ardhi. Kumekuwa na tabia ya watu kubadilisha matumizi ya ardhi bila utaratibu, na unakuta Serikali inapoteza mapato mengi katika maeneo haya. Unakuta mtu aliomba kibali cha kupata eneo kama makazi badaye anakwenda kufanya biashara na wakati huo huo yeye anakuwa anaingiza pesa nyingi Serikali aipati chochote. Kwa hiyo, nilitamani pia Ofisi ya Waziri Mkuu iliangalie hili pia na kufanyia mkakati maalumu, badala ya kuendelea kutenga maeneo na kupima mapya kila siku na kugawa kuwe na uhakiki wa maeneo yalishatolewa na sisi kama taifa tuweze kunufaika kwa ubadilishaji wa maeneo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninafahamu maeneo mengi ya miji yamechangamka lakini ukienda kuhakiki unaweza ukakuta *either* pale mjini hawana hati na yale maeneo hayajapimwa; lakini unakuta wao wanaendelea kufaidika na Serikali haipati kitu chochote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine nilitamani kuongelea ni suala la *TAZARA*. Tunafahamu upo ukakasi katika suala la *TAZARA,* lakini tufahamu kabisa *TAZARA* ni uchumi wa Nyanda za Juu Kusini. Watusaidie hiyo sheria ambayo haifanyiwi marekebisho kwa kushirikiana na wenzetu wa upande wa Zambia walichukuwe kwa haraka. Katika hotuba hii sijaona kitu chochote kinachozungumziwa kuhusu *TAZARA*. *TAZARA* ni muhimu, *TAZARA* bado iko vizuri, lakini inachakaa na miundombinu inachakaa kwa sababu tu hakuna uangalizi mzuri kutokana na hiyo sheria wanayosema ina ukakasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nirudi kwenye hoja halisi ambayo nilitamani kuizungumzia leo. Tunafahamu kabisa nchini hapa kuna janga la madawa ya kulevya. Tunapoongelea madawa ya kulevya mimi awali nilikuwa naona ni kitu cha kawaida sana; lakini kuna siku wabobezi wenyewe wa masuala ya madawa ya kulevya walinifafanulia, na hivyo niliona ipo haja kama taifa kuingia kwenye mapambano dhabiti ya kuahakikisha madawa ya kulevya kwetu inakuwa ni kitu cha kusimuliwa, kwamba yasiwepo kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unapoongelea madawa ya kulevya unaongelea kuhusu nguvu kazi ya taifa ambapo vijana wengi wanaharibika na wanakuwa hawawezi kufanya kazi yoyote ya kulijenga taifa kwa kujipatia kipato chao wenyewe. Lakini pia tunaliongelea maadili ya taifa. Tunafahamu vijana wengi wanaotumia madawa ya kulevya ni watu ambao

hawajali lolote na maadiliyao yanakuwa mabovu, wanakuwa vibaka, wengine ndiyo wanajiuza wengine unakuta ndio hao wanaoingia kwenye vitendo vya ushoga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia kwa upande wa Serikali tunakuwa tunapoteza pesa nyingi kwa kununua hizi dawa, na taifa linapoteza fedha kwa biashara hii haramu. Sasa, kiuchumi hili linasababisha tunaendelea kushuka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka kusema nini; tunajua kabisa *program* mbalimbali za dawa za kulevya zimekuwa zikiendelea chini ya Kamishna Jenerali wetu Kusaya na wataalamu wake. Hata hivyo, bado ziko changamoto za msingi ambazo kama taifa tunatakiwa tuwape *support* Ofisi ya Mamlaka Dawa za Kulevya ili iweze kufanya kazi vizuri. Tunafahamu kabisa pesa inayotolewa ni ndogo, lakini pia kuna kitu ambacho kimesahaulika. Wanabainika watu wa dawa za kulevya lakini hakuna *linkage* na *TAMISEMI* ambao ndiyo iliyo karibu sana na wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na ninataka kusema nini, kuna kundi la watu wa ustawi wa jamii ambao ndio wanao-*deal* na watu wote wenye changamoto za kijamii ikiwa ni pamoja na hawa wa dawa za kulevya. Kule chini hatuna watu ambao wanasimamia. Yaani katika TAMISEMI ukienda kufuata *structure* ile huwezi ukamkuta mtu ambaye yuko maalum kwa ajili ya kusimamia masuala ya kulevya katika Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na hii sasa inavyokuwa hapa unaona kwamba, mamlaka inapambana kwa namna yake lakini TAMISEMI yenye watu haina habari na hiki kitu. Kwa hiyo niseme tu mimi kwamba, ofisi hii ya mamlaka itengenezewe utaratibu wa kuwa *linked* na TAMISEMI ili waweze kuwahudumia na kuwabaini hawa watu kwa wepesi kuanzia kwenye ngazi za vijiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pamoja na kutoa hizo pesa kwa ajili ya upambanaji wa uingizaji na matumizi na kupunguza madhara ya dawa za kulevya kuna kitu ambacho kimesahaulika. Kwamba, tukumbuke wale watu wanaotumia dawa za kulevya jamii imeshawatenga; ni watu wasiokubalika katika jamii. tunafanya nini kama Serikali kuwaaminisha hawa watu tumewatibu katika vituo vyetu vya matibabu ya dawa za kulevya ili waweze kurudi kwenye jamii na kupokelewa na kuweza kushiriki katika shughuli za maendeleo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mimi niseme, kwamba ipo haja kupitia Ofisi ya Kamishna kutenga fungu maalum la fedha ambalo litasaidia katika kuwajengea uwezo au kuwapa mitaji hawa vijana. Na itengenezeke sera ambayo itaonesha kwamba hawa vijana, sasa baada ya kuacha madawa ya kulevya waingine katika utendaji kazi, hata wakawa wanarudishwa mmoja mmoja kwenye ofisi, kwa wale ambao wamesoma. Hii

itasaidia kuepukana na changamoto hii. La sivyo tutakuwa tunawatibu lakini wanaendelea kurudi kwenye matumizi ya dawa kwa sababu watakuwa wanakosa *support* ya kijamii, kiserikali katika kuacha kabisa haya masuala ya dawa za kulevya. Tutakuwa tunafanya kazi ya kuwatibu, wanarudia, kitu ambacho siyo sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Neema Mwandabila. Sasa namuita Mheshimiwa Suma Fyandomo Ikenda, wakati huo Dkt. Florence Samizi anajiandaa Pamoja na Mheshimiwa Joseph Kakunda.

**MHE. SUMA I. FYANDOMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia bajeti ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kwanza namshukuru sana Mwenyezi Mungu mwingi wa Rehema amenipa kibali nami niweze kusimama kuchangia kwenye Bunge hili Tukufu. Awali ya yote ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais Mama Samia Suluhu Hassan na Amiri Jeshi Mkuu, ambapo ametusaidia sana kwenye Hospitali ya Mkoa wa Mbeya. Kwenye hospitali ile ametupatia fedha kiasi cha shilingi bilioni tano kwa ajili ya kujenga jengo la upasuaji, lakini pia ametoa milioni 800 kwa ajili jengo la *emergence*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye jengo lile tuna upungufu. Nilikuwa naomba sana, jengo lile halina wodi ya wanawake. Ninaomba sana kwenye bajeti hii tusiache kuweka fedha kwa ajili ya kujenga jengo la wodi ya wanawake, ni matatizo. Hii ni kwa sababu wanawake wanapata tabu sana maana wakiuguwa sehemu ya kuwalaza wanawake inakuwa ni tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kuchangia suala la *TASAF*. Ninaishukuru sana Serikali kwa sababu inatoa fedha kwa ajili ya watu wasiojiweza na wazee. Ninaishukuru na kuipongeza sana na Serikali.

Mheshimiwa Mwneyekiti, hata hivyo hatujaiangalia kwa mapana. Nimejaribu kupita kwenye kaya tofautitofauti ambazo zinasaidiwa na hizi fedha za *TASAF*; unapita kwenye kaya unamkuta bibi ama babu amekaa upenuni hawezi kutafuta hata kuni hawezi kuwasha moto hawezi kufanya chochote. Fedha wanaweze wakawa wamemfikishia, lakini anaweza akaa upenuni kwakwe anavizia *either* apite kijana ambaye akimuona ampatie fedha akamsaidie akanunue sukari. Sasa inawezekana akapita kijana ambaye ni mcha Mungu, wakati huo huo anaweza akapita kijana ambaye si mcha Mungu; hiyo pesa imeondoka anabaki tu kusikitika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuishauri Serikali ninaomba sana hizi fedha TASAF ninaomba kila wilaya wafanye mpango wa kujenga *hostel* kwa ajili ya kutunza hawa wazee wetu. Itawasaidia sana hawa wazee. Naamini wakikaa kwenye *hostel* watapata huduma zote, na fedha hizi

zitakwenda moja kwa moja kwenye vituo vya hosteli ili wazee wetu waweze kupata huduma stahiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi nimeuliza swali, lakini katika kuuliza lile swali nilijibiwa. Kwenye Wizara ya Ujenzi kuna sehemu ambayo sikuielewa vizuri, sehemu yenyewe ninaomba sana tuchukulie kwa uzito. Ni kuhusu hii barabara ya kutoka Igawa mpaka Tunduma hapa ninachangia, ninaomba sana hiyo barabara mtu anapotoka Dar es Salaam, anatoka Dodoma akifika Igawa kuanza safari ya kuelekea Mbeya Mjini mpaka Tunduma moyo lazima ulipuke, moyo unafanya fya' fya' kwa sababu anakuwa hana uhakika wa kufika salama nyumbani kwake. Yaani hakuna alama za barabarani, barabara ni finyu na ina mashimo. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nikwambie hali ni mbaya sana. Mtu akitoka Mbeya Mjini anakwenda Mbalizi ni lazima aage, amuage mtu yeyote, kama mke wake hayupo ama mume wake ametoka anampigia simu, hata kama yuko Dar es Salaam amesafiri anasema natoka kidogo hapa Mbeya Mjini naenda Mbalizi. Hii ni kwa sababu ile barabara haamini kama anaweza kurudi salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini wakati huo huo hiyo barabara ya kutoka Mbalizi kuelekea Tunduma ni finy, ajali zimekuwa nyingi sana, ndugu zetu wanakufa wengi sana kwa sababu ya barabara finyu. Ninaomba tuchukulie kwa uzito. Bunge la Bajeti ya mwaka jana nilisikitishwa sana kwamba ilitengwa bajeti ya km tano za lami; km tano kutoka wapi mpaka wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachoomba hapa…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante!

**MHE. SUMA I. FYANDOMO: …**dakika moja tafadhali. Walisema kwamba wanatafuta mkandarasi; ninaomba tuchukulie *serious* sana, mkandarasi atafutwe haraka ili ile barabara ianze kujengwa Mbeya tunalia jamani, Mbeya tunateseka sana na ile barabara. Madereva wanajua lakini na sisi tunaosafiri tunajua kwa sababu mioyo yetu haikai sawasawa tunapopita zile barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, nashukuru sana.

**MWENYEKITI:** Umemaliza ee!

**MHE. SUMA I. FYANDOMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Umemaliza maana nilikuwa nimekuongeza dakika moja

**MHE. SUMA I. FYANDOMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Si unaongelea Mbeya Mjini!

**MHE. SUMA I. FYANDOMO:** Ninakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Nilikuwa nimekuongeza dakika moja kwa sababu nimeona pale bosi wangu naye anapiga makofi, na mimi napenda kibarua changu.

**MHE. SUMA I. FYANDOMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana, hata Mheshimiwa mwenyewe akifika maeneo yale lazima ashike kiti sawasawa kwamba nitafika salama, na ndiyo maana na yeye inamgusa sana ile barabara ya kutoka Igawa hadi Tunduma. Ninaomba sana; wananchi wa Mkoa wa Mbeya tuna kilio, na machozi. Naomba Serikali ichukulie kwa uzito sana, tafadhali sana sisi kule Mbeya hatuko mikono salama kwa sababu maisha ya watu wengi sana yanaathiriwa na barabara, watu wanakufa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tafadhali sana, naomba sana, ninaunga mkono hoja juu ya hili; lakini pia ninaomba kwa upande wa Serikali.

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. SUMA I. FYANDOMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante ninakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Suma Fyandomo Ikenda, ulipokuwa unahitimisha nilifikiri utagusia na barabara ya Mafinga – Mgororo na Nyororo – Mtwango, unapopita pale kila siku.

Sasa namuita Mheshimiwa Daktari Florence Samizi, wakati huo Mheshimiwa Joseph Kakunda na Mheshimiwa Mohamed Said Issa wanajiandaa.

**MHE. DKT. FLORENCE G. SAMIZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana nami kunipatia nafasi niweze kuchangia Hotuba hii ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi kwanza kabisa nianze kwa kumpongeza Rais wetu kwa jinsi ambavyo anaendelea kujali huduma za wananchi wetu. Kipekee niendelee kumpongeza kwa jinsi ambavyo nami nimefaidika sana katika Jimbo la Muhambwe. Tumepata miradi mbalimbali ambayo kwa kweli wananchi wa Muhambwe tunamshukuru sana kwa sababu tutaimarisha huduma za jamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali yetu imeendelea kuboresha huduma za afya kupitia sera ya mwaka 2007 kwa kuendelea kutoa huduma za afya kwa makundi maalum. Hii ikiwemo watoto chini ya miaka mitano, wajawazito na wazee wasiojiweza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hotuba ya Mheshimiwa Waziri mkuu kwenye ukurasa wa 13 na wa 53 imeendelea kujipambanua zaidi kuonyesha jinsi gani itaendelea kujali afya za makundi haya. Tumeendelea kufanya vizuri kwa sababu taifa lolote lenye ustawi wa afya ya jamii yake linapimwa kwa vifo vya mama na mtoto. Na kipekee nchi yetu kupitia takwimu za mwaka 2015/2016 *Demographic survey* inaonyesha kwamba tunapata vifo vya akina mama 556 katika kila vizazi 100,000 vya Watoto hai. Haya ni mafanikio makubwa sana katika jamii yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pamoja na mafanikio yote hayo tuliyokuwa nayo, sera hii ya mwaka 2007 ya kutoa huduma kwa makundi haya maalum bado inatoa mianya ya changamoto kwa makundi haya. Tumejitahidi katika hospitali zetu tumeweka madirisha ya kuyahudumia makundi haya, kama vile dirisha la kuhudumia wazee au dirisha la kuchukulia dawa kwa wazee au mabango yanayosema kwamba mzee atahudumiwa kwanza. Hata hivyo ni ukweli usiopingika kwamba madirisha haya mengi yamekuwa kama picha au anasa maana yanaandaliwa tu pale ambapo tunasikia kuna usimamizi shirikishi *(supportive supervision)*, ili viongozi wetu wakija wayaone, lakini kiuhalisia yale madirisha hayafanyi kazi inavyotakikana ndio maana yale makundi bado yanapata tabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vile sera hii ni ya muda mrefu tangu mwaka 2007 na Serikali yetu imejikita kuwa na malengo maalum yaliyozinduliwa mwezi wa sita mwaka jana, na kuonyesha jinsi gani inaendelea kuboresha huduma za afya na kipekee makundi maalum na jinsi ambayo taarifa ya Waziri Mkuu imeonyesha, basi ni muda muafaka sasa kuipitia ile sera ili iweze kuendana na hali ya sasa. Kwa maana kwamba makundi haya yaratibiwe vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na ushauri wangu katika hili, kwa vile Serikali inatoa pesa nyingi kwa ajili ya kuyahudumia makundi haya basi ni muda muafaka twende kwenye bima ya afya kwa makundi haya. Ile pesa tunayotumia kama ruzuku katika manunuzi ya dawa basi tuwakatie bima za afya ili waweze kupata huduma hizi kwa uhakika. Hii itasaidia kwanza waweze kupata dawa, lakini pili itawaondolea unyanyapaa wanaoupata wanapoenda hospitalini na kuwaambia hawa ni wale wa bure. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vile vile itawasaidia muda wote waweze kupata dawa, na pia itawapunguzia watumishi Maafisa Ustawi wa Jamii ambao wanafanya kazi ya kuratibu tu hawa wagonjwa kwa kugonga muhuri na kuwaorodhesha, ambapo hawa maafisa ustawi wa jamii wangeweza kufanya kazi zingine zenye maana zaidi kama vile kuratibu malezi ya watoto

wetu, zero mpaka miaka nane, kudhibiti ukatili wa kijinsia ili kuboresha afya zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vile vile naungana na wenzangu wote walioongea kuhusu ajira. Bado suala la ajira ni tatizo katika nchi yetu; na kipekee nitajikita kwa wale vijana wa Muhambwe ambao wanapitia changamoto kubwa ya kukosa ajira kwenye ile miradi ambayo tunayo katika Jimbo letu. Tunashukuru Mungu Jimbo letu lina mradi mkubwa wa barabara ya kutoka Kibingo mpaka Kasulu. Lakini ni ukweli usiopingika kwamba vijana wetu hawapati ajira katika miradi ile.

Mheshiimwa Mwenyekiti, Waziri Mkuu ana sera nzuri sana ya kusema vijana wapate ajira. Lakini ni nani ana ratibu hili zoezi mpaka kufika kule? Je, mkataba wa huyu mwekezaji unaonesha ni vijana wangapi watapata kazi? Ni wangapi wazawa, na ni wangapi watafanya kazi za kubeba vibendera? Inasikitisha sana pale ambapo hata mbeba kibendera ametoka kwingine. Hatumaanishi ubaguzi lakini tunaomba vijana wa Muhambwe wafikiriwe kwanza kwenye hii miradi inayotekelezeka katika Jimbo letu ili nao waweze kupata ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo la mradi mkubwa wa barabara, naiomba Serikali; kwa vile ujenzi wa barabara unaendelea na unatia matumaini kwa kasi nzuri sana, lakini miradi hii inayo miradi shikizi ya jamii, ikiwemo vituo vya afya, shule, kituo cha zimamoto ambavyo kwenye Jimbo langu vinategemea kujengwa pale Nyankwi katika Kata ya Busunzu. Tunaona ujenzi wa barabara unaendela lakini hatuoni miradi hii ikianza kujengwa. Ninafahamu mingine iko Kasulu na mingine iko Buhigwe. Tunaiomba Serikali basi, miradi hii shikizi ya barabara iende sambamba na ujenzi wa barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo machache naomba kuunga hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Daktari Samizi kwa mchango wako. Sasa namuita Mheshimiwa Joseph Kakunda aweze kutoa mchango wake.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kunipa nafasi ili nami nichangie hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Nianze kwanza kwa kuwapongeza Viongozi wetu wa Chama cha Mapinduzi na Serikali chini ya uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuongoza vizuri nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kihistoria daima tutawaenzi baba zetu 13 na Mama yetu mmoja kwa kuiongoza nchi hii vizuri tangu tupate uhuru. Baba zetu wanane wameiongoza Serikali ya Mapindu Zanzibar na baba watano na mama yetu mmoja wameongoza Jamhuri ya Muungano wa Tanzania vizuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niweke katika historia ya kumbukumbu. Daima tutamkumbuka baba wa Uhuru na Umoja wa taifa hili, Marehemu Mwalim Julius Kambarage Nyerere, tutamkumbuka baba wa mageuzi ya kiuchumi na kisiasa Mzee Ally Hassan Mwinyi, tutamkumbuka baba wa Sera za Uwazi na Ukweli Muasisi wa sera na mikakati ya kuondoa umaskini Tanzania, Mzee Benjamin William Mkapa ambaye alituachia Dira ya Maendeleo ya Taifa inayotekelezwa tangu mwaka 2000 mpaka mwaka 2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna wenzangu waliwahi kutamka hapa kwamba hatuna dira wala maono. Tunayo Dira ya Taifa ya Maendeleo ambayo tumeendelea kutekeleza kwa mipango ya miaka mitano mitano na mipango ya mwaka mmoja mmoja kama huu ambao tunajadili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile tunamkumbuka baba wa siasa za maridhiano ya Kitaifa Mzee wetu Jakaya Mrisho Kikwete na pia tunamkumbuka baba wa ujenzi wa miundombinu na umiliki wa rasilimali za Taifa Marehemu Daktari John Pombe Joseph Magufuli. Na sasa tunaye Mama yetu ambaye ameithibitishia Dunia, narudia, ameithibitishia Dunia huruma yake kwa kila mtanzania kupitia kazi zake zinazopeleka maendeleo kila pembe ya nchi, hata maeneo ambayo yalikuwa hayajawahi kuona darasa jipya sasa mwaka jana yameona darasa jipya. Wanachi wa Uswada kule Kitunda, wananchi wa Idimbwa kule Kitunda sasa wameona darasa jipya kwa sababu ya juhudi za Mama Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rais wetu kesho ataondoka nchini kwenda Marekani kwenda kuzindua filamu ambayo inatangaza utalii wa Tanzania. Nikiri wazi kwamba mwanzoni sikuelewa filamu hii itakuwa na manufaa gani, lakini baada ya kudadavua takwimu ambazo zinaweza zikaletwa na utalii utakaongezwa kupitia filamu hiyo, ninampongeza sana Rais wetu kwa kwenda kesho Marekani kuzindue hiyo filamu, na tunategemea mafuriko ya watu kuja kuiangalia nchi hii, kwenda kuangalia vivutio vya utalii katika nchi hii. Na utalii umekuwa na mchango mkubwa sana kwenye pato la Taifa, kwa hiyo siyo jambo ndogo alilolifanya Mheshimiwa Rais wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na nchi hii ina orodha ya Viongozi wa kujivunia hawastahili kubezwa hata Kiongozi mmoja, tumefanya vizuri sana. Naomba historia zao ziandikwe katika vitabu watoto na wanafunzi wasome shuleni na vyuo vikuu ili taifa hili liendelee kuuliziwa kupitia Uongozi wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mambo ya msingi ya kushauri. Jambo la kwanza ni mfumko wa bei. Yamesemwa mambo mengi sana kuhusu mfumko wa bei. Leo nilikuwa nasoma the *Washington Post* kuhusiana na *inflation* ya Marekani, linasema hivi, nanukuu "*The consumer price index is expected to come in at hooping 8.4 percent this April. America hasn't witnessed inflation levels above 80 percent since 1981.*"

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake nini? Ina maana Marekani wanalia *inflation*, Uingereza wanalia *inflation*. Na sababu za mfumko wa bei Kimataifa ziko tatu, sababu ya kwanza ni *lockdown*, sisi hatujaona *lockdown* ndiyo maana tunashangaa wenzetu Marekani na nchi nyingine walifungia watu wao ndani na hakuna kutoka, halafu wakaanza kugawa fedha za bure hazina jasho. Matokeo yake *demand* ya vitu vya matumizi ya nyumbani ikaongezeka, hasahasa *demand* ya vyakula na bidhaa za umeme. Na hiyo ndiyo imesababisha *inflation* Dunia nzima. Sisi tunahangaika na *imported inflation*. Mtawaparura bure Mawaziri hapa wakati ambapo inflation zingine zimeletwa kutoka nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu ya pili ni kufungwa kwa viwanda vya uzalishaji kulikosababisha bidhaa kupungua, hasa mbolea, na ndiyo maana bei ya mbolea bado ipo juu sana. Halafu ya tatu ambayo imegongelea msumari ni vita ya Urusi na Ukraine ambayo vimeongeza chumvi kwenye kidonda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuna haja ya kugomba kwa sababu ya *inflation* inayotuathiri kwa sasa hivi, sababu zinajulikana. Naomba tuungane na Serikali na kuhakikisha kwamba hatua ambazo zinachukuliwa na Serikali tunaziunga mkono.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina ushauri katika maeneo machache. Eneo la kwanza ni kuhusu Benki ya Kilimo *(TADB*) mwaka jana Benki Kuu ilitoa fedha Shilingi trioni moja ili zipewe Mabenki waweze kukopesha wananchi. Mojawapo ya ambayo Benki tulitegemea ipate hizo hela ni *TADB*, lakini haikupata hata senti moja kwa sababu Benki hii ya *TADB,* Benki ya Maendeleo ya Kilimo haikuwa na vigezo vya kuweza kupata hizo fedha, matokeo yake haikupata hata senti tano. Ninaomba Serikali na kuishauri Serikali yangu sikivu wekezeni kwenye *TADB* ili ipate vigezo vya kukopesheka nayo iweze kukopesha wakulima maana hii ni Benki ya wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wa pili ni muhimu sana Serikali iwe na *buffers of fund*, fedha ambazo ni maalum kwa ajili ya kununua mazao endapo soko la mawazo litakuwa si nzuri kwa wakulima wetu ili wakulima waweze kupata jasho lao vizuri, thamani ya jasho lao. Ushauri wa tatu Mfuko wa Pembejeo, naomba Mfuko wa Pembejeo usitumike kukopesha tu mikopo midogo midogo. Mfuko wa Pembejeo utumike vilevile kuweka fedha za ruzuku kwa ajili ya mahitaji muhimu kama pembejeo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wa nne, naomba Wizara ya Kilimo iangalie mazao mengine. Kwa mfano kule kwetu zao la pilipili limeanza kulimwa na watu wengi. Ninaomba msaada wa Wizara ya Kilimo ilete wataalam kuwashauri wananchi namna gani walime zao pilipili ambalo litaongeza pato kutoka kwenye pato la tumbaku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu wa tano, ninaomba Serikali itunge haraka sera ya ufuatiliaji na tathmini ili kuimarisha ufuatiliaji na tathmini. Ni ufuatiliaji na tathmini katika nchi nyingine ndio unapunguza maswali ya ukaguzi, ukaguzi wa ndani na ukaguzi wa nje unapunguzwa na *M&E*. Sasa ninaomba Serikali hapa Tanzania itunge haraka Sera ya ufuatiliaji na tathmini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wa sita, Serikali iuangalie mfumo wa Ajira. Mfumo wa ajira umeanza kukosa imani wanaotafuta ajira. Kila siku sasa imeanza wanaamini kwamba bila kiongozi hawezi kuajiriwa, bila Mbunge hawezi kuajiriwa, bila Waziri hawezi kuajiriwa. Mfumo huu uangaliwe vizuri ili wanaotafuta ajira warudia kuuamini, wauamini vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu wa mwisho, yametajwa sana kuhusu *MSD*, lakini mimi nataka nishauri Meja Jenerali Gabriel Sauli Mhidize ambaye ndiye Mkurugenzi Mkuu wa *MSD* ni miongoni mwa wazalendo wakubwa wachache waliowahi kupatikana Tanzania. Ninaomba Serikali isitoe uamuzi wa haraka haraka fanye uchunguzi, fanyeni uchunguzi wa kina mtagundua kwamba Jenerali Mhidize ni mzalendo ambaye anataka kusaidia watanzania. Na mkikamilisha uchunguzi huo naamini mtampa tuzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti huyu mtu amejaribu kutaka kuwasaidia wagonjwa wa figo, amekwenda mpaka kwenye viwanda anasema viwanja vinazalisha chombo ambacho kitarahisisha wagonjwa wa figo wapunguziwe gharama. Kutoka shilingi laki tano mpaka laki moja na 30. Sasa kwa nini tusimuunge mkono mtu kama huyo? Tatizo kubwa lililopo pale ni kwamba kuna wafanyabiashara ambao wanafaidika na biashara ya dawa na wana *cartel* zao ndiyo ambao wanahakikisha huyu Jenerali Mhidize hafanikiwi katika… *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Kakunda muda wako umekwisha…

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, dakika moja.

**MWENYEKITI:** Mchangiajia wetu wa mwisho atakuwa Mheshimiwa Mohamed Said Issa; namuita aweze kuchangia.

**MHE. MOHAMED SAID ISSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda nimshukuru Allah Subhanahu wa Ta’ala kwa leo kupata nafasi na mimi kuweza kuchangia katika Bunge hili tukufu katika Hotuba ya Waziri Mkuu. Lakini pia nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii ambayo ni kwa ruksa yako ndiyo naweza kuzungumza hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi mchango wangu kwanza utajikita katika biashara; na hii biashara ni katika nchi mbili hivi Zanzibar na Tanganyika, yaani Tanzania Bara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Zanzibar na Tanzania Bara tumekuwa tukitegemeana katika mambo mengine ikiwemo biashara. Tunatumia bandari zetu ya Zanzibar na Dar es Salaam.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tumsikilize mchangiaji.

**MHE. MOHAMED SAID ISSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatumia bandari zetu ambazo zipo katika Zanzibar na Tanzania Bara katika kupitisha mizigo yetu, lakini mara nyingi biashara huwa inatokea Zanzibar kuja Dar es Salaam ama Tanzania Bara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye biashara ambayo tunafanya sisi Wazanzibar au wananchi wa Zanzibar tumekuwa tukikutana na changamoto nyingi sana ambazo kwa kiasi kikubwa imeonekana inakuwa ni tatizo linalosababishwa makusudi lakini si mipango ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mipango hii mara nyingi iko vizuri, lakini watendaji ndio wanaoiharibu. Nitoe mfano kidogo. Katika suala la *declaration* ya mizigo ambayo inasafiri kutoka Zanzibar kuja Tanzania Bara, mizigo ile mara nyingi meli yetu inakuwa ni za hapo kwa hapo siyo zile Meli ambazo tayari zina *shadow*. Kwa maana hiyo wafanyabiashara ambao wanaleta mizigo wanakuwa na mizigo ambayo ni ya kushtukizwa. Kwa mfano kama kipindi hiki cha mwezi wa Ramadhan, mfanyabiashara ananunua mzigo leo anataka apakie mzigo kwenye meli lakini kwa bahati mbaya ni lazima awe ametuma ripoti mapema ili mzigo ule uweze kupakiwa na kufika kule, nje ya hapo mzigo ule ukifika meli inapigwa faini na mzigo unapigwa faini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo hii ni changamoto ambayo wafanyabiashara wa Zanzibar wanakutana nalo. lakini si hilo tu, wafanyabiashara wa Zanzibar tumekuwa tukikutana na changamoto ya mizigo ambayo inafika pale Dar es Salaam. Tunakutana na bei kubwa ya *wharfage* ambayo inakuwa inachajiwa mizigo ambayo inatoka Zanzibar. Kwa hiyo tungeomba bei ile iendane na hali halisi, hasa ukizingatia ile sehemu ambayo inashushwa ni sehemu ambayo fedha zake za kujengea pale zilitoka kwa Rais wa Kwanza wa Zanzibar Mheshimiwa Abeid Aman Karume, kwa ajili ya kuwasaidia Wanzazibar lakini leo imekuwa inawakwaza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, baada ya kuyasema hayo, ningependa kwenda kwenye hilohilo la *TRA*. Mizigo inapotoka bandarini kwenda madukani imekuwa ikisumbuliwa na *TRA* haohao ilhali

imeshafanyiwa *inspection* na kulipiwa kodi kama kawaida lakini ikifika njiani ikifika tu, ikitoka nje ya geti kuna *TRA* wengine wanajitokeza na kuwasumbua wafanyabiasha hawa na kushindwa kufanya kazi zao vizuri. Kwa hiyo hili naomba lifanyiwe kazi ili kuendeleza Muungano wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nizungumzie suala la Muungano. Katika ukurasa wa 72 Mheshimiwa Waziri Mkuu ameelezea kuudumisha, kuuenzi na kuulinda Muungano na mimi naipongeza Serikali yetu hilo ndiyo tunalolihitaji kwa sababu Muungano huu ni tunu ya taifa na sote tunaupenda. Lakini kubwa zaidi nilitaka nichangie hapa; hizi kero za Muungano ambazo zimekuwa zikifanyiwa kazi, mimi nakubaliana nazo, ni nzuri na zinasaidia kuondoa changamoto lakini bado tunatakiwa tufike kwa wananchi kujua ni changamoto gani hasa zinaweza kuulinda Muungano? Kwa sababu wananchi bado wanasema kwamba hizi changamoto ni zile zinazoikabili Serikali ya Zanzibar na Serikali ya Tanzania, siyo zinazowakabili wananchi. Kwa hiyo, baada ya kutatua changamoto hizi 11 basi turudi kwa wananchi ili na wao waseme ni lipi hasa linaweza kuimarisha Muungano wetu huu na ukawa Muungano wa mfano kama ilivyosema Hotuba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hapo, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mohamed Issa, huyu ndiye mchangiaji wetu wa mwisho Waheshimiwa Wabunge na hapa mezani kwangu nina mambo mawili. La kwanza ni Mwongozo wa Spika kama ilivyokuwa imeombwa mchana na Mheshimiwa Mbuge mwenzetu.

Mwongozo wa Spika kuhusu suala lililoembewa na Mheshimiwa Kunti Majala Mbunge kuhusu taarifa zinazotolewa na Mawaziri kuzidi dakika mbili. Waheshimiwa Wabunge leo tarehe 12 Aprili, 2022 katika kikao cha Tano cha Mkutano wa Saba wa Bunge, Mheshimiwa Kunti Majala Mbuge alisimama na kuomba Mwongozo wa Spika akitumia Kanuni ya 76 ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Juni, 2020 ambapo alisema kuwa Mawaziri wanaingilia hoja za Wabunge kwa kutumia fursa ya taarifa na kwamba wamevunja Kanuni ya 77 kwa kuzidisha muda wa dakika mbili uliyowekwa kikanuni. Hivyo, kupunguza muda wa Bunge kutoa mawazo ya kuishauri Serikali.

Waheshimiwa Wabunge ninaomba kunukuu "Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mwongozo wako ni kwa nini kitendo hiki kinaendelea kwa Mawaziri kuendelea kutumia fursa ya Kanuni ya 77 ya taarifa halafu wanachangia badala ya kutoa taarifa ndani ya muda ambao umepangwa ndani ya Kanuni." Mwisho wa kunukuu.

Waheshimiwa Wabunge, baada kupokea Mwongozo huu ilibidi kupitia taarifa rasmi za Bunge *(Hansard)* ili kupima hoja hiyo iliyotolewa na Mheshimiwa Mbunge na baadaye kuitolea Mwongozo. Waheshimiwa Wabunge Kanuni ya 77 Kifungu cha Kwanza ya Kanuni za Kudumu za Bunge

inampa fursa Mbunge yeyote kusimama mahali pake na kusema taarifa na kwa ruhusa ya Spika atatoa taarifa na ufafanuzi kwa muda wa dakika zisizozidi mbili kwa Mbunge anayesema. Waheshimiwa Wabunge naomba ninukuu; 77.-(1) Mbunge yeyote anaweza kusimama mahali pake na kusema "taarifa" na kwa ruhusa ya Spika, atatoa taarifa na ufafanuzi kwa muda wa dakika zisizozidi mbili kwa Mbunge anayesema aketi kusikiliza taarifa hiyo.

Waheshimiwa Wabunge, hivyo kwa mujibu wa Kanuni ya 77 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, muda wa kutoa taarifa ni dakika zisizozidi mbili. Waheshimiwa Wabunge nawasisitiza kuwa Mbunge anayepata fursa, narudia, nawasisitiza kuwa Mbunge anayepata fursa ya kutoa taarifa ni vyema taarifa yake ikawa ni fupi na izingatiwe muda uliowekwa kikanuni. Aidha, Waheshimiwa Mawaziri kwa kuwa nanyi ni sehemu ya Wabunge, naelekeza mnapotoa taarifa kuzingatia muda usiozidi dakika mbili kama ulivyowekwa katika Kanuni zetu. Huo ndio Mwongozo wangu leo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya Mwongozo huo jambo la pili ambalo ninaleta kwenu ni kuwakumbusha. Nawakumbusha kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu wetu Kassim Majaliwa Majaliwa, anawaalika katika Iftar leo jioni mara baada ya kuahirisha shughuli za Bunge kama tulivyotangaza awali, kwenye viwanja vyetu vya Bunge, jirani na Zahanati ya Bunge. Waheshimiwa Wabunge wote, Wafanyakazi wa Serikali pamoja ma Watumishi wa Bunge; anawakaribisha nyote.

Baada ya maelezo hayo, Waheshimiwa Wabunge nina tangazo muhimu hapa kutoka kwa Katibu wa Wabunge wa CCM katika Bunge letu, anawatangazia Wabunge wote wa CCM kukutana kwenye kikao cha *Party Caucas* kwa muda ambao mlitangaziwa hapo awali nafikiri wote mnafahamu alivyowatangazia. Kikao hicho nimeambiwa hakina waalikwa ni Wabunge wa CCM na kimsingi itakuwa baada ya Iftar, ukimbi wa Pius Msekwa. Baada ya matangazo hayo na maelezo hayo. *(Makofi)*

Naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho tarehe 13 Aprili, 2022 saa tatu asubuhi.

*(Saa 12.00 Jioni Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Jumatano, Tarehe 13 Aprili, 2022 Saa Tatu Asubuhi)*